# Nipashe

Jumanne Desemba 3, 2019 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580091

www.ippmedia.com

The Guardian digital   nipasheTZ   nipasheTZ   nipasheTZ   0745 700710




## Kichocho, minyoo tumbo tishio afya za wakazi mkoani Mwanza

UKURASA 3



Nipashe TESA

TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI

Chama cha wafanyakazi ni mkombozi wa mfumishi

Miundombinu mibovu inavyokwaza kesi GBV

Utandawazi unavyoongeza changamoto, malezi kifamilia

Jamii zilivyofaidika miradi uhimilivu tabianchi Miti 1,000,000 yapandwa, visima, mabwawa tele

UKURASA 13


## YALIYOMO

**UKURASA WA 2**

**AKANA CHADEMA KUMNUNUA SUMAYE**
MBUNGE wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, amedai mahakamani kuwa chama chake...

**UKURASA WA 4**

**SERIKALI KUHAKIKI WAKIMBIZI JIJINI DAR**
WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, leo itafanya uzinduzi wa kuhuisha takwimu...

**UKURASA WA 26**

**LUKUVI AMTUMBUA MKUU IDARA YA ARDHI**
WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemvua cheo Mkuu wa Idara...


# Mapya yaibuka vifurushi NHIF

**UKOMO** wa mgonjwa kulazwa ni mwezi mmoja hadi miwili, chanzo cha vigezo...*Endelea ukurasa wa 2*

## PAPA MSOFE KORTINI MADAI YA UHUJUMU UCHUMI

UKURASA 3



Mfanyabiashara Marijani Msofe maarufu kama 'Papa Msofe' (katikati), na wenzake wakiwa chini ya ulinzi wa askari polisi, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusomewa mashtaka ya kesi ya uhujumu uchumi. **PICHA: HELLEN MWANGO**




Scan Hapa

Fungua App ya QR code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play   App Store


## DC Sabaya arejesha eneo la Tanesco baada ya miaka 35

UKURASA 2

**MICHEZO** **MWAKINYO AMRUDIA MATUMLA, ASHUKIWA** UK. 32   **MAONI, KATUNI UK.6**

## HABARI KITAIFA

# Mapya yaibuka vifurushi NHIF

**Na Salome Kitomari**

MFUKO wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) umetaja ukomo wa muda wa mgonjwa kulazwa katika vifurushi vyake vipya vya bima ya afya.

Vifurushi hivyo ni vilivyopewa majina ya 'Najali Afya', 'Wekeza Afya' na 'Timiza Afya' vilivyozinduliwa jijini Dar es Salaam wiki iliyopita.

Akiwasilisha mada kwenye mkutano wa wahariri wa vyombo vya habari jana jijini jana, Mkurugenzi wa Huduma za Wanachama wa NHIF, Christopher Mapunda, alibainisha kuwa ukomo wa muda wa mgonjwa kulazwa ni kati ya siku 30 na 60.

Alisema huduma hizo za kulazwa zitatofautiana kutoka kifurushi kimoja hadi kingine, akibainisha kuwa kwa kifurushi cha 'Najali Afya' ambacho kiwango chake cha chini ni Sh. 240,000 kwa mtu binafsi kwa mwaka, ukomo wa kulazwa ni siku 30.

Kwa kifurushi cha 'Wekeza Afya' ambacho kiwango cha chini ni Sh. 384,000 kwa mwaka, ukomo wa kulazwa ni siku 45 na kwa kifurushi cha 'Timiza Afya' ambacho kiwango chake cha chini ni Sh. 516,000 kwa mwaka, ukomo wa muda wa kulazwa ni siku 60.

"Tumepanga siku za kulazwa kulingana na vifurushi kutokana na ukweli kwamba watu wengine wanalazwa siku nyingi ambazo siyo za lazima. Tulibaini kuwa wastani wa kila Mtanzania kwenda hospitalini ni mara mbili kwa mwaka," alisema.

Alisema vifurushi hivyo vimeeleza namna huduma za uzazi zitagharamiwa, lakini zitatolewa baada ya mwanachama kuchangia kuanzia mwaka mmoja hadi mwili.

Mkurugenzi huyo pia alisema kila kifurushi kina huduma saba ambazo mwanachama atazitapa kwenye zahanati hadi hospitali za kitaifa.

Alisema kwenye kila kifurushi, mwanachama atapata huduma za matibabu katika vituo zaidi ya 7,000 vilivyosajiliwa na NHIF ndani ya nchi, lakini ili kila mmoja kufikia lengo, ataruhusiwa kudunduliza fedha kwenye mfuko kwa miezi mitatu ndipo aanze kupata huduma za matibabu.

**NAJALI AFYA**

Mapunda alisema kifurushi hicho kinatoa fursa ya kusajili mtu zaidi ya mmoja katika familia kuendana na mahitaji ya mchangiaji.

Alitaja huduma zilizopo kuwa ni kulipiwa ada ya kujiandikisha na kumwona daktari, kulipiwa huduma ya kulazwa hadi siku 30 kwa mwaka kwa kila mwanafa-

INAENDELEA UK 8



Mamalishe akisonga ugali kwa ajili ya mlo wa mchana kwa wateja wake, katika mazingira yasiyo salama kiafya kutokana kuwa ni eneo la wazi lenye vumbi, huko Msasani, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# DC Sabaya arejesha eneo la Tanesco baada ya miaka 35

**Na Mwandishi Wetu, HAI**

MKUU wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, ameamuru kukamatwa na kuhojiwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), ofisa mstaafu wa Jeshi la Wananchi (JWTZ), Kapteni John Mushi, baada ya kudaiwa kujimilikisha isivyo halali kiwanja cha Shirika la Umeme (Tanesco) kwa miaka 35.

Imedaiwa kuwa wakati ofisa huyo akimiliki kiwanja hicho kilichoko eneo la Bomang'ombe wilayani humo, Tanesco ilikuwa inalipa kodi ya pango la ardhi ambayo kwa kipindi chote ni Sh. milioni 20.

Akiwa ameongozana na kamati yake ya ulinzi na usalama jana, Ole Sabaya alipofika katika eneo hilo, aliamuru ofisa huyo kuwekwa chini ya ulinzi wa Jeshi la Polisi kisha kumkabidhi kwa Mkuu wa Takukuru Wilaya ya Hai kwa ajili ya mahojiano ya namna alivyokipata kiwanja hicho.

"Miaka hiyo ya 1980 wakati mzee huyu (Kapt. Mushi) akiwa Mkurugenzi wa Fiber Board (bodi ya samani zitokanazo na mbao) ambayo ni taasisi ya serikali, walikuwa wakinunua magogo kutoka West Kilimanjaro.

"Kwa sababu hili ni eneo la wazi na ni eneo la umma, wakawa wanayaweka hapa. Mmenielewa? Huyu akiwa DG (Mkurugenzi Mkuu) kama ambavyo ninyi Tanesco leo mnavyoweza mkaweka nguzo katika eneo lolote la umma, ndiyo kilichokuwa kinafanyika.

"Mwaka 1982, hiyo Fiber Board ikabinafsishwa ikarudi kuwa mikononi mwa wale waliochukua, ikawa sehemu ya wamiliki ni taasisi binafsi.

"Huyu akijua kwamba hili ni eneo la umma na akijua kwamba walikuwa wanaweka magogo yao hapa, akaendelea kulihodhi hili eneo.

"Kwa hiyo, ninyi mlivyokuja kupewa Tanesco pale ukubwa wake wa jumla ilikuwa ni mita za mraba 7,271, lakini Tanesco wana 3,900, akabaki na

INAENDELEA UK 8

# Akana Chadema kumnunua Sumaye

**Na Hellen Mwango**

MBUNGE wa Iringa Mjini (Chadema), Mchungaji Peter Msigwa, amedai mahakamani kuwa chama chake hakikumnunua Waziri Mkuu wa zamani, Fredrick Sumaye, bali alijiunga kwa mapenzi yake.

Msigwa ambaye ni mshtakiwa wa pili katika kesi ya uchochezi na wenzake wanane alidai pia Mbunge wa Ukonga (CCM), Mwita Waitara, alihama chama chake (Chadema) kwa kununuliwa lakini hakushiriki kikao cha makubaliano ya kumnunua.

Kasisi huyo alitoa madai hayo jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba wakati akihojiwa na upande wa Jamhuri dhidi ya utetezi wake.

Katika kesi hiyo, Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakurugenzi wa Mashtaka Wasaidizi, Faraja Nchimbi, Joseph Pande, Wakili wa Serikali Mwandamizi Wankyo Simon na Wakili wa Serikali Jacqueline Nyantori.

Akihojiwa na Nyantori shahidi huyo wa pili wa utetezi alidai kuwa anamfahamu Sumaye kwamba alikuwa Waziri Mkuu wa Tanzania lakini kwa sasa amehamia Chadema.

Ifuatayo ni sehemu ya mahojiano yao;

**Nyantori:** Mchungaji unasema wewe ni mtumishi kwa hiyo utaongea ukweli na uko chini ya kiapo sahihi?

**Msigwa:** Ndiyo.

**Nyantori:** Unamfahamu Sumaye?

**Msigwa:** Ndiyo ninamfahamu.

**Nyantori:** Yuko wapi kwa sasa?

**Msigwa:** Kwa sasa ni mwanachama wa Chadema.

**Nyantori:** Je, Chadema mlimnunua Sumaye kwa shilingi ngapi?

**Msigwa:** Chadema hatuna hela hatukumnunua Sumaye bali alikuja kwa **mapenzi** yake.

**Nyantori:** Umesema Waitara alinunuliwa na Chama Cha Mapinduzi, alinunuliwa kwa shilingi ngapi?

**Msigwa:** Sijui, ila najua

INAENDELEA UK 8


## HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA

## TANGAZO LA UUZAJI WA VIWANJA

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma anawatangazia Wananchi wote kuwa zoezi la upimaji wa viwanja limekamilika na kuanzia **TAREHE 3/12/2019** viwanja vitaanza kuuzwa kila siku za Jumatatu hadi Ijumaa katika eneo la wazi la Manispaa ya zamani (karibu na Sabasaba) kuanzia saa 2 Asubuhi hadi saa 9.30 Alasiri.

**Viwanja vinavyouzwa ni katika maeneo ya:**

| ENEO | MATUMIZI NA BEI TSHS KWA (SQM1) |
|---|---|
| NALA (Karibu na Chuo cha IFM na Kituo cha kupaki Malori) | • Makazi 4,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| CHAHWA (Karibu na Ikulu) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| Mahoma Makulu (Nyuma ya Mji wa Serikali) | • Makazi 3,000/=<br>• Makazi na Biashara 5,000/= |
| KIKOMBO (Karibu na Bandari kavu na Makao Makuu ya Ulinzi ya Taifa) | • Makazi 2,000/=<br>• Makazi na Biashara 3,500/= |
| MTUMBA (Karibu na Mji wa Serikali na Ikulu) | • ZONE I Makazi 8,000/= Makazi na Biashara 8,500/=<br>• ZONE II Makazi 6,000/= Makazi na Biashara 7,500/=<br>• ZONE III Makazi 3,000/= Makazi na Biashara 5,500/= |

**NB: Malipo yote yafanyike ndani ya Siku 90 baada ya kupata hati ya madai.**

***Kwa mawasiliano zaidi piga simu namba 0714 785513.***

**Tangazo hili limetolewa na:**
**Mkurugenzi wa Jiji,**
**DODOMA**

215542002

## HABARI KITAIFA

# Papa Msofe kortini tuhuma uhujumu uchumi

**Na Hellen Mwango**

WAFANYABIASHARA wanne akiwamo Marijan Msofe (53), maarufu kama 'Papa Msofe' na Wakili wa Kujitegemea, Mwesigwa Mhingo (36), wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa kesi ya uhujumu uchumi ikiwamo kuratibu genge la uhalifu na kutakatisha Dola za Marekani 410,000 (sawa na Sh. milioni 943).

Mbali na Papa Msofe na Mhingo, washtakiwa wengine ni Wenceslaus Mtui (49), Josephine Haule (38) na Fadhili Mganga (61).

Washtakiwa hao walisomewa mashtaka yao mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi, anayesikiliza kesi hiyo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam.

Upande wa Jamhuri uliongozwa na Wakili wa Serikali Mkuu Maternus Marandu, Wakili wa Serikali Mwandamizi Ladislaus Komanya na Wakili wa Serikali Glory Mwenda.

Komanya alidai kuwa katika tarehe tofauti kati ya Desemba 2018 na Septemba, mwaka huu, washtakiwa wote kwa pamoja na wenzao ambao hawajakamatwa walifanya mpango wa kuongoza genge la uhalifu.

Katika shtaka la pili, ilidaiwa kuwa kati ya Desemba, mwaka jana na Septemba, mwaka huu, washtakiwa wote, mahali tofauti, walitakatisha Dola za Marekani 300,000 (sawa na Sh.milioni 690) kutoka kwa Pascal Jean Camille.

Shtaka la tatu, ilidaiwa kuwa siku ya tukio la pili, washtakiwa wakiwa wa nia ovu, walijipatia kwa njia ya udanganyifu Dola za Marekani 300,000 kutoka kwa Camille baada ya kumdanganya kuwa wangemuuzia kilo 200 za madini aina ya dhahabu na kuyasafirisha kwenda Ureno, huku wakijua si kweli.

Upande wa Jamhuri ulidai katika shtaka la nne, katika tarehe tofauti kati ya Desemba mwaka jana na Septemba mwaka huu washtakiwa walitakatisha

INAENDELEA UK 8




Mwakilishi wa Tanzania Election Alliance (TanEA), Wallace Mayunga, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitoa taarifa ya awali ya utazamaji wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019, uliofanyika hivi karibuni. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Kichocho, minyoo tishio Mwanza

**Na Anthony Gervas, MWANZA**

UGONJWA wa kichocho na minyoo ya tumbo vimetajwa kuwa tisho katika Mkoa wa Mwanza, huku Wilaya ya Ukerewe ikiongoza kwa maambukizi.

Hayo yalibainishwa na Mratibu wa Magonjwa yasiyopewa Kipaumbele mkoani Mwanza, Dk. Mabai Thobias, katika mahojiano maalum na Nipashe jijini humo mwishoni mwa wiki.

"Takwimu kutoka katika vituo vya kukusanyia taarifa za afya mkoani Mwanza, mwaka 2018 zinaonyesha watu waliokuwa wameathirika na ugonjwa wa kichocho pekee, Wilaya ya Ukerewe watu 1,765, Buchosa 1,000, Nyamagana 600 na Ilemela 572.

"Ugonjwa wa kichocho upo, hakuna wilaya iliyo salama katika Mkoa wa Mwanza, Ilemela na Nyamagana zaidi ya asilimia 80 kuna kichocho na iligundulika katika utafiti wa afya kuwa jamii inayoishi kando ya Ziwa Victoria iko hatarini zaidi. Kati ya watu 10, wanane au saba wanakuwa wameathirika," alibainisha.

Kwa upande wa minyoo, Dk. Thobias alisema: Mkoa wa Mwanza mwaka jana ulikuwa na wagonjwa 17,000, Ilemela ilikuwa na zaidi ya wagonjwa 9,000, Ukerewe zaidi 7,000, Sengerema zaidi ya 5,000 na Buchosa zaidi watu 5,000."

Alisema kwa ujumla, wilaya zote za mkoa huo ambazo ni Ilemela, Nyamagana, Magu, Misungwi, Sengerema, Buchosa na Kwimba watu wake wameathirika na magonjwa ya kichocho na minyoo ya tumbo.

"Kundi linaloathirika zaidi na ugonjwa wa minyoo ya tumbo ni watoto wenye umri wa kwenda shule kuanzia miaka mitano hadi watu wazima miaka 60.

"Tatizo hili linachagizwa na kutumia vyakula visivyokuwa salama, hasa kachumbali, karoti, kabichi na kutonawa mikono watu wanapotoka kujisaidia chooni, kutembea peku na kutokuwa na vyoo," alisema.

Akifafanua zaidi kuhusu kichocho, Dk. Thobias alisema kinasababishwa na vimelea vya Schistosoma ambavyo vinaenezwa na konokono.

Alisema ugonjwa huo uko katika aina mbili ambazo ni kichocho cha tumbo na kichocho cha kibofu cha mkojo.

Alisema maambukizi ya ugonjwa huo kuenezwa na konokono, akibainisha kuwa binadamu anapokwenda kujisaidia haja ndogo au kubwa katika vyanzo mbalimbali vya maji, kama ana ugonjwa huo, huacha mayai yake katika vyanzo hivyo na baadaye hupevuliwa na konokono.

Alisema kuwa baada ya kupevuliwa mayai hayo na husambaa ndani ya maji, hivyo yakitumiwa na binadamu, anapata maambukizi ya ugonjwa huo.

Dk. Thobias alisema dalili za ugonjwa huo ni pamoja na kuumwa tumbo na kukojoa damu na kwamba mgonjwa akichelewa kupata matibabu, huathirika kwa mfumo mzima wa chakula ndani ya tumbo, kupata kansa ya kibofu cha mkojo na hata kupoteza maisha.

Mtaalamu huyo wa afya alisema wavuvi wa Ziwa Victoria ndiyo kundi lililoko katika hatari zaidi ya kuathirika kwa kichocho kutokana na shughuli zao za kukaa kwenye maji kwa muda mrefu.

Dk. Thobias aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kuzingatia kanuni za afya kwa kwenda kupima afya zao mara kwa mara na kuachana na kasumba ya kubuni matibabu wakiwa nyumbani kwa dawa za miti shamba.


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe: ps@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Moshi,
S.L.P. 2888,
40470DODOMA,
25 - 11 - 2019

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Jumanne tarehe **03 – 12 – 2019** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd.** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam kuelekea Kabanga,** gari hizo zenye namba za usajili:

   **T 221 BYM / T 837 DJB**
   **T 245 BXH / T 387 DHQ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | **mita** | **25** |
| **Upana** | - | **mita** | **4.10** |
| **Kimo** | - | **mita** | **5.2** |

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam Port hadi Kabanga Kupitia Dodoma,** gari litasafiri muda wa mchana tu **(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)**

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

215542302



中国水电
SINOHYDRO

**JOB ANNOUNCEMENTS**

We are **SINOHYDRO CORPORATION LIMITED,** currently implementing the Zanzibar Irrigation Infrastructure Construction Project both at Unguja and Pemba.

We are recruiting heavy equipment **operators, truck drivers, electricians, fitters, concrete workers, steel bar workers, and experienced worker of** all related disciplines.

We are sourcing **fuels, steel bars, cement, aggregates, rip rap stones, geotextiles, PE/PVC pipes, steel pipes, scaffoldings, and various other materials.**

We are also in need of small machines, tools, and equipment.

**Kindly send your application/quotation to Mr. Yan at yyg608@163.com or call 0778 460047.**

115529602

# Serikali kuhakiki wakimbizi jijini Dar

**"Uhuishaji takwimu utahusisha wakimbizi wote waishio Dar es Salaam wenye nyaraka, walioruhusiwa kuishi nje ya kambi za wakimbizi na maeneo mengine kuanzia saa 2 asubuhi," ilifafanua taarifa hiyo.**

**Na Mwandishi Wetu**

WIZARA ya Mambo ya Ndani ya Nchi kupitia Idara ya Huduma kwa Wakimbizi, leo itafanya uzinduzi wa kuhuisha takwimu za wakimbizi waishio jijini Dar es Salaam.

Taarifa iliyotolewa na Idara ya Huduma kwa Wakimbizi katika Wizara hiyo imefafanua kuwa, uhakiki huo utafanywa na idara hiyo kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR).

Taarifa hiyo ilieleza jana kuwa uzinduzi huo utafanyika katika Ukumbi wa Maofisa wa Polisi, Oysterbay, jijini.

"Uhuishaji takwimu utahusisha wakimbizi wote waishio Dar es Salaam wenye nyaraka, walioruhusiwa kuishi nje ya kambi za wakimbizi na maeneo mengine kuanzia saa 2 asubuhi," ilifafanua taarifa hiyo.

Kwa mujibu wa taarifa hiyo, baada ya uzinduzi uhuishaji takwimu utafanyika katika Ofisi za Shirika la Relief of Development Society (REDOSO).

Ofisi hizo zipo Kinondoni, Biafra ambapo wakazi, waombaji hifadhi wote pamoja na familia zao, wanapaswa kufika ili kuhuisha takwimu zao bila kukosa.

Taarifa iliongeza kuwa mkimbizi yeyote ambaye hatajitokeza wakati wote wa uhuishaji takwimu, taarifa zake hazitahuishwa na usajili wake utasitishwa.

Wakimbizi hao wametakiwa kufika na nyaraka za utambulisho zikiwamo barua ya uthibitisho wa mkimbizi, usajili, kibali cha kuishi nje ya kambi, vyeti vya kuzaliwa.

Nyaraka nyingine ni vyeti vya ndoa, hati ya kusafiria, vitambulisho vya kazi, shule, chuo na nyaraka nyingine yoyote inayomtambulisha mkimbizi ambayo inatambulika kisheria.

"Shughuli zote zinazohusiana na uhakiki wa taarifa za mkimbizi na waomba hifadhi zinatolewa bure.

"Uhuishaji huu hautahusisha wakimbizi wa mwaka 1972 wanaotoka makazi ya Ulyankulu, Katumba, Mishano na waishio vijijini mkoani Kigoma," ilieleza taarifa hiyo.



Waziri wa Mambo ya Ndani, Kangi Lugola (katikati), Waziri wa Mambo ya Ndani wa Burundi, Pascal Barandagiye (kushoto) na Kamishna Msaidizi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Wakimbizi (UNHCR), George Okoth Obbo, wakibadilishana makabrasha, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kusaini mkataba unaohusu makubaliano katika kuhakikisha urejeshwaji wa wakimbizi wa Burundi wanaotaka kurejeshwa kwa hiyari.. **PICHA: WMNN**

# Wanaoishi VVU walalamika kunyanyapaliwa biashara

**Na Beatrice Shayo**

WANAWAKE wanaoishi na virusi vya Ukimwi wamelalamikia kitendo cha kunyanyapaliwa katika biashara zao za mamalishe na kuwalazimu kubadili biashara zao kwenda kwenye ufugaji.

Katibu wa Chama cha Wajane wanaoishi na virusi vya Ukimwi, Caroline Domiani, alitoa malalamiko hayo wakati wa halfa ya kuwachangia wajasiriamali hao ili wawe na maendeleo ya kiuchumi.

"Changamoto ni sisi ambao tunafanya biashara ya mama lishe watu wengi wanatukwepa kuja kununua biashara zetu yaani wanaona kama vyakula vyetu tunavyovipika vinakuwa na maambukizi ni kutunyanyapaa hakuna jingine na hii inachangiwa na ukosefu wa elimu," alisema.

Domiani alisema hali hiyo imemwathiri kwa kiasi kikubwa na kuamua kubadilisha biashara kwenda katika ufugaji wa kuku.

"Hata ndugu zangu upande wa mume walininyanyapaa hadi sasa sina mawasiliano nao nilikuwa naumia kila siku kunyanyapaliwa nikaamua kujitegemea mwenyewe na watoto wangu watatu," alisema.

Alipendekeza elimu iwe inatolewa ya kutosha hadi vijijini na maeneo ya pembezoni ili watambue mwenye virusi vya Ukimwi si mtu wa kufa ama hastaili kufanya biashara.

"Kama napika chakula kwa usafi kwa nini usije kununua chakula change, Ukimwi haukai kwenye chakula labda kama nina vidonda na wewe una vidonda ndio kutakuwa na tatizo, lakini kama mimi ni mzima siwezi kukuambukiza hapa ni elimu inatakiwa ili watu waache kutunyanyapaa," alisema.

Naye Maricela Peter alisema, anafanya biashara ya nyanya na karanga za kusaga na hukutana na changamoto kubwa ya kunyanyapaliwa hata anapoingia kwenye vikundi vya kuweka (Vikoba) huonekana mtu asiyeweza kutoa fedha.

"Wanatuona hatuna uwezo, ukipika hata maandalizi wanatupita na kwenda kununua kwa wengine kwa vile tunaishi na virusi vya Ukimwi mimi ni muwazi na pia huwa nawaelimisha wenzangu kuhusu huu ugonjwa ukiz

INAENDELEA UK 8

# Vyuo vya fedha vyatakiwa viwango kimataifa

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango, amevitaka vyuo vya fedha nchini kutoa elimu inayoendana na viwango vya kimataifa ili kukidhi mahitaji ya soko la dunia na ukuaji wa uchumi.

Dk. Mpango aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika mahafali ya 45 ya Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM), ambayo mgeni rasmi alikuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa.

Alisema chuo cha IFM ni cha mfano katika kufikia malengo hayo na kwamba serikali inaendelea kukifadhili chuo hicho ili kuzalisha watalaam wenye vigezo vya kufikia malengo ya nchi katika kukuza uchumi wa taifa.

"Hivyo naendelea kusisitiza tena, jukumu la chuo hiki ni kutoa wahitimu wenye weledi na ujuzi wa hali ya juu. Lakini wawe wazalendo kweli kwa nchi yetu, wanaochukia rushwa, ufisadi na waliodhamiria kutoa mchango mkubwa kwa nchi yetu," alisema Mpango.

Dk. Mpango alisema serikali inatambua umuhimu wa chuo hicho na kwamba itaendelea kukijengea uwezo, kuboresha miundombinu na kuongeza rasilimali watu ili kuendelea kutekeleza malengo yake kwa ufanisi. Alisema katika nchi zilizoendelea kwa kasi walikuwa na mifumo madhubuti ya usimamizi wa fedha katika serikali, taasisi za umma, benki na bima hivyo Tanzania inatakiwa kuiga mfano.

Aliahidi kuwa serikali itaendelea kulipa mishahara ya watumishi wa chuo hicho ambayo ni Sh. bilioni 11 ambazo Hazina wanazilipa kila mwaka.

Naye Kaimu Mkuu wa chuo hicho, Dk. Immanuel Mvaza, alisema ili serikali iweze kufikia lengo la kukuza uchumi wa viwanda ifikapo 2020, wanahitajika watalaam wa kutosha wa biashara za kimataifa kutoka chuo hicho.

Alisema kwa miaka 19 wanashirikiana na Chuo Kikuu cha Biashara za Kimataifa cha India (IIFT), kwa ajili ya kuzalisha wataalam wa usimamizi wa biashara za kimataifa ambao watawezesha kufikia lengo hilo la kukuza uchumi.


KDF Kilimanjaro Development Forum Today. Tomorrow. Together

P.O Box 32055,
Dar es Salaam, Tanzania
+255 688 591 182
john@stageneraltz.com
www. kilimanjarodevforum.co.tz

MKUTANO MKUU WA MWAKA WA WANACHAMA

Wanachama wa KDF wanatangaziwa kwamba kutakuwa na mkutano mkuu wa mwaka wa wanachama wote utakaofanyika tarehe 21, Desemba, 2019 katika ukumbi wa ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Manispaa ya Moshi.

**Agenda:**
1. Kupokea taarifa ya maendeleo ya KDF;
2. Kupokea na kupitia taarifa ya fedha ya KDF;
3. Kuchagua maafisa wa KDF na wajumbe wa bodi ya uongozi;
4. Kuteua wakaguzi na wadhamini au kuwathibitisha wanaoendelea;
5. Kupanga michango/ada za mwaka unaofuata, na
6. Kupitia na kupitisha marekebisho ya katiba.

**Uchaguzi wa viongozi katika nafasi zifuatazo;**
1. Mwenyekiti
2. Makamu Mwenyekiti
3. Katibu
4. Naibu Katibu
5. Mweka Hazina
6. Mweka Hazina Msaidizi

**Maombi ya kugombea nafasi hizi yatumwe kwa anwani zifuatazo:**
Dr. Jonas Kipokola,
Katibu (KDF),
S.L.P 8448, Moshi au barua pepe
info@kilimanjarodevelopmentforum.org au piga simu 0754386003
Tarehe ya mwisho ya kupokea maombi ya kugombea ni tarehe 7 Desemba, 2019.

Mkutano Mkuu utafuatiwa na sherehe ya Kilimanjaro Day itakayofanyika siku hiyo hiyo. Umoja wetu ndiyo nguvu ya mafanikio yetu, karibuni sana

Imetolewa na:
Dr. Jonas Kipokola
Katibu, Kilimanjaro Development Forum

615528802

## HABARI KITAIFA

# ‘Udhibiti Ukimwi usitegemee wahisani wa nje’

**Na Elizabeth Faustine,**

**MWANZA**

SERIKALI imetakiwa kuhamasisha kampuni kubwa nchini kuchangia Mfuko wa Taifa wa Kudhibiti Ukimwi ili kuepuka utegemezi kwa wahisani nje ya nchi.

Meneja wa Mgodi wa Geita Gold Mine (GGM), kitengo cha afya, usalama na mazingira, Dk. Kiva Mvungi, alisema hayo wakati akizungumza na waandishi wa habari katika kilele cha maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika jijini Mwanza.

Dk. Mvungi alisema ili kufanikisha mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi lazima kuwapo na juhudi na nia kwa wanasiasa ya kuongeza mapato katika mfuko huo.

“Ni vyema serikali ihamasishe kampuni kubwa kama za simu, usafirishaji, uzalishaji na mengine,” alisema.

Dk. Mvungi alisema mgodi huo wenye wafanyakazi karibu 5,000 una sera na miongozo mbalimbali kwa wafanyakazi ikiwamo kutoa elimu, kupima afya bure na kutoa huduma ya matibabu kwa wenye maambukizi ya virusi vya Ukimwi.

Mgodi huo unatoa Sh. milioni 750 kila mwaka ukishirikiana na Tume ya Kudhibiti Ukimwi nchini (Tacaids) kwa ajili ya kupambana na Ukimwi na Sh. milioni 250 kati ya hizo zinaingizwa katika Mfuko wa Taifa wa Ukimwi.

Mkurugenzi wa Tacaids, Dk. Leonard Maboko, alisema mchango wa wadau ni muhimu kuwezesha mapambano hayo na uzinduzi wa maadhimisho hayo ulianza kwa matembezi ya hisani yaliyoongozwa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella na kupatikana Sh. 570,000.

Akitoa tathmini ya upimaji uliofanyika tangu kuanza kwa maadhimisho hayo, Novemba 25, mwaka huu hadi siku ya kilele Desemba Mosi, Dk. Maboko alisema watu 2,265 walipima virusi vya Ukimwi.

Dk. Maboko alizishukuru taasisi zote, vyombo vya habari na kampuni zinazoshirikiana nao katika mapambano dhidi ya virusi vya Ukimwi wakiwamo GGM ambao kwa miaka 17 wamechangia fedha kupitia mradi wa Kilimanjaro HIV& AIDS Challenge, zaidi ya Dola za Marekani bilioni tano (sawa Sh. trilioni 11) kwa ajili ya kufanikisha mapambano hayo.




Baadhi ya wahitimu katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), wakiwa kwenye mahafali ya 17 ya chuo hicho, yaliyofanyika jijini Dar es Salaam wikiendi. Waliohitimu ni wa fani za udaktari, uuguzi na ustawi wa jamii. **PICHA: ROMANA MALLYA**

# Bil. 216/- zawekezwa Mfuko wa Umoja

**Na Beatrice Philemon**

JUMLA ya Sh. bilioni 216 zimewekezwa katika Mfuko wa Umoja (Umoja Fund) na wawekezaji nchini kupitia Kampuni ya Uwekezaji ya UTT AMIS kuanzia Mei 2005 ulipozinduliwa hadi Juni mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Mkurugenzi wa Uwekezaji wa Mfuko wa Umoja, Pamela Nchimbi, katika mkutano mkuu wa mwaka uliwashirikisha wawekezaji kutoka maeneo mbalimbali nchini ili kupata taarifa kuhusu mifuko yote ya UTT AMIS inavyoendeshwa, kupata taarifa za hesabu na kujadili changamoto zilizopo katika uendeshaji na namna ya kuzitatua.

Alisema Mfuko wa Umoja ni mfuko wa kwanza kuanzishwa na UTT AMIS, mfuko umeendelea kufanya vizuri kwa miaka 14 mfululizo.

Katika kipindi cha miaka minne mfululizo kuanzia Juni 2015 hadi Juni, 2019, ukubwa wa Mfuko wa Umoja umekuwa ukipanda na kushuka.

Juni 2019, ukubwa wa Mfuko wa Umoja uliongezeka kwa Sh. bilioni nne kutoka Sh. bilioni 212 kama ilivyokuwa Juni 2015 hadi Sh. bilioni 216, Juni 2019.

Vile vile, thamani ya kipande (NAV) iliongezeka hadi Sh. milioni 576.92 kutoka Sh. milioni 455.50 mnamo Juni 2015 ambayo ni sawa na ongezeko la asilimia 27.00 .

Akielezea faida ya mfuko, alisema faida kwa miaka minne kwa wastani ilikuwa asilimia 6.44.

Mwaka 2016 faida ilikuwa asilimia sita, mwaka 2017 faida ilikuwa asilimia 6.6, mwaka 2018 faida ilikuwa asilimia 14.45 na mwaka 2019 faida ilishuka mpaka asilimia 1.29.

Mpaka sasa faida jumuishi ya mfuko tangu kuanzishwa ni asilimia 13.42, ingawa kumekuwapo na changamoto kadha katika soko la hisa.

Kupanda na kushuka kwa faida na thamani ya kipande cha Mfuko wa Umoja imesababishwa na mdororo katika soko la hisa.

“Mwekezaji yeyote anayetaka kuwekeza kupitia mfuko wa Umoja, unaruhusu mwekezaji wake kuuza vipande kwa wakati wowote, hivyo kumpa fursa mwekezaji kupata faida anapozihitaji na hakuna kiwango cha chini cha uwekezaji kinachoruhusu kupata faida,” alisema Pamela.

Mwenyekiti wa Bodi ya Kampuni ya UTT AMIS, Casmir Kyuki, alisema ili kuwahudumia wawekezaji kwa njia rahisi zaidi na kupanua wigo kwa wawekezaji, UTT AMIS imezindua mfumo mpya wa Tehama unaojulikana kama ‘UTT AMIS APP’ ili kusaidia wawekezaji kununua vipande kwa njia ya simu badala ya kwenda katika ofisi za UTT AMIS kupata huduma.

“Kupitia mfumo huu mwekezaji ataweza kutumia simu kiganjani (mobile devices) kupata taarifa za bei ya kipande, kununua kipande kwa simu ya kiganjani, taarifa za uwekezaji, taarifa zote za mifuko ya UTT AMIS, thamani ya kipande cha mfuko wowote na pia kupata taarifa fupi ya akaunti yako (last five transactions) ikiwemo uwekezaji wako,” alisema.

Ili kupata huduma hii kupitia UTT AMIS APP, mwekezaji lazima ajiunge na huduma ya simu ili aweze kupata huduma hii kwenye kiganja.

Alieleza kuwa kupitia mfumo huu wawekezaji wanaotumia mtandao wa Tigo-Pesa, M-Pesa, Airtel Money, T-Pesa, Halopesa wataweza kununua vipande kupitia simu zao.

Vile vile, maboresho zaidi yanaendelea ili kuwawezesha watumiaji wa simu za kisasa (smart phone) kupata huduma kwa urahisi zaidi na kwa kuanzia mifumo ya UTT AMIS, imeunganishwa na mifumo ya benki ya CRDB ambayo pia ni msimamizi wa mifuko.

Faida katika mfuko imekuwa juu ya kigezo linganishi ikiwa ni wastani wa faida ya asilimia kuni kwa miaka mitano iliyopita.

Pia katika kipindi hicho chote thamani ya mfuko imeendelea kukua pamoja na idadi ya wawekezaji kuongezeka kutokana na kuongezeka kwa imani na uelewa kuhusu mifuko ya uwekezaji wa pamoja.


## UBALOZI WA MAREKANI NA UINGEREZA DAR ES SALAAM

## MNADA WA HADHARA:

**UNIVERSAL AUCTION CENTRE** Kwa idhini waliyopewa na **Ubalozi wa Marekani na Uingereza** watauza kwa mnada wa hadhara Funicha za nyumbani, Magari na Magenereta tarehe 7 December, 2019 Jumamosi kuanzia saa 4:00 asubuhi. Mnada utafanyika Golden Resort Sinza, Lion Street.

**Fenicha na Computer zitaanza kuuzwa kuanzia saa 4:00** asubuhi: Sofa set, China base, Hutch, Chest drawer, Dresser, Credenza, Coffee table, Dining table, Book case, Conference table, Office desk, Chairs, Carpet, Vitanda, Magodoro, Fridge double door, Freezer, Washer, Dryer, Gas & electric cooker, A/c split units, Photocopy m/c, TV set, Video camera set, Computer set, Air compressor, Water pump na vingine vingi.

**Magari na genereta yataanza kuuzwa kuanzia saa 6:00 mchana:**

| Idadi | Aina | Model | Mwaka | Ushuru |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Mercedes Benz Station Wagon | ML 270 Diesel Engine | 2007 | Haujalipwa |
| 1 | Hyster Electric Fork Lift 2 Tons | E50XM2-27 | 2012 | Haujalipwa |
| 4 | Generator 40 & 50 KVA | Perkins Diesel Engine | 2007/2009 | Haujalipwa |
| 12 | Digital Voltage Stabilizer 80 KVA | 3 Phase 415 Volts | - | Haujalipwa |
| 2 | JLG Electric Ladder (175kgs.Capacity) | 25EL(Lifting height25fts) | 2003 | Haujalipwa |
| 1 | Mercedes Benz Saloon | WDB20 Diesel Engine | 2002 | Umelipwa |
| 1 | Toyota Rav 4 Station Wagon | SXA11 Petrol Engine | 1997 | Umelipwa |

Mali zote zinaweza kukaguliwa Golden Resort Sinza,Lion Street kuanzia tarehe 4 mpaka 6 December, 2019, kuanzia saa 4:00 asubuhi mpaka saa 11:00 jioni.

**MASHARTI YA MNADA.**

1. Mnunuzi wa Fanicha atatakiwa kulipa malipo yote kwa keshia (cashier). Na mnunuzi wa Gari atatakiwa kulipa 25% pale pale na salio lilipwe ndani ya siku 4 za kazi mwisho wa kulipa tarehe 13 December, 2019 Saa 10:00 jioni. Ukishindwa kulipa kwa muda huo Gari au Genereta litauzwa kwa mshindi mwingine aliyefata na dhamana haitarudishwa.
2. Malipo kwa njia ya **VISA na Master cards za bank ya CRDB** yanakubalika.
3. Mali zote zitauzwa kama zilivyo bila dhamana.
4. Mnunuzi atawajibika kulipa ushuru na kodi zingine zote.
5. Mali yote iliyouzwa itatakiwa kuondolewa baada ya kulipa malipo yote pamoja na kodi
6. Kila mtu **atatakiwa lazima kuwa na bid** namba itakayopatikana getini.

**Kwa maelezo zaidi waone:**
**UNIVERSAL AUCTION CENTRE**
**PLOT NO: 5 “E” LION STREET SINZA DAR ES SALAAM**
**CELL NO: 0754 284 926, 0759 284 926**
**E-mail: universalauction@hotmail.com**
**Insta: universalauctioncentre**

115541002

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Vijana wajitambue, wachukue tahadhari maambukizo ya VVU

Maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani kwa mwaka huu, yameacha ujumbe mzito kwa vijana wetu nchini, kwamba wanakabiliwa na hatari kubwa ya kuambukizwa Virusi vya Ukimwi (VVU).

Kwa kijana makini anayejitambua na thamani ya maisha yake binafsi na kwa taifa, bila shaka akisoma takwimu zilizotolewa wakati wa maadhimisho ya mwaka huu jijini Mwanza Jumapili, atatanya tafakuri na kujitathmini kuhusu maisha yake.

Kimsingi, kundi la vijana hasa wa kike linadaiwa kuongoza kwa kuwa na maambukizi mapya ya VVU kwa mujibu wa takwimu za maambukizi ya virusi hivyo kwa mwaka 2016/2017.

Akizungumza katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika katika Uwanja wa Rock City Mall jijini Mwanza, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema katika maambukizi mapya 72,000 vijana ni asilimia 40 na kati ya hao asilimia 80 ni wa kike.

Takwimu hizi zinadhihirisha kuwa kundi la vijana hasa wa kike ndilo linaloonekana kuwa kwenye hatari kubwa ya kupata maambukizi mapya ya VVU.

Waziri Mhagama alisema miongoni mwa sababu ni pamoja na ngono zembe katika umri mdogo, hali inayosababisha mhusika kuwa na wapenzi wengi, inayojenga hatari ya kupata maambukizi mapya ya virusi vya Ukimwi.

Alisema serikali kwa kushirikiana na wadau wamejitoa kuelimisha umma hasa kwenye mikusanyiko ili kupunguza maambukizi mapya katika jamii.

Aliwasihi watu wanaoishi na virusi hivyo kuendelea kutumia dawa na wanaume kuacha kuwarubuni vijana wadogo kwa lengo la kufanya nao mapenzi.

Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, alisema wameshusha umri wa vijana kupima maambukizi ya VVU bila kupata ridhaa ya mzazi au mlezi kutoka miaka 18 hadi miaka 15 na kuwasihi vijana kupima afya zao ili wapate kufahamu na watakaobainika kuwa na maambukizi kuanza dawa mapema.

Tunaunga mkono jitihada zinazofanywa na serikali katika kupunguza kama siyo kutokomeza maambukizi ya VVU ikiwamo kutoa elimu kwa umma.

Hata hivyo, takwimu zilizotolewa Jumapili zinatufanya tuwaone vijana kuwa sasa ndio wananyemelewa na hatari ya VVU na Ukimwi. Hivyo tunawashauri kushtushwa na takwimu hizo na kuchukua hatua ya kujilinda dhidi ya kasi hii kubwa ya maambukizi.

Tahadhari iwe kujitambua kuwa wao ndio nguvu kazi ya familia na taifa kwa ujumla hususan kutojiingiza kwenye ulevi, dawa za kulevya pamoja na kufanya ngono zembe.

Takwimu hizi mpya pia zinaonyesha jinsi wasichana walivyo katika hatari zaidi ya kuambukizwa VVU na Ukimwi kwa kuwa zinaeleza kuwa asilimia 80 ya vijana wanaoambukizwa ni wasichana.


Hii ina maana kubwa, kiasi cha kutufanya Nipashe kuitafsiri hali hii kuwa wasichana wengi ni wepesi wa kurubuniwa na wanaume na kufanya nao ngono bila tahadhari; kwa maana ya kutotumia kondomu.

Na vilevile, inatushawishi kuamini kuwa wasichama wengi wa umri huo wanajihusisha na biashara ya ngono, na wanakosa msimamo wa kuwakatalia wanaume wanapowashawishi au kuwalazimisha kufanya nao ngomo bila kinga.

Ni wakati mwafaka sasa kwa vijana wote kutambua kuwa Ukimwi unaua, na ni ugonjwa ambao hadi sasa hauna kinga wala tiba, na njia pekee ya kuepukana nao ni kuchukua tahadhari. Hivyo hawanabudi kuchukua hatua sasa.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Ubora wa elimu ya awali utaondoa mbumbumbu

**ELIMU** ya awali ni nguzo muhimu katika kumjengea mtoto uwezo wa kusoma, kuandika na kuhesabu (KKK) ili wanapoingia darasa la kwanza awe tayari ameandaliwa kikamilifu, katika maeneo hayo matatu muhimu.

Kutokana na umuhimu huo, serikali inahimiza kila shule ya msingi iwe na darasa la elimu ya awali au shule shikizi, ambazo majengo yake yanajengwa kwa nguvu za wananchi.

Miongoni mwa maeneo ambayo kasi ya ujenzi wa shule hizo imepamba moto ni kwenye vijiji mbalimbali vya Musoma mkoani Mara, ambako wananchi wanajitolea kwa hali na mali ili kufanikisha ujenzi huo.

Wanafanya hivyo kuitikia maelekezo ya serikali ya kuhakikisha kila shule ya msingi inakuwa na darasa la shule ya awali kwa ajili ya kuwanoa watoto wanaojiandaa kuingia darasa la kwanza.

Musoma Vijijini ina vijiji 68 na karibu vijiji vyote wananchi wanaendelea na ujenzi wa majengo ya shule shikizi, hatua ambayo itawezesha watoto wote kupata elimu ya awali.

Ujenzi huo unaendelea kila kijiji, kutokana na ukweli kwamba elimu ya awali ni msingi muhimu, kwani elimu ya baadaye inategemea kwa kiasi kikubwa mafanikio ya elimu hiyo.

Kuwapo kwa madarasa hayo ni fursa kwa watoto wote wakiwamo wanaotoka familia duni zisizo za uwezo wa kupeleka watoto katika shule za awali za kulipia, hivyo ni muhimu kuunga mkono ujenzi huo.

"Tunataka kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule shikizi, ndiyo maana tunahamasisha wananchi wetu kushiriki kwa hali na mali, katika ujenzi wa shule hizi muhimu," Prof. Sospeter Muhongo anasema.

Profesa Muhongo ni Mbunge wa Musoma Vijijini, anasema wananchi wake wameitikia maelekezo ya serikali, kwa kutambua kuwa elimu ndiyo kila kitu, hivyo hawana budi kuhakikisha wanakuwa na shule shikizi.

Kimsingi ni kwamba nyumba imara inahitaji msingi uliokamilika, hii ikihusisha mahitaji yote muhimu kuanzia msingi bora na imara uliojengwa na fundi mwenye weledi wa hali ya juu, akizingatia ubora vifaa anavyotumia.

Iwapo hilo halitafuatwa katika kujenga msingi imara, nyumba itaanguka wakati wowote na inawezekana ikaanguka wakati ujenzi ukiendelea au miaka michache baada ya ujenzi kukamilika.

Hivyo ndivyo ilivyo hasa kwenye elimu, kwamba elimu ya awali iliyo bora ndiyo msingi wa kupata wahitimu walio bora katika ngazi zote za kitaaluma. Umuhimu wake hauwezi kulinganishwa na kitu chochote kile.

Kwa ujumla ni kwamba, elimu ya awali ndiyo inayomwandaa na kujenga msingi mzuri kwa mtoto kabla ya kuanza darasa la kwanza, sekondari na hatimaye kuhitimu masomo ya chuo kikuu.

Hivyo ili kuhakikisha kuwa elimu ya awali inatolewa kwa watoto wote, serikali iliagiza, katika kila shule ya msingi lazima ianzishwe darasa la elimu ya awali, ili kuwaandaa wanafunzi kuingia darasa la kwanza.

Serikali ilifikia uamuzi huo kupitia Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 1995 na tamko la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi la mwaka 2010, na sasa ujenzi wa madarasa hayo umekamilika na mengine yakiendelea.

Iwapo nchi nzima itakuwa na madarasa hayo, huku elimu ya awali ikitolewa katika misingi inayotakiwa, itakuwa ni njia bora na nzuri ya kuimarisha ubora wa elimu kuanzia awali hadi ngazi ya juu.

Hatua hii ikiimarishwa inaweza kumwondoa adui ujinga ambaye anasababisha kuwapo kwa watu wasiojua kusoma na kuandika, kuanzia kwa vijana hadi watu wazima.

Ni muhimu Watanzania kuunga mkono hatua hii inayolenga kuboresha elimu ya awali kabla ya kupanda ngazi nyingine za juu, kwani ndiko ambako mtoto anatakiwa kutoka akiwa anajua kusoma, kuandika na kuhesabu.

Kuwapo kwa shule hizo kutasaidia kumaliza tatizo la kuwapo kwa Watanzania wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu, kwa sababu watakuwa wamepata msingi mzuri wa elimu kuanzia shule za awali.

Sera mpya ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 iliyozinduliwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete mwaka 2015, suala la elimu ya awali limepewa kipaumbele.

## BARUA & MJADALA

# Waziri wa Maji tumekosa nini?

***MHARIRI***

*MIMI ni msomaji wa gazeti lako la Nipashe na wiki iliyopita Jumanne nilikutana na picha ya watoto wa shule na wanakijiji wa Tandala Wilaya ya Chemba huko Dodoma, wakichota maji yasiyo salama kwenye kisima.*

*Mwandishi na mpigapicha wanasema hiyo ni hatari kwa watoto wa shule na jamii ya eneo hilo.*

*Nisema kwa uchungu kuwa tunawahitaji wapiga picha hao wafike Mbezi Msumi jijini Dar es Salaam, wilayani Ubungo waone jinsi ambavyo tunakunywa maji ya madimbwi.*

*Tunatumia maji machafu ya visimani tena vya ardhini ambayo pamoja na kuwa chanzo cha maradhi ya kichocho, upele, kuhara na kutapika ni sehemu ambayo watu wanapoteza maisha.*

*Mimi ni mkazi wa Msumi naomba Waziri wa Maji Prof. Makame Mbarawa afike kwenye ofisi za serikali za mitaa Msumi na aonyeshwe madimbwi ambayo wananchi wanachota maji ya kunywa.*

*Maisha ya Msumi yanazungukwa na misiba kutokana na watu wazima kwa watoto kutumbukia kwenye visima na madimbwi na kupoteza maisha matukio yanayotokea kila mwaka. Waziri pia anaweza kuthibitisha hilo.*

*Kama wananchi na Watanzania tunaolipa kodi tunaomba Mamlaka ya Maji Dar es Salaam, DAWASA ituletee maji au itufanyie utaratibu wa muda wa kupata maji safi na salama ya kunywa.*

*Tumekuwa tukiulizia maji DAWASA Kimara na mwanzoni tuliahidiwa kuwa tungepeata maji kupitia mradi wa Salasala, hata hivyo tumekatishwa tamaa tulipoambiwa kuwa hakutakuwa na maji kwa sababu idadi ya wateja wa Mbopo, Kisauke na Madale ni kubwa mno, hivyo Msumi watafikiriwa baadaye. Tunajiuliza hali hii mpaka lini?*

***Waathirika wa Msumi.***

**WASILIANA NASI:**

**TUNAKARIBISHA BARUA NA MAONI YA MSOMAJI, UNAWEZA KUTUMA KUPITIA KWA MHARIRI S.L.P. 31042, DAR ES SALAAM AU mhariri@nipashe.co.tz**

# Ubunifu ukitumika upinzani utaimarika

**Na Mwandishi Wetu**




MWAKA 1992 ndiyo wakati ambao Tanzania iliridhia kufuata mfumo wa siasa za vyama vingi, kisha ukafuatia uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo huo, uliofanyika mwaka 1995, na ukawa mwanzo wa serikali ya awamu ya tatu.

Sasa ni miaka 27 tangu Tanzania iridhie mfumo huo kuwapo nchini, na pia ni miaka 24 tangu kufanyika uchaguzi wa kwanza ndani ya mfumo wa vyama vingi vya siasa.

Lakini, pamoja na hayo, kuna haja ya kutafakari na kuangalia nyuma kuhusu mfumo huo na umuhimu wake kwa siasa za Tanzania na kile ambacho kimefanywa na upinzani kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Kwanza niseme kwamba nafasi ya vyama vya upinzani katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni ni muhimu ingawa navyo vina mambo ambayo ni vyema vikasahihisha.

Taifa linatambua michango ya vyama hivyo kwa ustawi wa nchi katika nyanja mbalimbali zikiwamo za demokrasia, kuongeza uwajibikaji na utawala bora, lakini pia vinatakiwa kuweka ubunifu wa kuviwezesha kuwa imara zaidi.

Moja ya ubunifu huo ni kujitanua zaidi kwenye maeneo ya ngazi za matawini au kwenye vitongoji na vijijini, ambako kuna wanachama wengi ili viweze kuungwa mkono na watu wengi badala ya kujulikana juu hasa kwenye miji mikubwa na midogo wakati kwenye maeneo ya chini hakuna wanachama wala wapinzani hawafahamiki.

Kimsingi ni kwamba hatua ya vyama vya upinzani kushindwa kujitanua kwenye ngazi za chini, ili kuungwa mkono na wengi ni changamoto ya siku nyingi ambayo imekuwapo kwa muda mrefu tangu kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi.

Inawezekana vipo ambavyo vimejificha kwenye 'kichaka' cha kutoruhusiwa kufanya siasa hadi mwaka 2020, lakini hiyo siyo sababu, bali vyama vya upinzani vimejisahau kwamba kuimarisha chama kunaanzia ngazi ya chini.

Kwa kutambua hilo, ndiyo maana Chama Cha Mapinduzi kina mashina na matawi kote nchini, kwani huko ndiko waliko wanachama wa kuweka kukipigia kura na siyo mashabiki tu.

Sina maana kwamba upinzani hauna wanachama ngazi ya chini, lakini idadi yao ingeongezeka iwapo vyama hivyo vingekuwa na mkakati ya kujiimarisha ngazi ya chini kama ilivyo kwa CCM.

Yawezekana wengi wao wakawa ni mashabiki tu wa upinzani, ambao mwisho wa siku wanaweza kubadilika, lakini mwanachama anayejua itikadi ya chama chake habadiliki kirahisi.

Mchango wa vyama ni muhimili kwa maendeleo ya taifa, lakini navyo viwe na mkakati wa kujiimarisha, yaani kufuata wanachama ngazi ya chini na kufungua ofisi za kutosha, ili kujihakikishia ushindi katika uchaguzi.

Miaka 27 ya kuwapo kwa mfumo wa vyama vingi nchini ni mingi ambayo inatosha kuwafanya viongozi wa vyama hivyo kubuni mbinu mbalimbali za kuviwezesha kuendelea kuwa imara.

Suala la migogoro ndani ya vyama hivyo nalo ni tatizo, ambalo halina budi kutafutiwa ufumbuzi wa kudumu kuliko kuikubali na kusababisha vikosi nguvu mbele kwa kuyumbisha wanachama.

Ikumbukwe kwamba wapo baadhi ya wanachama ambao wamekimbia vyama vyao, kwa sababu ya migogoro isiyoisha, ingawa ni suala la kutofautiana katika taasisi ni jambo la kawaida.

Kinachotakiwa ni jinsi ya kumaliza tofauti ili zisisababishe migogoro, ambayo mwisho wake ni kuyumba kwa chama na kukifanya kisiwe na nguvu za kushawishi Watanzania.

Inawezekana kuna vyama bado vinajipa matumaini kwamba vina nguvu ile ile ya mwanzo na kumbe vimeshayumba, na sasa vinatakiwa kujipanga upya ili visimame imara kwenye harakati za kisiasa.

Kuendelea kuamini kwamba bado vinapendwa bila kujiimarisha kwenye ngazi ya chini ni sawa na kujidanganya, hebu viwe na mkakati wa kujiimarisha huko chini kwa kutumia viongozi walioko huko.

Siamini kwamba kuzuiwa kwa mikutano ya kisiasa kunaweza kukwamisha vyama kujiimarisha ngazi ya chini, kama chama kina viongozi wa ngazi hiyo, wafanye kazi kuimarisha vyama vyao, wasisubiri viongozi wa kitaifa.

Kuna mikakati mingi anayoweza kufanywa na vyama hivyo, lakini hii miwili ya kujiimarisha ngazi za chini na kumaliza migogoro ya ndani, inaweza kusaidia kuviongezea uhai.

Ikumbukwe kuwa chama ni watu, na watu wako ngazi ya chini kwenye mashina na matawi, ambako zinapaswa zijengwe ofisi za kutosha na kufanya kazi, ili Watanzania wa maeneo hayo wajue upo upinzani na waone kile unachokifanya kwa ajili ya maendeleo ya nchi.


## BONITE BOTTLERS LIMITED

**Advertisements of Employment**

1. **Area Sales Supervisor**

**Qualification:**
- Applicant should be a holder of Bachelor of Commerce in Marketing / Business Administration or any other related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**
- Ability to manage and monitor staff performance to ensure the preset targets are met
- Ability to actively pursue opportunities to improve Route to Market and leveraging best practices.
- Ability to drive horizontal expansion through outlet creation incentive programs
- Ability to identify Commercial and Market development improvement initiatives to drive incremental volume, and profit share.
- Ability to track performance against objectives and initiate corrective measures.
- Ability to supervise people and meet sales target assigned.
- Able to work independently with minimum supervision
- Self motivated, flexible person and a good team player

√ **Experience: Any experience in related field will be added advantage.**

2. **Salesman**

**Qualification:**
- Applicant should be a holder of form IV/VI with Diploma in Sales and Marketing / Business Administration or any related field from recognized Institution.

**Key skills & Abilities:**
- Skills and knowledge of customer care and customer services.
- Ability and skills of route sales.
- Ability to forecast sales/load to be taken for each day to the location assigned.
- Able to work independently with minimum supervision.
- Self motivated, flexible person and a good team player.
- Ability to seek out and develop news business and maximize all possible opportunities to increase Sales

√ **Experience: Any experience in the same field will be added advantage**

**Mode of Application:**
All applications accompanied with cover letter, photocopies of certificates and CVs to be sent to undersigned address, reach him not later than 11/12/2019.

**The Managing Director,**
**Bonite Bottlers Ltd,**
**P. O. Box 1352,**
**MOSHI.**
**E- mail hr@bbl.co.tz**

215540902

## DC Sabaya arejesha eneo la Tanesco baada ya miaka 35

INATOKA UK 3

mita za mraba 3,371," alidai.

Kwa mujibu wa Ole Sabaya, hakuna mtu yeyote aliyempa ofisa huyo mstaafu eneo hilo na wala hana barua ya uthibitisho wa kumiliki eneo hilo.

"Sikia Mushi, huna 'offer' (barua ya toleo), acha kutukoroga, huna barua uliyoandika kwa mkurugenzi yeyote ya kuomba eneo na hii unajua kabisa ni mali ya umma, lakini kwa makusudi toka mwaka 1984 umeihodhi kinyume cha utaratibu.

"Na wewe watu wanakufuata, Tanesco wanakuambia uwape eneo lao unawatishia, unasema wewe ni kapteni wa jeshi mstaafu, unasema mtu yeyote akitaka kujua ukichaa wako, aje hapa aingilie. Sasa, Tanesco hamna kichaa, nimekuja mimi kichaa mwenzako hapa.

"Takukuru huyu nawakabidhi hapa sasa hivi, fedha ya serikali yote ambayo unajua imepotea kutokana na wewe kulikalia eneo hili kimabavu ni jambo la kwanza naitaka.

"Jambo la pili, Tanesco kuanzia sasa hivi, nataka muondoe mali yote na msimamie uondoaji wa kila kitu hapa na vipelekwe pale maeneo ya halmashauri mpaka tutakapopata mali yetu ya serikali. Jambo la tatu, umeisababishia serikali hasara kwa miaka 35," alisema.

Kutokana na maagizo hayo ya Ole Sabaya, bidhaa zilizokuwa kwenye eneo hilo, mashine za kufyatulia matofali kwa umeme na vifaa vya ujenzi zilibebwa kwa malori na kupelekwa ofisi za halmashauri.

Ilidaiwa kuwa vifaa hivyo ni mali ya mfanyabiashara wa Sanya Juu wilayani Siha, Kedimond Ollotu, aliyekuwa amekodi eneo hilo kwa ajili ya shughuli zake za biashara ya vifaa vya ujenzi.

## Mapya yaibuka vifurushi NHIF

milia, kulipiwa dawa zilizosajiliwa na kuruhusiwa kuhudumiwa hadi ngazi ya kituo cha afya.

Alisema huduma nyingine ni kulipiwa gharama za huduma za kinywa na meno kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa, kulipiwa gharama za huduma za upasuaji mdogo zaidi ya aina 27 na za upasuaji mkubwa zaidi ya 14.

Alizitaja huduma nyingine kuwa ni kuanza kulipiwa huduma za uzazi baada ya kuchangia kwa miaka miwili kwa kuzingatia vigezo na msharti yaliyowekwa, na kulipiwa huduma za vipimo vya aina 162 vikiwamo vya Ultrasound, X-Ray, Echo na EEF.

**WEKEZA AFYA**

Alisema kwenye kifurushi hicho, wanachama watatibiwa kwenye vituo zaidi ya 7,000 na kupata huduma za kulipiwa ada ya kujiandikisha na kuonana na daktari, kulipiwa huduma ya kulazwa hadi siku 45 kwa mwaka kwa kila mnufaika.

Pia kulipiwa dawa zilizosajiliwa na kuruhusiwa hadi ngazi ya hospitali ya wilaya, kulipiwa huduma za kinywa na meno kwa kuzingatia masharti, kupata zaidi ya aina 30 za huduma za upasuaji mdogo na zaidi ya aina 36 za upasuaji mkubwa.

Alizitaja huduma nyingine chini ya kifurushi hicho kuwa ni kuanza kulipiwa huduma za uzazi baada ya mwaka mmoja wa kuchangia kwa kuzingatia vigezo na msharti yaliyowekwa, na kulipiwa aina 197 za huduma za vipimo vikiwamo Ultrasaound, X-Ray, Echo na EEG.

**TIMIZA AFYA**

Mapunda alisema ndani ya kifurushi hicho, huduma zitakazopatikana ni kulipiwa ada ya kujiandikisha na kumwona daktari na kulipiwa huduma ya kulazwa hadi siku 60 kwa mwaka.

Alisema nyingine ni kulipiwa dawa zilizosajiliwa na kuruhusiwa hadi ngazi ya hospitali ya mkoa, kulipia huduma za kinywa na meno kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa.

Mkurugenzi huyo alisema huduma nyingine ni kulipiwa zaidi ya aina 50 za huduma za upasuaji mdogo na zaidi ya aina 80 za upasuaji mkubwa na kuanza kulipiwa huduma za uzazi baada ya mwaka mmoja wa kuchangia.

Alisema huduma nyingine ndani ya kifurushi hicho ni kulipiwa aina 223 za huduma za vipimo vikiwamo CT Scan, MRI, Ultrasoud, X-Ray, Echo na EEG kwa kuzingatia vigezo na masharti yaliyowekwa.

Kwa mujibu wa Mapunda, madhumuni ya vifurushi hivyo ni kutoa fursa kwa wananchi walio katika sekta isiyo rasmi wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea, kujisajili na kunufaika na huduma za matibabu.

**VIBALI MAALUMU**

Alisema wastani wa gharama za matibabu kwa mgonjwa wa saratani ni zaidi ya Sh. milioni 69.9, huduma ya kusafisha figo ni zaidi ya Sh. milioni 35.8 na upasuaji mkubwa wa moyo ni zaidi ya Sh. milioni 12.5.

Mkurugenzi huyo alisema takwimu za mwenendo wa gharama za matibabu kwa magonjwa na huduma za vibali maalum kwa miaka mitatu zimeongezeka.

Alitaja magonjwa na viwango vyake kwenye mabano kuwa ni mwaka 2015 saratani (Sh. bilioni 11.7), figo (Sh. bilioni 11.4), huduma za moyo (Sh. milioni 128.5), vifaa tiba pandikizi (Sh. milioni 23.6), kipimo cha MRI (Sh. bilioni 4.4), kipimo cha CT Scan (Sh. bilioni 2.5), vipimo vinginevyo (Sh. milioni 37) na kinywa na vifaa tiba (Sh. milioni 44.6).

Alisema kwa mwaka 2016/2017, saratani (Sh. bilioni 18), figo (Sh. bilioni 12.6), huduma za moyo (Sh. bilioni 1.9), vifaa tiba pandikizi (Sh. bilioni 1.1), kipimo cha MRI (Sh. bilioni 4.7), kipimo cha CT Scan (Sh. bilioni 3.1), vipimo vingine (Sh. milioni 293), kinywa na vifaa tiba (Sh. bilioni moja).

Kwa mwaka 2017/18, saratani (Sh. bilioni 30.6), figo (Sh. bilioni 26.1), huduma za moyo (Sh. bilioni 4.4), vifaa tiba pandikizi (Sh. bilioni mbili), kipimo cha MRI (Sh. bilioni 8.6), kipimo cha CT Scan (Sh. bilioni 4.3), vipimo vingine (Sh. milioni 924.7) na kinywa na vifaa tiba (Sh. bilioni 1.9).

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa NHIF, Bernard Konga, alisema asilimia nane ya Watanzania wanahudumiwa kwa bima ya afya, asilimia 25 Mfuko wa CHF na chini ya asilimia moja kwenye sekta binafsi.

"Watanzania wengi wanabaki katikati, hawana pa kwenda, ndiyo maana NHIF imechukua hatua ya kuhakikisha Watanzania wengi wanapata huduma hiyo," alisema.

Kwa mujibu wa Konga, kabla ya NHIF kutangaza vifurushi hivyo, ilifanya utafiti Septemba mwaka huu, kwa kwenda kwa wananchi kwa Wilaya za Ilala na Temeke jijini, na ndani ya wiki tatu, watu 700 walijitokeza wakalipia na kuchagia kifurushi wanachokitaka na kuupatia mfuko zaidi ya Sh. milioni 440.

Alidai mfuko huo uko imara kiasi cha kumudu kujiendesha kwa miaka mitano bila michango ya wanachama.

Kwa sasa viwango vya uchangiaji vya NHIF kwa kila kundi kwenye mabano ni kila mwezi Watumishi wa Umma (asilimia sita ya mshahara na mwajiri, wafanyakazi wa kampuni binafsi (asilimia sita), wanafunzi wa vyuo na shule Sh. 50,400.

Makundi mengine ni wajasiariamali wadogo (Sh. 100,000), wakulima katika vyama vya ushirika (Sh. 76,800) na watoto weye umri wa chini ya miaka 18 (Sh. 50,400).

## Akana Chadema kumnunua Sumaye

INATOKA UK 2

aliahidiwa uwaziri.

**Nyantori:** Ulishiriki vikao vya kumnunua Waitara?

**Msigwa:** Hapana sikushiriki vikao vya kumnunua Waitara.

Pia alidai kuwa mbali na ubunge, pia ni mjumbe wa kamati kuu ya Chadema na kwamba alishiriki kikamilifu kupitisha jina la Salum Mwalimu kuwa mgombea wa ubunge Jimbo la Kinondoni.

Alidai kuwa siku ya kufunga kampeni washtakiwa wote walikuwapo katika viwanja vya Buibui pamoja na wabunge wengine wa Chadema wakiwamo Frank Mwakajoka, David Silinde, Saed Kubenea, Mwita Waitara na John Heche. Alidai kuwa kuhamasisha kubeba silaha kisheria si kosa inategemea na mazingira.

Wakati huohuo, mshtakiwa wa tatu, Mwalimu alidai kuwa video ya maandamano ilihaririwa na alianza kwa kutoa darasa la jinsi ya kuchukua picha, kuhariri video, kutangaza na mengineyo kuanzia saa nane hadi saa kumi kasoro.

Alidai video iliyotolewa mahakamani kuonyesha washtakiwa hao waliandamana ilihaririwa na alieleza sababu za picha kuonekana imehaririwa.

Alidai mtiririko wa matukio, wakati mhusika anazungumza, picha kupandana na viashiri vingine vingi alivitaja vinavyoruhusu video iliyohaririwa.

Salum alidai amemwacha mbali sana kitaaluma na uzoefu shahidi huyo wa sita kwa kuwa yeye amefundisha hadi watu wa digrii katika Chuo Kikuu cha Kiislamu Morogoro. "Mheshimiwa Hakimu, mimi kitaaluma nimeangalia ile video na aliyozungumza shahidi Koplo Charles yalikuwa yanakinzana kwa sababu picha zimehaririwa sana," alidai Mwalimu.

Mshtakiwa huyo alidai kukumbushwa habari ya mawakala wa uchaguzi katika Jimbo la Kinondoni ni sawa na kutoneshwa kidonda kwa kuwa mawakala wake wengi walizuiwa kusimamia kwa sababu ya kukosa baadhi ya nyaraka.

Mbali na Msigwa, Heche na Mwalimu, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Kibamba, John Mnyika, Katibu Mkuu wa Chadema, Vicent Mashinji; Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee, Mwenyekiti wa Taifa Chadema, Freeman Mbowe; na Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko.

Wote kwa pamoja wanakabiliwa na mashtaka 13 likiwamo la kula njama kwa madai kuwa Februari 1 na 16, mwaka jana, jijini Dar es Salaam, walifanya mkusanyiko usio halali na kukiuka tamko kutawanyika.

## Papa Msofe kortini tuhuma uhujumu uchumi

INATOKA UK 3

Dola za Marekani 110,000 (Sawa na Sh.milioni 253) kutoka kwa John Mahsson wakati wakijua ni zao la uhalifu.

Komanya alidai katika shtaka la tano, washtakiwa walijipatia Dola za Marekani 110,000 kutoka kwa Mahsson baada ya kumlaghai kwamba wangemuuzia kilo 20 za madini aina ya dhahabu na kusafirisha mpaka Ureno, huku wakijua si kweli.

Washtakiwa hawakutakiwa kujibu chochote kwa kuwa mahakama hiyo haina mamlaka ya kusikiliza kesi hiyo.

Upande huo wa Jamhuri ulidai kuwa upelelezi wa kesi hiyo bado haujakamilika, hivyo kuomba tarehe nyingine ya kutajwa.

Hakimu Shaidi alisema kesi hiyo itatajwa tena Desemba 16, mwaka huu, na washtakiwa wapelekwe mahabusu.

## Wanaoishi VVU walalamika kunyanyapaliwa biashara

INATOKA UK 4

ingatia masharti unaweza kuishi muda mrefu na ukawalea watoto wako kuliko hao walio wazima," alisema.

Mkurugenzi wa Open Kitchen, Upendo Mwalongo, alisema wana programu ya 'Amka twende' ambayo imewakutanisha wanawake wajasiriamali ili kuwanyanyua kiuchumi.

Alisema Siku ya Maadhimisho ya Wanawake Duniani wamepata bahati ya kukutana na wanawake wajane ambao wanaishi na maambukizi ya virusi vya Ukimwi kutoka Manispaa ya Temeke kwa ajili ya kuwajengea uwezo wa kibiashara pamoja na kuwawezesha kufikia ndoto zao katika ujasiriamali.

Alisema kikundi hicho watakiwezesha kwa kuwapatia fedha walizokusanya Sh. milioni 11 katika harambee waliyoifanya ili mwakani wawe kitofauti kibiashara.

Mwalongo alisema changamoto kubwa aliyoiona kwa wajasiriamali hao ni kukosekana kwa watu kwa ajili ya kuwawezesha, hivyo amewakutanisha na wafanyabiashara wakubwa ili waweze kujifunza mambo mbalimbali pamoja na kusaidiwa kifedha.

## HABARI KITAIFA

## Tahadhari mabadiliko tabianchi

**Na Enock Charles**

WANANCHI wametakiwa kuchukua hatua kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira ili kuhakikisha dunia inaendelea kuwa mahali salama pa kuishi kwa kizazi cha sasa va vijavyo.

Tahadhari hiyo ilitolewa na Mratibu wa taasisi isiyo ya kiserikali ya Nipe Fagio, Revocatus Fivawo, walipokishiriki kufanya usafi katika ufukwe wa Coco Dar es Salaam mwishoni mwa wiki yakiwa ni maadhimisho ya siku ya kimataifa ya kufanya usafi inayofahamika kama Friday for Future.

Fivawo alisema siku hiyo ilianzishwa baada ya mtoto mmoja nchini Sweden kuchukua uamuzi wa kushinda kutwa nzima katika viwanja vya Bunge la nchi hiyo, akishinikiza uamuzi unaofanywa na viongozi usiathiri maisha yake na watoto wengine.

"Tupo hapa kuendelea kupambana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira na tumewashirikisha watoto kutoka shule nne za jiji la Dar es Salaam ikiwamo International School of Tanganyika, Dar es Salaam International Academy, Shule ya Msingi Mtendeni na Yombo."

"Lengo letu ni kwamba tunataka tuondoke tuiache dunia kwa watoto wetu na wao wawaachie watoto wao dunia ambayo ni salama kwa kuishi," alisema Fivawo.

Fivawo alisema zaidi ya watu 300 wakiwamo raia wa kigeni kutoka mashirika na balozi mbalimbali walijitolea kushiriki tukio hilo ambapo zaidi ya jumla ya viroba 120 vya taka vyenye uzito tani 2.4 zilikunsanywa na kuondolewa katika eneo hilo.

Mmoja wa raia wa kigeni aliyeshiriki tukio hilo, Katrin Bornemann,

alisema ushiriki wao katika tukio hilo ni kutaka kuweka alama kuhusu masuala ya mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa mazingira na kuijengea jamii tabia ya kuchukia hali hiyo.

"Kuwashirikisha watoto wadogo katika tukio hili la kufanya usafi nikuwawezesha kufahamu suala hili na kuliona kama adui kwa maisha yao wenyewe na vizazi vijavyo," alisema Katrin.

# Mimba zakatisha masomo wanafunzi 700 mkoa mmoja

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

WANAFUNZI wa kike 722 wameshindwa kuendelea na elimu ya msingi na sekondari mkoani Rukwa, kutokana na kupata ujauzito wakiwa shuleni.

Mganga Mkuu wa mkoa wa Rukwa, Boniface Kasululu, alisema hayo wakati akiwasilisha taarifa ya mpango mkakati wa kudhibiti mimba za utotoni ambao ni matokeo ya kikao cha wadau kilichoitishwa kwa ushirikiano wa Serikali mashirika ya Plan International, Africare na Jhpiego yanayotekeleza mradi wa uzazi salama mkoani humo.

Alisema kwa mujibu wa takwimu za matukio ya mimba za utotoni katika mkoa huo, kwa kipindi cha miaka mitatu (2017/2019) wanafunzi 722 walipata ujauzito.

Alisema kati ya hao, 171 walikuwa wa shule za msingi na 551 kwa shule za Sekondari.

Kwa kuwa Mkoa haukuwa na makakati madhubuti wa kutafuta na kushughulikia taarifa za mimba za utotoni, ni dhahiri takwimu hizo ni za chini ukilinganisha na uhalisia.

Mimba za utotoni na uzazi katika umri mdogo ni miongoni mwa changamoto zinazoukabili mkoa huo, ambapo takwimu za utafiti wa kidemografia za mwaka 2015/2016 zinaonyesha asilimia 29 ya wanawake wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi19 katika mkoa ni wajawazito au wameshajifungua.

Alisema utafiti mbalimbali unaonyesha zipo sababu nyingi zinachangia uwapo mimba za utotoni ambapo yake ni hali ya umaskini kwa sehemu kubwa ya wananchi, elimu duni, mila, desturi na imani zinazomkandamiza mtoto wa kike.

Sababu nyingine ni malezi hafifu na kuporomoka kwa maadili katika jamii, kutokuwajibika kwa wazazi na viongozi katika ulinzi wa watoto hasa mtoto wa kike, uelewa mdogo wa jamii kuhusu sheria zinazosimamia masuala ya mahusiano ya watoto na wanafunzi.

Pia ukatili wa kijinsia, shinikizo rika, idadi ndogo ya shule za bweni na idadi ndogo ya shule zinazotoa huduma ya chakula cha mchana kwa wanafunzi.

Alisema mkoa una mikakati kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na shule ya msingi na kila kata inakuwa na sekondari ili kusaidia wanafunzi kutotembea umbali mrefu kwa ajili ya kufuata masomo kwa baadhi ya vijana wa kiume hutumia mwanya huo kuwalaghai watoto wa kike.

Aidha, Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, aliwataka watendaji wa serikali ngazi ya wilaya mkoani kuacha tabia ya kuficha takwimu za mimba hizo kwani kufanya hivyo kutaathiri utekelezaji wa mkakati huo.

Alisema kuwa iwapo watakuwa wawazi katika tatizo hilo, mashirika ya Africare, Plan International pamoja na Jhpiego ambayo yanatekeleza mradi wa uzazi salama mkoani Rukwa yamekuwa pia yakijitahidi kupambana na tatizo la ndoa pamoja na mimba za utotoni, watapata msaada kupitia mashirika hayo ili waweze kutokomeza tatizo hilo.

Mkuu wa mkoa huo, Joachim Wangabo, alisema atahakikisha mpango mkakati huo unafika hadi ngazi za vijiji na mitaa ili wananchi wauelewe na kushirikiana na serikali katika utekelezaji wake ili malengo kusudiwa yaweze kufikiwa.




Kaimu Mkuu wa kitengo cha Tigo Pesa, Angelica Pesha, akizindua kampeni mpya ya Tigo Pesa, ijulikanayo kama Wakala Kinara, jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, kwaajili ya mawakala wa huduma hiyo, ambapo wakala wa kwanza Tanzania atajinyakulia 20m/-. Kushoto ni Meneja Mwandamizi wa Tigo Pesa, Abdallah Mashashi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wassira akumbusha kumuenzi Nyerere

**Na Romana Mallya**

MWENYEKITI wa Bodi ya Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Steven Wassira, amewataka wahitimu wa chuo hicho kumuenzi Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Nyerere, kwa kuwa mabalozi wa maadili katika jamii na kazini.

Wassira aliyasema hayo jana jijini Dar wa Salaam wakati wa mahafali ya 14 ya chuo hicho yaliyohusisha wahitimu 3,237 wa astashahada, stashahada na shahada, wanawake wakiwa 1,735 (asilimia 54).

Wassira alisema shabaha ya chuo hicho chenye kampasi mbili ya Kivukoni ya Dar es Salaam na ya Karume visiwani Zanzibar, ni kuwaandaa vijana katika kuchukua nafasi za uongozi wa jamii.

"Matendo yenu yawe kioo kwenye jamii na muonyeshe tofauti na wanafunzi wa vyuo vingine. Matendo yenu yatafsiri kuwa mmesoma chuo chenye jina kubwa la Mwalimu Nyerere.

"Licha ya kwamba mmechukua mafunzo mbalimbali lakini mmejifunza maadili ili muwe viongozi bora," alisema.

Mkuu wa chuo hicho, Prof. Shadrack Mwakalila, alisema wanatarajia kuanza kuendesha programu tatu za shahada ya uzamili ambazo ni Shahada ya Uzamili katika Menejimenti ya Rasilimali Watu, Shahada ya Uzamili ya Elimu katika Menejimenti, Mipango na Utawala na ya Uongozi, Maadili na Utawala Bora.

Prof. Mwakalila pia alisema wana mkakati wa kuendelea kutoa mafunzo ya muda mfupi ya uongozi, maadili na utawala bora.

Alisema wamefanikiwa kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia na kuongeza udahili wa wanafunzi, akibainisha kuwa Kampasi ya Kivukoni wameongezeka kutoka 7,856 mwaka 2018 na kufikia 8,043 mwaka huu.

Alisema katika Kampasi ya Zanzibar, udahili umeongezeka kutoka 1,243 mwaka 2018 hadi kufikia 1,753 mwaka huu.

"Tuna tatizo la upungufu wa wahadhiri na wafanyakazi. Vibali vinavyotolewa vya kuajiri watumishi havikidhi mahitaji ya rasilimali watu katika idara mbalimbali za kitaaluma na uendeshaji," alisema.

## SOS yawapa sare wanafunzi 600

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

KATIKA kuboreshaji utoaji elimu Wilaya ya Iringa, Shirika la Children's Villages Tanzania (SOS) limetoa sare za shule kwa wanafunzi 604 katika shule mbalimbali za mradi wilayani humo.

Wanafunzi hao ni wanaoishi katika mazingira magumu ambao wanasoma shule za msingi katika kata za Nyang'oro na Malengakali wilayani Iringa, Mkoa wa Iringa.

Akikabidhi msaada huo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa, Robert Masunya kwa Kaimu Mratibu wa Mradi wa SOS ofisi ya Iringa, Francis Mwakitiga, alisema wanafunzi watafurahia katika masomo yao kwa kuwa wengi walikuwa wanakosa sare.

Alisema sare hizo zitawafanya wanafunzi wenye uwezo mdogo wa uchumi kutimiza azama yao ya elimu.

Mwakitiga alisema sare hizo zimegharimu Sh. milioni 23 ambazo zitagawiwa kwa wanafunzi shule za Ikengeza, Mawindi, Chamndindi na Holo katika Kata ya Nyang'oro na shule za Isaka, Makadupa na Iguluba katika Kata ya Malengamakali.

Alisema sare hizo zitawafanya wanafunzi kufurahia masomo pamoja na kuwafanya kuwa raia wema katika jamii.

Aliongeza kuwa Halmashauri ya Wilaya ya Iringa imekuwa bega kwa bega na shirika hilo kwa kuhakikisha mradi wa elimu unafikia malengo.

Mkurungezi Mteandaji wa Halmashauri ya Iringa, Robert Masunya, aliipongeza SOS kupitia ofisi ya Iringa na kupitia mradi wao wa elimu kwa kuwasaidia wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu.

Aidha, mkurugenzi huyo aliwataka wasimamizi wa mradi huo hasa waratibu elimu wa kata kuhakikisha wanasimamia ugawaji wa sare kwa walengwa.

Masunya alisisitiza kuwa SOS kwa kusaidiana na serikali wanahakikisha wanafunzi wanaoishi katika mazingira magumu nao wanapata fursa ya kupata elimu bila upendeleo.

**Mwakitiga alisema sare hizo zimegharimu Sh. milioni 23 ambazo zitagawiwa kwa wanafunzi shule za Ikengeza, Mawindi, Chamndindi na Holo katika Kata ya Nyang'oro na shule za Isaka, Makadupa na Iguluba katika Kata ya Malengamakali.**

# Simiyu yakabiliwa na uhaba wa damu

**Na Happy Severine, SIMIYU**

MKOA wa Simiyu unakabiliwa na uhaba mkubwa wa damu zaidi ya uniti 10,000, hali inayosababisha banki ya damu ya mkoa huo kuazima mkoani Mwanza ili kuokoa uhai wa wanawake na watoto ambao ndio wahitaji wakuu wa damu.

Hayo yalisemwa na Mratibu wa damu Mkoa wa Simiyu, Shem Aron Nyambaro, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani yaliyofanyika kimkoa wilayani Itilima. Alisema mahitaji ya mkoa ni uniti 18,000, ila wamekusanya uniti 6,000 tu, ambacho ni kiasi kidogo kisichokidhi mahitaji.

Nyambaro alisema changamoto wanayoipata katika kufikia lengo la ukusanyaji wa damu uwapo wa mwitikio mdogo wa wananchi katika kujitolea kuchangia damu kulingana na mahitaji.

"Mkoa unaupungufu mkubwa wa damu, na mpaka sasa tuna upungufu wa uniti 12,000 na watumiaji wakubwa wa damu ni wanawake na watoto," alisema.

Sambamba na hilo, Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu imetajwa kuwa kinara wa Maambukizo ya Virusi vya Ukimwi (VVU) mwaka 2019 baada ya Wilaya ya Busega mkoani humo kuongoza kwa maambukizi hayo kwa muda wa miaka miwili mfululuzo 2018, 2017.

Mkoa huo wenye wilaya tano, Maswa, Itilima, Busega, Bariadi na Meatu, unatajwa kuwa eneo ambalo maambukizi ya VVU yameongezeka kutoka asilimia 3.6 mwaka 2012 hadi kufikia asilimia 3.9 chini ya kiwango cha kitaifa cha asilimia 4.7, 2019.

Akieleza hali halisi ya maambukizi ya VVV Mratibu wa Ukimwi Mkoa wa Simiyu, Dk. Kulemba, alisema Wilaya ya Busega inashika nafasi ya pili kwa asilimia 2.8, wakifuatiwa na Halmashuari ya Mji wa Bariadi asilimia 2.1, huku Wilaya ya Itilima na Meatu asilimia 1.8 na mwisho ni Bariadi Vijijini asilimia 1.7.

Alisema katika zoezi la kutoa huduma za ushauri nasaha na upimaji ambalo lilifanyika kuanzia Januari hadi Novemba 2019 kwa halmashauri zote, Maswa ilionekana kuwa na maambukizi mengi mapya.

Naye Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Festo Dugange, alisema elimu zaidi inahitajika kwa wananchi juu ya kuepuka na ngono zembe, kuacha kutumia dawa za kulevya pamoja na unywaji wa pombe uliopindukia.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya ya Itilima, Benson Kilangi, aliwataka wanaume kutambua umuhimu wa kwenda kupima, huku akiziagiza halmashuari kuhakikisha elimu zaidi inatolewa.



Wachuuzi wa mahidi ya kuchoma na kuchemsha wakiwa kwenye foleni ya kusubiri bidhaa hiyo, kushushwa toka kwenye lori, katika soko la Ubungo Mawasiliano, jijini Dar es Salaam wikiendi. Mhindi mmoja mbichi uliuzwa kwa bei ya 300/-. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Elimu yatajwa kudhibiti maambukizo VVU

**Restuta Damian, MULEBA**

MKOA wa Kagera umetakiwa kutoa elimu shuleni ili kuondoa maambukizo mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) ambayo yametajwa kuwa asilimia 6.5 katika mkoa.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Richard Luyango kwa niaba ya Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, katika Siku ya Maadhimisho ya Ukimwi Duniani ambapo kimkoa yalifanyika Kata ya Izigo wilayani Muleba.

Luyango alisema elimu shuleni ni njia mojawapo ya maazimio ya mkoa katika kutokomeza hali ya maambukizo ya VVU.

Alisema idadi kubwa ya maambukizo inaonyesha kuwa vijana waliona na umri wa miaka 15 hadi 29 ambao ndiyo nguvu kazi, ndio wanaoongoza kwa kuambukizwa.

"Kwa asilimia hii na mchanganuo ulivyo, vijana wa miaka 15 hadi 29 idadi kubwa ni nguvu kazi ya Taifa ambayo ndio hazina ya vijana katika utendaji na uzalishaji," alisema Luyango.

Aidha, Luyango alisema watu 8,729 ndiyo walibainika na maambukizo ya VVU ikiwa wanawake ni asilimia 1.3 na wanaume ni asilimia 1.2.

Alifafanua zaidi kuwa jumla ya watu waliopima kwenye mkoa huo ni zaidi ya milioni 1.5, ambapo wanawake ni zaidi ya 900,000 na wanaume ni zaidi ya 600,000.

Hata hivyo, alisema kwa upande wa vipimo vya maambukizo ya VVU kwa Januari hadi Septemba hali ya maambuko ni asilimia 3.3 kwa mkoa.

Awali akitoa taarifa ya hali ilivyo katika kila halmashauri za wilaya, Mratibu wa Ukimwi Wilaya ya Muleba, Emilieta William, alisema baadha ya changamoto zinazosababisha ongezeko la maambukizo ni umaskini kwa jamii, biashara ya ngono, kupungua kwa uaminifu kwa wanandoa na kufanya ngono bila kinga.

"Mchanganuo wa hali ya maambukizi kwa kila halmashauri kwa viwango vya asilimia Muleba asilimia 1.7 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 3.7, Halmashauri ya Wilaya Bukoba asilimia 1.8 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 5.2, " alieleza William.

Alieleza kuwa Missenyi asilimia 1.8 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 5.8, Karagwe asilimia 1.6 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 1.7 na Kyerwa asilimia 1.2 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 3.0.

"Biharamulo asilimia 1.0 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 1.9 na Manispaa ya Bukoba asilimia 1.9 ikilinganishwa na mwaka huu asilimia 1.9.

## Wanaoishi mazingira magumu wakumbukwa

**Na Allan Isack, ARUSHA**

WANANCHI wametakiwa kujenga tabia ya kusaidia makundi yasiyojiweza ya watoto yatima, wanaoishi katika mazingira magumu na wale wanaokabiliwa na matatizo ya kimaisha ili wafikie malengo ya kimaisha.

Rai hiyo ilitolewa juzi na Ofisa Elimu Msingi wa Jiji la Arusha, Sarah Mwangasa, katika hafla fupi ya ugawaji wa msaada wa sare za shule ikiwamo mabegi, madaftari na vyakula vilivyotolewa na kikundi cha kijamii cha Friends of Batuli kwa wanafunzi wanaosoma katika Shule za Msingi za Osunyai na Sombetini jijini Arusha.

Mwangasa alisema kuna watoto wasiojiweza na wanaosoma katika shule 48 za Jiji la Arusha ambao wanakabiliwa na matatizo mbalimbali ya mahitaji muhimu ya kimaisha.

"Natoa rai kwa jamii kuona umuhimu wa kujitolea kusaidia jamii kadri wanavyobarikiwa na Mwenyezi Mungu ili watoto hawa wafanikiwe kufikia malengo yao," alisema Mwangasa.

Awali, Msemaji wa Kundi la Friends of Batuli, Mwalimu Batuli Kisaya, alisema kundi hilo limeanzishwa mahususi kwa lengo la kusaidia jamii hususani watoto yatima na wenye mahitaji maalumu kupitia michango yao wanayochangishana.

Alisema kundi hilo limeguswa na watoto yatima wanaosoma katika shule hizo, baada ya kubaini kuwa wanakabiliwa na tatizo la uhitaji wa vitendea kazi vya shuleni ndiyo maana wamehamasishana kuwachangia watoto hao.

"Kundi letu limejikita kuhamasisha jamii kwa vitendo ili kusaidia makundi maalumu ili na wao wapate faraja na kuishi kama watoto wengine wanaolelewa na wazazi wao," alisema Batuli.

Alisema kikundi hicho kimegawa msaada wa mabegi ya shule, sare na vyakula kwa wanafunzi 59 na msaada huo umegharimu Sh. milioni 1.5.

Wakizungumza kwa niaba ya wanafunzi waliopatiwa msaada huo, Robert Jacob na Jeremiah Daniel, kutoka shule za msingi Osunyai na Sombetini, walishukuru kwa msaada huo na kuiomba jamii kuyakumbuka makundi maalumu yenye mahitaji kama yao.

**"Kundi letu limejikita kuhamasisha jamii kwa vitendo ili kusaidia makundi maalumu ili na wao wapate faraja na kuishi kama watoto wengine wanaolelewa na wazazi wao," alisema Batuli.**

# Mamia wajitokeza kujitambua kiafya

**Na Allan Isack, SIMANJIRO**

WAKAZI 4,076 wa Mji Mdogo wa Mirerani, Simanjiro mkoani Manyara, wamejitokeza kupima magonjwa mbalimbali ikiwamo virusi vya Ukimwi (VVU) katika maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani.

Mkuu wa Wilaya ya Simanjiro, Zephania Chaula, akizungumza wakati wa maadhimisho hayo, ambayo kimkoa yalifanyika Mirerani, alisema wananchi hao wamejitokeza kupima magonjwa mbalimbali.

Chaula alisema waliopima VVU ni 2,739 wanawake ni 1,168 na wanaume 1,571 na waliogundulika kuwa na maambukizi ni 98 sawa na asilimia 3.6.

Alisema waliofanyiwa uchunguzi wa ugonjwa wa kifua kikuu (TB) ni 337 wakiwamo wanaume ni 139 na wanawake 198, lakini majibu yao bado hayajatoka.

Kwa mujibu wa Chaula, wanawake 178, walifanyiwa uchunguzi wa saratani ya mlango wa kizazi na 68 wakakutwa na dalili za kansa na walipatiwa tiba ya mgandisho papo hapo.

"Watu 78 walipimwa magonjwa ya zinaa na 11 walikutwa na maambukizi, wanawake ni 226, walipata huduma ya uzazi wa mpango, watu tisa walichangia damu na watu 507 walipima uzito na urefu," alisema.

Mkurugenzi wa Tanzanite Founder Foundation, Asha Ngoma, ambaye ni mmoja wa waandaaji wa maadhimisho hayo, aliwashukuru watu walioshiriki kufanikisha kazi hiyo.

Ngoma alisema lengo lililojiwekea ni kutoa elimu kwa watoto wa wachimbaji wa madini, wamiliki wa migodi na wananchi wanaoishi kwenye maeneo yanayozunguka migodi kuhusiana na afya na usalama maeneo ya kazi.

Alisema wananchi wengi walishiriki maadhimisho hayo, pia walishiriki michezo mbalimbali kama kuvuta kamba, kukimbia mbio fupi, kusikiliza mashairi, ngojera, nyimbo, hotuba na ujumbe wa kupiga vita maambukizo mapya ya VVU.

Kaimu Mratibu wa Ukimwi mkoani Manyara, Scola Mwalyanzi, alisema wamejiwekea lengo kupima watu kwa asilimia 93 mkoani humo litatimia ifikapo mwaka 2020.

Mwalyanzi alisema Mkoa wa Manyara kiwango cha maambukizo ya VVU kimeongezeka kutoka asilimia 1.5 mwaka 2011/12 hadi asilimia 2.3 mwaka 2016/17.




Dk. Adam Akyoo (katikati), kutoka Shule ya Kilimo, Uchumi na Biashara ya Chuo Kikuu cha Sokoine (SUA), akitoa darasa la mbegu kwa wafanyabiashara wa mbegu, Lilian Mmbando (kushoto) na Mary Mushi wa Halisi Organic Farm, ambao ni washiriki wa mkutano wa pili Baraza la Biashara la Afrika Mashariki, uliofanyika jijini Arusha mwishoni mwa wiki. **PICHA: DANIEL SABUNI**

# Washauriwa kuwalea watoto kwa maadili

**Na Allan Isack, ARUSHA**

JAMII imetakiwa kuwalea watoto katika maadili mema ili kujenga taifa la vijana wenye uwezo wa kutambua mambo mazuri na mabaya.

Mchungaji Elias Parirong wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri (KKKT) Dayosisi ya Kaskazini Kati, Usharika wa Endulen, alisema hayo wakati Kwaya ya Agape ilipotembelea kituo cha watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu cha Samaritian Village Tanzania, Moshono jijini Arusha.

Mchungaji Elias alisema watoto wakilelewa katika maadili, wimbi la watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu litapungua sambamba na kumaliza migogoro ya kifamilia kwenye jamii.

Kikundi cha kwaya hiyo, kina wanakwaya 15, kutoka Usharika wa Endulen Mtaa wa Makao na walitembelea kituo hicho kwa lengo la kutoa sadaka yao ya shukrani.

Wiki ijayo kikundi hicho kitasafiri kwenda Ubelgiji kwa ajili ya kuhudhuria kongamano la uimbaji lililofadhiliwa na Wakristo kutoka nchini humo.

Mchungaji Parirong alisema jamii inapaswa kutambua wajibu wao katika kuwalea watoto kimaadili ili kupunguza tatizo la watoto wa mitaani na wale wanaoishi katika mazingira magumu.

Mratibu wa kwaya hiyo, Joshua Thadeo, alisema ni wajibu wa jamii kuwapa watoto mahitaji muhimu ili kukabiliana na matatizo mbalimbali wanayokumbana nayo.

Alisema watoto wamekuwa wakikabiliwa na matatizo mbalimbali ya kimaisha ikiwamo uhitaji wa elimu, afya na malazi.


Hata hivyo, aliwataka wadau na mashirika ya watu binafsi kutoa misaada kwa watoto ili wapate haki zao za msingi kama watoto wengine.

"Tulipopata ufadhili huu wa kwenda nchini Ubelgiji kwa ufadhili wa Wakristo wa nchi hiyo wakiongozwa na Werner Van Ackra na Greta Farket, tumeona tuje kumshukuru Mungu na hawa watoto hii ni kama sadaka yetu," alisema Thadeo.

Mwenyekiti wa kwaya hiyo, Jackson Maghembe, aliitaka jamii kuwa wavumilivu katika familia zao jambo ambalo litapunguza ongezeko la watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu.

Mkurugenzi wa Kituo cha Samaritan Village, Josephat Mmanyi, alishukuru kwa msaada uliotolewa na kwaya hiyo.

Alitoa wito kwa serikali, wadau na mashirika mbalimbali kujitolea kuwasadia watoto hao kwa kuwa kufanya hivyo watajipatia baraka mbele za Mungu.





## Chuo cha Maendeleo Same chawezeshwa

**Na Mwandishi Wetu, SAME**

SERIKALI imeviongezea uwezo wa rasilimali fedha vyuo vya maendeleo ya wananchi (FDC) katika Wilaya ya Same, mkoani Kilimanjaro baada ya kuvipatia Sh. milioni 647.

Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, alisema jana kuwa serikali imetoa fedha hizo kwa FDC Same ili kukarabati majengo yote na kujenga bweni, madarasa mawili, jengo la utawala, karakana ya magari na darasa la chekechea.

"Katika kuviboresha vyuo hivi, maelekezo yaliyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni lazima watoto wa kike waliokatisha masomo yao kutokana na ujauzito, waanzishiwe mpango maalum wa kuwasaidia kufikia ndoto zao kupitia vyuo hivi.

"Yote haya yanafanywa ili wapate ujuzi utakaowafanya wajiajiri au waajiriwe wakiwa mahiri kwenye fani zao na hata mtoto wa maskini amudu ada," aliongeza.

Mkuu huyo wa wilaya alisema kutokana na fedha hizo ambazo serikali kuu imepeleka Same, ni habari njema kwamba sasa gharama ya ada imeshuka hadi kufikia Sh. 250,000 kwa mwanafunzi wa bweni.

Juni 3, mwaka huu Bungeni jijini Dodoma, serikali ilisema haina mpango wa kuvibadili vyuo vya maendeleo ya wananchi kuwa vyuo vya ufundi stadi (Veta).

Kauli hiyo ilitolewa na Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, William ole Nasha, huku akisisitiza kuwa serikali imejikita katika kuboresha vyuo hivyo kwa kuvikarabati na kuviongezea vifaa vya kujifunza na kufundishia ili kutoa mafunzo bora.

Naibu Waziri huyo alisema elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi hutolewa katika shule na vyuo katika viwango na madaraja mbalimbali kulingana na malengo yake.

Alisisitiza kuwa vyuo vya maendeleo ya wananchi vilianzishwa kwa lengo la kumsaidia mwananchi kukabiliana na changamoto za maendeleo katika mazingira yake kwa kumpatia maarifa na stadi anuwai.

**"Yote haya yanafanywa ili wapate ujuzi utakaowafanya wajiajiri au waajiriwe wakiwa mahiri kwenye fani zao na hata mtoto wa maskini amudu ada," aliongeza.**

# Waondolewa hofu kula nyama vibudu

**Na Mwandishi Wetu, ROMBO**

IDARA ya Afya ya Halmashauri ya Wilaya ya Rombo mkoani Kilimanjaro, imesisitiza kwamba hakuna kitoweo chochote cha nyama ya ng'ombe au mbuzi kinachouzwa katika maduka ya nyama bila kukaguliwa na madktari wa mifugo.

Daktari wa Mifugo wa Wilaya hiyo, Emil Mkemwa, alisema hofu iliyokuwa imetanda kuhusu kuwapo kwa nyama ambazo hazijapimwa ni propaganda za baadhi ya wafanyabiashara.

Mkemwa alitoa ufafanuzi huo jana baada ya baadhi ya madiwani kuhoji kuhusu taarifa zinazosambaa za kuwapo kwa nyama ambazo hazijapimwa katika maduka ya nyama.

"Hofu iliyokuwa miongoni mwa waheshimiwa madiwani juu ya nyama zisizokaguliwa na wataalamu wa mifugo kuuzwa na kudaiwa kuliwa na wananchi, naomba niiondoe na niwahakikishie kuwa nyama zote zinazouzwa kwenye bucha rasmi zimekaguliwa na ni salama kwa matumizi ya binadamu," alisema Dk. Mkemwa.

Inadaiwa madiwani hao waliibua taarifa hizo katika kikao cha kamati ya uchumi, ujenzi na mazingira, wakidai kuwa kuna baadhi ya wafugaji ambao hujifanya wao ni wataalamu wa mifugo na kuchinja mifugo na kuuzia wananchi bila kukaguliwa na wataalamu, kitu ambacho kinahatarisha maisha ya wananchi wa Rombo.

Dk. Mkemwa alisema kuwa japokuwa kuna changamoto ya idara ya mifugo kuwa na wataalamu 15 tu, kwa uchache wao hujipanga kuhakikisha nyama zote zinazochinjwa na kuuzwa kwenye bucha rasmi zinakaguliwa na ni salama kwa matumizi ya binadamu.

Kutokana na kuzagaa kwa taarifa hizo, Dk. Mkemwa aliomba ushirikiano baina ya wataalamu wa mifugo na madiwani kupeana taarifa iwapo kuna wafugaji na wafanyabiashara wasio waaminifu katika maeneo yao, ambao wanawakwepa wataalamu wa mifugo na kuchinja mifugo inayougua, bila kujua inaugua nini au kuuza nyama ya mizoga ili hatua stahiki zichukuliwe.

Diwani wa Mrao Keryo, Athuman Kimaryo, alisema kiuhalisia bado wananchi wengi wanakula nyama ambayo haijakaguliwa kwa sababu kuna wananchi wanachinja mifugo kuanzia saa 9:00 usiku na ikifika saa 11 alfajiri, nyama hiyo huuzwa na kumalizika wakati mtaalamu wa mifugo anafika kufanya ukaguzi.

Naye Diwani wa Tarakea Motamburu, Beda Moshi, alisema kuwa rahisi kwa wataalamu kuwapitia wananchi wote hata wakiwapo wanne katika kata moja, kwa sababu kila mtu anachinjia nyumbani na kwamba wanyama wanaochinjwa ni tofauti, hivyo bado usalama wa nyama zinazoliwa na wananchi ni mdogo.



Mtaalamu wa Masoko wa kampuni ya utafutaji na uokoaji katika Mlima Kilimanjaro na Meru,William Mbogho akizungumza wakati wa mafunzo kwa waongoza watalii wa mkoa wa Kilimanjaro, jana. Mafunzo hayo yaliyotolewa bure yamelenga kupunguza changamoto za kiafya kwa wageni pindi wapandapo mlima. **PICHA: DIXON BUSAGAGA**

# Ekari 9 zatengwa kwa uwekezaji

**Na Mwandishi Wetu, SAME**

HALMASHAURI ya Wilaya ya Same, imetenga eneo lenye ukubwa wa ekari tisa katika Kata ya Gavao Saweni, kwa ajili ya kupisha mradi mkubwa wa uwekezaji wa viwanda vidogo.

Taarifa ya Mkuu wa Wilaya ya Same, Rosemary Senyamule, iliyotolewa jana, inaeleza kuwa eneo hilo ni mahususi kwa ajili ya kutekeleza shughuli za viwanda na zingine za kiuchumi ili kutoa ajira kwa makundi ya vijana.

"Hilo eneo tumelitenga mahususi kupisha uwekezaji wa viwanda vidogo na vya kati, eneo lenyewe lina ukubwa wa ekari tisa na lina nyumba kadhaa ambazo zipo tayari kwa ajili ya kupangishwa kwa shughuli mbalimbali za ujasiriamali," alisema Senyamule.

Alisema sekta ya viwanda inapewa kipaumbele kwa sasa kwa sababu ya nafasi kubwa iliyonayo katika kukuza uchumi wa mtu mmoja mmoja na kuongeza pato la taifa.

Aidha, Mkuu huyo wa Wilaya alisema viwanda hivyo vinachangia kuongeza ajira, soko la bidhaa za kilimo kupitia malighafi na mzunguko wenye sura pana katika kukuza uchumi wa nchi.

"Naamini tutafikia ndoto za Rais John Magufuli za kuifanya Tanzania kuwa nchi ya viwanda ifikapo mwaka 2025 iwapo juhudi za pamoja zitazingatiwa baina ya taasisi binafsi, serikali na wadau wa maendeleo kwa jumla," alieleza.

Hivi karibuni, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Teknolojia na Uendelezaji Viwanda wa Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO), Mhandisi Emmanuel Saiguran, alikaririwa akisema uanzishaji wa viwanda vidogo utasaidia uchumi kukua na kutoa ajira kwa wingi.

"Sasa hivi tunatafuta wadau wa maendeleo ili watusaidie kuendeleza miradi ya kongani mbalimbali tunayoitekeleza nchini," alisema.

Pia alisema bado wanahitaji wadau wengine wa maendeleo ili washirikiane kuendeleza miradi ya aina hiyo kwenye mikoa mingine.

Pamoja na mambo mengine, mkurugenzi huyo amesisitiza ili kuwafikia wajasiriamali vijijini na kutoa huduma kwa ufanisi katika maeneo ya kuendeleza huduma zake, kuhamasisha uanzishwaji viwanda, kutoa mafunzo ya ujasiriamali, uwekezaji katika masoko na kutoa huduma za kifedha wanahitaji angalau Sh. bilioni 50 kwa mwaka.

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 3, 2019
TEKNOLOJIA • ELIMU • SAYANSI



Ukurasa 18

## Chama cha wafanyakazi ni mkombozi wa mtumishi



Ukurasa 15

## Miundombinu mibovu inavyokwaza kesi GBV



Ukurasa 19

## Utandawazi unavyoongeza changamoto, malezi kifamilia



# Jamii zilivyofaidika miradi uhimilivu tabianchi Miti 1,000,000 yapandwa, visima, mabwawa tele

Ukurasa 16

# ELIMU KUTOKA POLISI



Mkuu wa Jeshi la Polisi Nchini, (IGP) Simon Sirro, katika moja ya matukio ya mwezi uliopita akitoa maelezp na maagizo jijini Dar es Salaam kuhusu mpango mkakati wa kukomesha vitendo vya rushwa barabarani. **PICHA: MTANDAO.**



Polisi wakitoa huduma za kijamii kwa kuwajali watoto na wanawake katika matukio yanayoongeza uhusiano baina ya polisi na raia. **PICHA MTANDAO.**



Mkuu wa Dawati la Jinsia na Watoto Mkoa wa Mbeya, Mrakibu Msaidizi wa Polisi Janeth Masangano. Taifa na dunia ipo kwenye msimu wa siku 10 za kupinga ukatili wa kijinsia. Polisi ni miongoni mwa wadau wanaookoa watoto , wanawake na makundi ya wanyonge wanaokabiliwa na ukatili wa kijinsia. Ni vyema watu wakaripoti polisi madai ya unyanyasaji watoto na kufikisha kesi hizo mahakamani ili kupunguza matendo hayo yanayowaumiza kisaikolojia na kimwili. **PICHA: POLISI**



## TUJIFUNZE KISWAHILI

**BARNABAS MARO**
marobarnabas@yahoo.com

# Mkataa kwao mtumwa hasa

MTU anayekataa kwao huwa mtumwa mahali anapoishi. Twakumbushwa umuhimu wa kuzikumbuka asili zetu au tutokako. Twapaswa kuwaonea fahari wazazi wetu au hata mataifa yetu.

Lugha ni mpangilio wa maneno yanayotumiwa na watu wa jamii fulani katika mawasiliano; mtindo anaotumia mtu katika kujieleza.

Lughawiya ni taaluma inayoshughulikia uchambuzi wa lugha katika nyanja mbalimbali kama vile sarufi, maana, matamshi na matumizi.

Maana moja ya neno 'baraza' ni kikundi cha watu aghalabu (kwa kawaida) wenye mnasaba (uhusiano baina ya watu, vitu au mambo; hali ya jambo) na shughuli maalumu, walioteuliwa kusimamia shughuli iliyo katika jamii.

Hapana shaka mamlaka zinazosimamia Kiswahili zilizoundwa ili kuelekeza utaratibu mzuri wa matumizi ya maneno ya Kiswahili. Pia, kusahihisha matumizi mabaya ya maneno yanayokosewa au yasiyo ya Kiswahili.

Nathubutu kusema zinashindwa kutimiza wajibu wake. Kwa sababu hiyo, baadhi ya vyombo vya mawasiliano vinatumia maneno yasiyostahili , yanayopaswa kuishia kwenye mazungumzo ya mitaani.

Pia, huchanganya maneno ya Kiingereza na Kiswahili ingawa ni ya Kiswahili. Lahaula (neno linalodhihirisha mshangao au sikitiko).

Mfano, kuna chombo maarufu cha habari ambacho kinaonekana kupitiliza katika matumizi ya mchanganyiko huo.

"Ninukuu machache ; "Next Unai Emery hali ni tete pale ...." Kimsingi 'next' ni neno la Kiingereza lenye maana zaidi ya moja, lakini kwa muktadha huu ni –enye kufuata. Ni neno ambalo ufahamu wake huo wa Kiingereza, unawafikia wachache waliobahatika kudodosa tafsiri yake

Pia, linginelo la Kiswahili liliandika: "ShowBiz... yarudishwa kitaani."

'ShowBiz' ni maneno mawili na si moja kama lilivyoandikwa. Huandikwa 'show biz' na maana yake ni biashara au shughuli za burudani. Kwa matumizi aliyohitaji neno 'burudani' lingekidhi haja.

Kwa nini wachanganye Kiswahili na Kiingereza? Au tunatumia tusichokielewa vizuri ?

Ebo (neno la kuonyesha mshangao au kuonya; tamko linaloonyesha hisia ya dharau inayotokana na kukasirika au kutoridhika). Hawajui kuwa "Cha wenyewe huliwa na wenyewe?" Maana yake kitu cha wengine huwafaidi wao wenyewe. Sentensi ifuatayo ina maana gani? "Baada ya majirani zao Tottenham kula kichwa cha kocha wao, sasa zamu ya ....." He ... 'walikula kichwa cha kocha wao' wakiangaliwa tu bila kuchukuliwa hatua za kisheria?

Ukurasa wa mbele wa gazeti hilo uliandikwa na herufi kubwa: "Simba Kufuru." Hueleza mara kwa mara kuwa maana sahihi ya neno 'kufuru' ni sema au amini jambo kinyume cha mafunzo ya dini yako, dharau dini yako.

Hata hivyo neno hilo laendelea kutumiwa kinyume kabisa cha maudhui (wazo linaloelezwa katika maandishi au katika kusema) yake.

"... apandwa na mzuka... " ndivyo ilivyoandikwa na gazeti hilo hilo. 'Mzuka' ni kiumbe kisichoonekana ila hudhaniwa kuwa kinaishi na huweza kumtokea mtu; pepo. Kiumbe asiyeonekana na anayedaiwa kuwa humwingia mtu kichwani na kusema anayotaka kupitia mtu huyo ambaye kwa wakati ule ni kiti cha pepo.

... alipungwa na nani? Mbona kichwa hicho ni tofauti na yaliyoandikwa? Tena ikaandikwa: "... anautamani usukani wa Ligi Kuu ... baada ya chama lake, ...kupanda hadi nafasi ya pili ..."

Husemwa: 'chama changu au chake; vyama vyetu,vyao.' Si sahihi kusema au kuandika chama 'langu', chama 'letu', chama 'lake', chama 'lao.'

Huo ni uchafuzi mkubwa wa lugha inayotegemewa kuwa mwalimu wa lugha ya Kiswahili duniani.

Katika mtizamo huohuo kuna lililoandikwa "... anakiwasha tu Sauzi." Hapo kuna la kushangaza, jina moja limeandikwa mara mbili katika matamshi tofauti Huu ni upotoshaji wa majina ya watu na kadhia (jambo linalojiri ; tukio la kuhuzunisha) hii imekuwa ikitokea mara kwa mara.

"Anakiwasha tu ..." maana yake nini? Kama mwandishi anafahamu maana yake asidhani wasomaji wote wanaelewa. Waandishi wanapaswa kuandika yanayoeleweka ili wasomaji wayaelewe vyema.

Ndiyo maana kila niandikapo hueleza maana sahihi ya baadhi ya maneno ninayodhani hayaeleweki na baadhi ya wasomaji. Maana ya 'Kosoa' (kosoana, kosolewa, kosoleka) ni kitendo cha kumrekebisha mtu.

Maneno 'lakini' na 'pia' hayatumiwi pamoja ingawa viongozi wetu, wabunge na mawaziri huyachanganya mara kwa mara wanapoongea na wananchi kueleza mambo yaliyofanyika, yanayofanyika na yatakayofanyika.

Kwa mfano: "Serikali imejenga reli ya kisasa 'lakini pia' inajenga madaraja ya juu ili kupunguza msongamamo wa magari."

Maana ya 'lakini' ni tamko la kuonyesha kasoro ya jambo. Neno linaloonyesha uwepo wa upungufu, kasoro au hitilafu; isipokuwa, ila. Mfano: "A alitaka kusomea urubani lakini baba yake (Mungu amrehemu Inshallah) alimkataza."

**Msemo: Muambaa na upwa hali ugali mkavu.**

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

ELIMU

NA GAUDENSIA MNGUMI

SIKU 16 KUPINGA UKATILI

# Miundombinu mibovu inavyokwaza kesi GBV

NI saa 3:40 asubuhi watu wanatembea kwa kasi kwenye barabara ya vumbi inayoelekea Kigamboni. Kuna vumbi nyingi, lakini kipindi cha mvua ni madimbwi na matope. Ndiko iliko Mahakama ya Hakimu wa Wilaya ya Mafia, kisiwa kilichoko mkoani Pwani.

Wanaotembea haraka wanawahi mahakamani ili kusikiliza kesi zao, lakini wamechelewa hivyo kesi imeahirishwa, mashahidi, walalamikiwa na mawakili wa jamhuri wameondoka.

Ongezeko la watoto wahalifu, miundombinu na ukosefu wa usafiri katika kisiwa hicho chenye visiwa kadhaa vidogo na mengineyo yanayoibuliwa na Hakimu Mfawidhi Mwandamizi wa Wilaya ya Mafia, Moses Maroa, katika mahojiano na Nipashe hivi karibuni, gazeti lilipotembelea eneo hilo.

Majadiliano yanaangazia kesi na masuala ya unyanyasaji kijinsia (GBV), suala linalodaiwa kuwa ni tatizo Mafia. Lengo ni kuielimisha jamii kuepuka ukatili wa kijinsia katika kipindi hiki cha siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia Duniani.

Maroa, anasema kesi za ubakaji wanawake kwa watoto, ulawiti na shambulio la aibu zinafikishwa mahakamani hapo. Na kwamba kesi inapofikishwa inasikilizwa kuanzia mwanzo hadi mwisho na uamuzi yanatolewa, sasa endelea...

**SWALI: Kuna madai kuwa kesi za unyanyasaji wa kijinsia mara nyingi watu hawaridhishwi na hukumu zake, unalielezeaje?**

**JIBU:** Wakati mwingine hukumu zinazotolea ni zile ambazo watu hawakuzitarajia. Ni kwasababu ya ushahidi kutojitosheleza.

Iwapo kesi itafikishwa mahakamani na hakuna ushahidi wa kutosha, au mashahidi hawatoi ushirikiano ni vigumu kumtia mshitakiwa hatiani. Kwenye kesi kama kuwapa wanafunzi mimba na ubakaji kukosekana ushahidi madhubuti kunasababisha hukumu inayotolewa iwe haikutarajiwa.

"Kwa mfano walalamikaji kuchelewa kufikisha malalamiko mahakamani, au kufungua kesi pale wanapoona mlalamikiwa anakiuka makubaliano.

Mathalani, mtoto amebakwa Januari, wakakubalina na kumaliza nyumbani kuwa watalipana, lakini mtuhumiwa akakiuka makubaliano pengine mwezi Agosti, kesi inapelekwa polisi na kuletwa mahakamani. Kutokana na ucheleweshaji inakuwa vigumu kupata ushahidi madhubuti."

Hapo ushahidi unakosa nguvu kama binti ana mimba bila kupima nasaba (DNA) inakuwa vigumu kwa sababu hakuna ushahidi wa awali unaoweza kuthibitika.



Watoto wa Shule ya Msingi Kilindoni, Mafia wakicheza ngoma kuhamasisha ulinzi wa mabinti dhidi ya ukatili wa kijinsia unaofanyika kupitia mradi wa SVAGs. **PICHA: GAUDENSIA MNGUMI.**

> "Kwa mfano walalamikaji kuchelewa kufikisha malalamiko mahakamani, au kufungua kesi pale wanapoona mlalamikiwa anakiuka makubaliano.

**SWALI: Zama hizi simu zimekuwa zikitumiwa kupata ushahidi, mahakama zinatumia ushahidi wa sms kwenye kesi za GBV? Washtakiwa wananaswa kwa matumizi ya simu kuhadaa mabinti?**

**JIBU:** Ushihidi wa simu ni mgumu. Wapo waliofikishwa, lakini walitumia simu ambazo si zao au namba zisizosajiliwa hivyo ni vigumu kuwakamata. Aidha, ujumbe hauna jina la muhusika moja kwa moja wala si namba yake, hivyo bado mahakama haiwezi kumhukumu kwa mawasiliano haya hata yakifikishwa mahakamani.

Kuna wengine wanatumia simu za rafiki zao kuwasiliana na wasichana hao ili wasikamatwe.

**SWALI: Nini kinafanyika kukabiliana na changamoto ya kukosekana ushahidi madhubuti?**

**JIBU:** Katika kesi za GBV mahakama inatoa elimu kuwaelimisha watu kuhusu umuhimu wa kufikisha kesi mahakamani mapema na kuwa na ushahidi siyo kusuluhishana. Wanaelimishwa umuhimu wa kufungua mashtaka, kutoa ushahidi na kufuatilia mchakato na taratibu zote za mashtaka mahakamani.

Aidha, tunawaeleza umuhimu wa kutii amri ya mahakama. Shahidi au yeyote akipata wito ni lazima afike mahakamani.

"Pia tunawafahamisha kuwa ibara ya 13 ya Katiba ya Tanzania inasema kila mtu hana hatia mbele ya sheria mpaka pale mahakama itakapothibitisha kuwa ana hatia. Hivyo ni jukumu la mshitaki, polisi na mashahidi kuithibitishia mahakama pasipo shaka na kumtia mlalamikiwa hatiani. Si vinginevyo."

**SWALI: Unaweza kuzizungumziaje kesi za GBV Mafia?**

**JIBU:** Ni nyingi ni wastani wa kila mwezi kesi moja. Mathalani takwimu zinaonyesha mwaka 2018 zilikuwa 12 ambazo kubaka nne na kulawiti nne pia nne za shambulio la aibu.

Mwaka huu ziko tisa mashataka ya ubakaji pekee ni saba.

### CHANGAMOTO:

**SWALI: Ni zipi unazoziona kuwa ni changamoto kubwa kisiwani hapa kwenye kesi za GBV?**

**JIBU:** Kwenye kesi za GBV ni mazoea ya kufichiana siri yanayofanywa na wazazi au walezi wa watoto wanaonyanyaswa.

Aidha, kukubaliana na kumaliza kesi kidugu ni tatizo pia. Shida ya kupatikana vipimo kwa mfano DNA. Polisi wanaweza kufungua kesi upya baada ya mtoto kuzaliwa kwa kumpima DNA na kuanzisha mashtaka upya, lakini hakuna ufuatiliaji unaofanyika mara kwa mara.

### WATOTO WAHALIFU

Kanuni ya adhabu kifungu cha 131(1,2,3), kinatoa adhabu kwa mtoto aliyebaka au kutenda kosa la kunyanyasa kingono ambayo ni viboko, kuonywa, kifungo na kifungo cha maisha.

Aidha, sheria ya mtoto ya mwaka 2009 inaamuru mtoto akiwa katika kesi kama hizo alindwe, aonywe pia inakataza adhabu ya kifungo cha maisha kwa anayenajisi mtoto mdogo badala yake anafungwa miaka mitano .

Licha ya kuwapo sharia hizo watoto chini ya miaka 18, wanabaka na kulawiti wenzao. Aidha, wengine wanawabaka, walemavu na wazee. Ni vyema kuwa na mahakama ya watoto watukutu za kutosha kwani idadi yao inaongezeka.

Kadhalika, pamoja na mahakama hizo ni muhimu kuwa na maofisa ustawi wa jamii ambao ni wadau wakubwa kwenye kusikiliza kesi za watoto hao.

### MIUNDOMBINU DUNI

Kukosekana usafiri ni tatizo kubwa si kwa mahakama pekee bali hata kwenye idara na sekta nyingine za umma na za binafsi kisiwani Mafia.

Vipo visiwa vingi vyenye wakazi ambavyo havina usafiri mbali na mitumbwi, ambayo nayo inategemea usalama wa bahari. Iwapo kuna dhoruba hakuna usafiri. Wakati mwingine dhoruba kali huchelewesha usafiri.

"Mahakama inaathirika. Kesi inaweza kuahirishwa kwa sababu shahidi na mshitaki wamechelewa kutokana na kukosekana usafiri au dhoruba baharini. Inatokea baada ya kesi kuahirishwa wanafika mahakamani. Ni usumbufu na gharama kwa wananchi. Wakati mwingine ni vigumu kuwafikia mashahidi muhimu na kuwaleta mahakamani au kupeleka DNA, yote haya yanakwamisha kesi na kuzichelewesha".

Kwa ujumla haki inatakiwa kutendeka na kuonekana ikitendeka bila kujali tatizo la miundombinu kukosekana usafiri ni changamoto kama hizo. Kwa hiyo serikali isaidie namna ya kutatua tatizo hilo ili kutoa haki kwa washitaki na washitakiwa kwa wakati.

**SWALI:Vipi kuhusu bajeti na usafirishaji wa mashahidi kutoka visiwani?**

**JIBU:** Nalo ni tatizo ufinyu wa bajeti ni tatizo kubwa na wakati mwingine mahahakama haina fedha ya kuwatoa mashahidi visiwani au sehemu nyingine mbali na kuwafikisha katika mahakama ya wilaya hivyo ni vyema kuwa na utaratibu wa kuangalia eneo hilo hasa Mafia ambako ni kisiwani.

**SWALI:Unadhani changamoto hizo zinatatuliwaje?**

**JIBU:** Elimu itolewe kukataza watu wasikae vikao kusuluhisha na kukubaliana kesi za GBV zifikishwe mahakamani.

Iwapo kesi ya ujauzito itakosa ushahidi muhimu mahakamani, binti akijifungua polisi wachukue DNA za mtoto na za baba mtuhimiwa, kuzipima na kufungua kesi upya wasinyamaze yakaishia kwenye hatua za mwanzo, waendelee.

Kwa upande wa usafiri utaratibu uandaliwe nauli za ndege tufikiriwe ili zipunguzwe tulipe nusu au Sh. 30,000 kuliko 150,000 au 300,000 kwenda na kurudi, ili kufanikisha shughuli na mipango ya mahakama na idara nyingine za serikali.

Makala hii imeandikwa wakati wa ziara ya wanahabari iliyoandaliwa na Shirika la ActionAid, wilayani Mafia. Shirika hilo linashirikiana na wadau kutokomeza ukatili dhidi ya mtoto wa kike (SVAGs) ili kuwaondoa wasichana kwenye ukatili wa kingono, mimba na mdoa za utotoni.

TEKNOLOJIA

NA GERALD KITABU

# Jamii zilivyofaidika miradi uhimilivu tabianchi Miti 1,000,000 yapandwa, visima, mabwawa tele



Moja ya maeneo yenye matumizi endelevu ya ardhi ikijumuisha kilimo na utunzaji wa uoto asili. **PICHA: GERALD KITABU**

TANZANIA imekuwa ikiathiriwa na athari za mabadiliko ya tabianchi kama ilivyo kwa mataifa mengine yanayoendelea. Athari hizo zinajumuisha kuongezeka kwa wastani wa joto, kina cha bahari, na majanga ya hali ya hewa ikiwamo ukame na mafuriko.

Pia, taathira nyingine ni kukauka na kupungua kwa vyanzo vya maji kama mito na maziwa; kuyeyuka kwa theluji ya kudumu hususani Mlima Kilimanjaro na kuongezeka kwa magonjwa ya mimea, mifugo na binadamu.

"Kutokana na mabadiliko ya tabianchi kuathiri nchi nyingi zinazoendelea, Umoja wa Ulaya (EU), ulianzisha "Global Climate Change Alliance (GCCA)" mwaka 2007. Lengo kuu likiwa ni kuimarisha uwezo wa uhimilivu wa athari za mabadiliko ya tabianchi na kupunguza umasikini kwa jamii zilizo hatarini. Kwa Tanzania, GCCA ilianza awamu ya kwanza kutoka mwaka 2011 mpaka 2013 na awamu ya pili kutoka mwaka 2015 mpaka 2019. Katika awamu hiyo ya pili, miradi mitano ilifadhiliwa na EU iliyotekelezwa mikoa ya Arusha, Dodoma, Tanga (Usambara Mashariki), Tabora (Igunga) na Zanzibar. Baadhi ya mambo yaliyofanyika katika miradi hiyo ni usimamizi wa rasilimali maji na matumizi bora ya ardhi kwa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi", alisema Fazal Issa - Mshauri Mwelekezi wa GCCA.

> Kutokana na mabadiliko ya tabianchi kuathiri nchi nyingi zinazoendelea, Umoja wa Ulaya (EU), ulianzisha "Global Climate Change Alliance (GCCA)" mwaka 2007.



Athari za mabadiliko ya tabianchi, upepo mkali na mvua kubwa zimesababisha migomba kuanguka katika mashamba ya ndizi na kuwaletea wakulima hasara. **PICHA: MTANDAO.**

**USIMAMIZI WA MAJI**

Tanzania imebarikiwa kuwa na vyanzo vingi vya maji ya juu na chini ardhini, ila bado ina changamoto kubwa ya usambazaji na upatikanaji wa maji hususani vijijini. Kuongezeka kwa idadi ya watu na mahitaji ya shughuli za kilimo, ufugaji na viwanda vitanitishia vyanzo hivyo vya maji. Pia, athari za mabadiliko ya tabianchi zinaongeza changamoto hiyo ya uhaba wa maji maradufu. Miradi hiyo mitano ya GCCA ilisaidia katika jitihada za uhimilivu katika sekta ya maji kwa matumizi na nyumbani na shughuli za kiuchumi.

Katika utekelezaji wa miradi hiyo, changamoto mbalimbali zilitambuliwa. Hizi zinajumuisha utekelezaji usioridhisha wa sheria ndogo ndogo na miongozo inayohusiana na usimamizi wa vyanzo vya maji, uelewa mdogo wa watumiaji maji; miongozo isiojitosheleza katika usimamizi wa miundombinu ya maji kwa kilimo na ufugaji; uwazi na uwajibikaji na kutohuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango ya sekta ya maji.

**MATUMIZI YA ARDHI**

Matumizi bora ya ardhi na uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi, kwa jamii za vijijini Tanzania, ardhi ni rasilimali muhimu sana. Takribani asilimia 72 ya wananchi wanaitegemea kwa ajili ya kipato chao na maisha yao kijumla hususani kwa kilimo na ufugaji. Shughuli hizo zikiwa zinaathiriwa sana na mabadiliko ya tabianchi. Hivyo, upatikanaji wa ardhi na kuwa na mipango bora ya usimamizi wa ardhi inayozingatia mabadiliko ya tabianchi ni muhimu sana kwa maisha endelevu vijijini.

Kutokana na kuongezeka kwa matumizi ya ardhi vijijini, Tanzania imekumbwa na migogoro mbalimbali ya matumizi ya ardhi hususani katika Kanda ya Kati ya nchi. Hivyo, mipango na matumizi bora ya ardhi inaonekana kuwa nyenzo muhimu ya kutatua migogoro hiyo. Japokuwa, ni asilimia 13 tu ya vijiji ndio vimekamilisha kuandaa mipango yao ya matumizi ya ardhi.

Miradi mitano ya GCCA iliona kuwa mabadiliko ya tabianchi yanachangia pia katika migogoro ya ardhi. Ukame uliokithiri unaosababishwa na mabadiliko ya tabianchi unasababisha kupungua sana na kupotea kwa vyanzo vya maji, kuharibika kwa bioanuwai na kuongezeka kwa kuhamahama ili kutafuta maji, malisho na ardhi kwa ajili ya kilimo.

Kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo, changamoto mbalimbali ziliainishwa. Changamoto hizo zinajumuisha ukosekanaji wa rasilimali na taarifa za kutosheleza; upangaji wa matumizi ya ardhi kwa maeneo madogo; mapungufu katika uratibu na usimamizi wa utekelezaji sheria; na kutohuisha masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika sera na mipango ya matumizi ya ardhi. Pia, changamoto nyingine ni fedha za utekelezaji wa mipango hiyo ya ardhi. Hii iliainishwa na Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji. Mgimwa anaongeza kuwa, ingawa serikali imepiga hatua katika uandaaji wa mipango ya ardhi ila bado changamoto inabaki kuwa namna ya kupata fedha za utekelezaji.

**MAFANIKIO MAKUBWA**

Utekelezaji wa miradi hiyo mitano ya GCCA inayodhaminiwa na EU umechochea kuleta matokeo chanya katika matumizi na usimamizi wa maji na ardhi kwa uhimili wa mabadiliko ya tabianchi. Hii inajumuisha upatikanaji wa maji kwa makazi 11,500; kuongezeka kwa matumizi ya pampu za maji za kamba; na kujengwa kwa mabwawa ya kunyweshea mifugo ambao yamesaidia pia kilimo cha mboga.

Pia, matokeo mengine ni kuongezeka kwa maeneo ya usimamizi endelevu kufikia hekta 25,000; kupanda miti takribani 1,000,000 na asilimia 72 ikistawi, upandaji wa mikoko; kupitishwa kwa sheria ndogo ndogo ya matumizi bora ya maji na ardhi; kukamata na kuwalipisha faini wahalifu wa ukataji miti ovyo, wanaolisha mifugo katika maeneo ya hifadhi, na wanaochoma mkaa bila kibali.

**KUIMARISHA UHIMILIVU**

Kutokana na changamoto na matokeo chanya yaliyoainishwa miradi hiyo mitano ya GCCA imetoa mapendekezo kadhaa ambayo yatasaidia uhimilivu wa mabadiliko ya tabianchi hususani katika sekta ya maji na ardhi.

Kwa upande wa sekta ya maji; mapendekezo ni kuboresha mifumo ya sheria na kitaasisi; kuimarisha uwezo wa jamii na watumiaji wa maji katika usimamizi wa rasilimali maji; uandaaji na usambazaji wa miongozo bora; na uhuishwaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango na sera za sekta ya maji.

Kwa upande wa ardhi; mapendekezo ni kuwa na miongozo tofauti kwa kuzingatia kanda za kilimo za kiikolojia; kujenga uwezo wa ushiriki wa wadau; kuwa na mikakati ya kutatua migogoro; na uhuishwaji wa masuala ya mabadiliko ya tabianchi katika mipango na sera za sekta ya ardhi.

Pia, George Simbachawene, Waziri Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais -Mazingira, anasisitiza kuhusu kuboresha ushirikiano kati ya serikali na asasi za kiraia na kuongeza uelewa wa jamii kuhusu mabadiliko ya tabianchi kama hatua muhimu za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Simbachawene anaongeza kwamba, ofisi yake inalenga kushirikana na wadau wasio wa taasisi za serikali kuandaa kongamano na kitaifa la wadau wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi angalau mara moja kwa mwaka ili kuhamasisha ushirikiano na utekelezaji wa pamoja wa mipango ya uhimili wa mabadiliko ya tabianchi.

HAKI, UWAJIBIKAJI & VITA YA RUSHWA

# Kuikabili rushwa ngono, elimu mbadala muhimu



Kizazi kinachotarajiwa kuunda taifa bora la baadaye. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Niko Kasera**

NI vigumu kuzungumzia rushwa ya ngono ambayo kwa hivi sasa imekithiri kwenye jamii. Itoshe kusema kwamba, kama zilivyo rushwa nyinginezo, hiki nacho ni kidonda kinachosababisha uozo usiovumilika kwenye jamii ya Kitanzania na duniani kote.

Shida ndani ya rushwa ya ngono ni kwamba inajitokeza zaidi kwa hulka ya kulaumiwa wanaume kama chanzo pekee cha tatizo hili. Ni kweli, ila nadhani kuna haja ya kwenda mbali zaidi ya hapo.

Naomba nitoe mfano mdogo wa kijamii, ambao nadhani ni muda sasa ufungue tafakari zetu. Siku chache zilizopita kulikwapo sherehe ya kijamii, tena imezama kiimani iliyoandaliwa na wazazi kwa binti mdogo.

Ilichukua maandalizi makubwa unaowahusu wengi mitaani kwake wakachangishwa, hata ilipofika siku shamrashamra zilianza pale nyumbani kwa umma wa wageni kumiminika penye sherehe. Nyimbo mbalimbali zilirindima, kuanzia za imani hadi mitindo mbali inayotamba redioni, bila kusahau singeli za vijana.

Baada ya mlo na mbwembwe zingine za kisherehe, makubwa yakaanza kuchukua nafasi katika utoaji zawadi, mshereheshaji 'akichombeza' mengi kupitia kipaza sauti chake.

Zilisikika kauli za 'kiutuuzima' kuwasifia kinamama waliopo katika uwezo wa kunengua na maumbile. Ni ndani ya muda huo vilevi vikaanza kusambazwa.

Jicho na fikra zangu la haraka zilihamisha mtazamo kutoka hafla iliyotanguliwa na imani, ikahamia katika dhana ya uhamashishaji ngono, tena ile ngono zembe. Kuanzia watoto wadogo, hadi wenye umri wa kujitambua, wazazi, kaka na dada zao. Nikajiuliza, tunajifunza nini hapo?

Hayo ndiyo tunayashuhudia na kwingineko, ikiwamo katika baadhi ya vyombo vya mawasiliano vya aina tofauti, ambavyo kimsingi ni nguzo kuu kwetu kudodosa ufahamu wa kinachoendelea nyumbani na duniani.

Kwa mtazamo wangu, sehemu kubwa ya mfumo wa maisha yetu ama kwa makusudi au bahati mbaya, tumetumia kujenga mazingira chanya ya kuwapo ngono zembe. Tunaendana na jamii inayoishi na kudhani ndoto za mafanikio zinapitia ngono zembe na ishara ya mojawapo ya mafanikio iko kwa wanaume.

Mtazamo huo ukitawala pande hizo mbili, ngono zembe inakuwa jambo la msingi kwao. Leo hii tunaposhuhudia uwapo wa rushwa ya ngono miongoni mwetu, kwanza tukubali; Tumeyakuza, tumeyataka, lakini tukitaka kuyamaliza, ni sharti tubadilike.

Kesi za rushwa ya ngono zipo katika sura mbalimbali. Kwanza, ni kuombwa na aliyeombwa akakataa. Pili, ni kuombwa kwa ahadi na aliyeombwa akatoa kwa kutarajia ahadi itimie, kisha haikutimia.

Zikibebwa maana hizo, ni kwamba mtoaji na mpokeaji wa rushwa hiyo wanapokuwa katika mustakabali wa kukubaliana na wakatimiziana, ni shida kubwa kulithibitisha. Inadaiwa, hilo ndilo limeshamiri na tunasikia malalamiko yake .

Wasomi wana mtazamo kwamba,tatizo sugu hudhibitiwa kupitia kinachoitwa kitaalamu 'etymology' kwamba kutatua jambo kupitia mzizi wake.

Tuanze kwa kujenga mtazamo fulani wa mwanamke kutetea hadhi yake na kumuondoa mwanaume kutoka namna anavomuona.

Kwa vipi? Tulifanyie kazi tatizo la kumuimarisha mwanamke kutoka unenguaji, kukata mauno, mavazi yato na staha na yote ya kujiweka kwa manufaa ya mwanaume. Tuseme hapana!

Hapa tutakuwa tumeanza safari ya kumuimarisha mtoto wa kike na kiume kwa usawa na safari ya vita kupunguza rushwa ya ngono itakuwa imeanza.

Ni bayana, adhabu kali ya kifungo hayatoshelezi vita. Dawa kamili ni kujenga tabia ambayo iko katika etimilojia. Ni busara tutumie elimu na hili inahitaji mjadala mpana, kuhusu kuzama katika yaliyomo katika elimu ya unyago, makuzi na nafasi ya mtoto wa kike kwenye jamii, vivyo hivyo kaka zao.

**Kwa maoni na ushauri, baruapepe: samawatiarts@yahoo.com**

## JE, WAJUA?
## NA MWANDISHI WETU

# Chama cha wafanyakazi ni mkombozi wa mtumishi

BAADHI ya watumishi iwe sekta ya umma au binafsi wanajiuliza hivi kuna manufaa yoyote katika kujiunga na chama cha wafanyakazi? Ni hofu ambayo inahitaji kuondolewa kwa kuwapa wafanyakazi faida na umuhimu wa kuwa mwanachama. Ni maelezo ya Katibu Mkuu wa Chama cha Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Tanzania (Talgwu), Rashid Mtima, anapozungumza na Nipashe.

Anasema faidia za kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi ni nyingi na hapa, anailenga zaidi Talgwu, ili kuhamasisha wafanyakazi kuona umuhimu wa vyama vyao.

Anasema taasisi hiyo ni miongoni mwa vyama vya wafanyakazi nchini ambao jukumu lake kuu ni kujenga nguvu ya pamoja ya kutetea haki na maslahi ya wafanyakazi waliopo chini ya mamlaka za serikali za mitaa.

Anautaja umoja huo kuwa unalenga kuleta umoja, muungano na mshikamano wa wafanyakazi ambao matarajio yao ni kupata ufumbuzi wa matatizo yao.

Talgwu ikiwa ni mwanachama wa Shirikisho la Chama cha Wafanyakazi (Tucta), shirikisho la vyama vya wafanyakazi vinavyotoa huduma kwa umma duniani (PSI) na Mtandao wa Vyama vya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa Afrika (Amalgun) lengo lake ni kuwasaidia wanachama wake.



Tabasamu la mtumishi huyu ni kwasababu ya kuwa mwanachama wa chama cha wafanyakazi . **PICHA: MTANDAO.**

### DHIMA

Mtima anasema Talgwu ina jukumu la kuelimisha, kunatetea na kulinda ajira na za wanachama wake kwa kuzingatia sheria, taratibu, kanuni, miongozo na nyaraka mbalimbali za kazi.

Ndiyo maana Talgwu inawahimiza wafanyakazi wa serikali za mitaa kujiunga na chama chao ili kupata bure msaada wa kisheria pindi mwanachama anapopata tatizo kazini.

Katibu Mkuu anasema chama kimesajiliwa chini ya sheria ya vyama vya wafanyakazi namba 10 ya mwaka 1998, na kupewa nambari ya usajili 010 iliyotolewa mwaka 2000.

Anasema hadi kufikia Oktoba mwaka huu chama hicho kinaunganisha wafanyakazi wote waliopo chini ya mamlaka za serikali za mitaa na taasisi nyingine kilikuwa na wanachama 71,228.

Anasema chama hicho kinachosimamia misingi ya kidemokrasia kwa kufuata miongozo iliyojiwekea na hufanya vikao kwa mujibu wa katiba na kutoka na maazimio ambayo huyatekeleza kwa maslahi ya wanachama wake.

Anasema chama hicho kimekuwa msaada mkubwa kwa wanachama wake kwa kuwasaidia katika changamoto mbalimbali wanazokumbana nazo wanapokuwa kazini.

"Chama kimekuwa kikitoa elimu kwa wanachama kuhusu masuala mbalimbali ya kiutumishi ili wazijue sheria za kazi, majukumu yao na hii inasaidia katika kuepuka migogoro inayojitokeza kati yao na waajiri mahala pa kazi,"anasema Mtima.

Kwa mujibu wa taratibu za chama hicho, endapo mtumishi atajiunga na kupata matatizo ya kiutumishi au mgogoro mahala pa kazi, atashughulikiwa kwa haraka ikiwa ni pamoja na kupata msaada wa kisheria bila gharama yoyote ile kwa sababu chama kimeajiri mawakili kusimamia kesi na migogoro inayowakabili wanachama wake.

Mtima anasema kwa kipindi cha Januari hadi Oktoba mwaka huu, chama kimesimamia kesi 108 zilizokuwa zinawakabili wanachama wake, kati ya hizo zilizomalizika ni 32 na wameshinda kesi 20 na nyingine 76 zinaendelea.

### MAFANIKIO

Akizungumzia mafanikio ya chama hicho, anasema Talgwu imekuwa ikifanya majadiliano na serikali kuhusu kero na changamoto zinazowakabili wafanyakazi na kufikia makubaliano.

"Kwa muktadha huu, Talgwu imepata mafanikio katika nyanja mbalimbali moja wapo ni baada ya serikali iliwarejesha kazini Julai 2017 kuwaondoa kazini watumishi wa umma wasiokuwa na cheti cha ufaulu wa elimu ya kidato cha nne. Baada ya majadiliano, Aprili 2018 serikali iliwarejesha kazini wanachama wa Talgwu," anasema Mtima.

Aidha, kwa kushirikiana na Tucta walishiriki kikamilifu katika mazungumzo na serikali kuhusu kurudishwa kwa kikokotoo cha awali na Rais John Magufuli, alifanya uamuzi wa msingi na kurejesha kikokotoo cha awali.

### MIKOPO

Aidha, Mtima anasema chama kimeanzisha taasisi ya fedha iitwayo Talgwu Microfinance PLC inayotoa mikopo.

Hapo awali ilikuwa inajulikana kama Talgwu Credit Support Ltd kwa ajili ya ununuzi wa hisa za taasisi ulizinduliwa rasmi na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) Sulemani Jafo, Julai mwaka jana.

Anasema madhumuni ya uuzaji hisa ni kukuza mtaji kwa ajili ya kupata uwezo mkubwa wa kukopesha wanachama wake.

Mtima anasema chama kimefanikiwa kuendelea kutoa mafunzo kwa viongozi na wanachama wake kuanzia ngazi ya matawi mpaka taifa ili kwenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi, kisiasa na kijamii yanayotokea duniani na kuanzia Agosti hadi Septemba mwaka huu, chama kilitoa mafunzo ya uongozi kwa viongozi wote wa matawi nchi nzima yaliyokwenda sambamba na mkutano mkuu wa kazi wa miaka miwili na nusu.

### KADI KIELEKTRONIKI

Mtima akitaja mafanikio mengine anasema chama kutoa kadi za kielektroniki za wanachama ni jambo la kujivunia kwani Talgwu ndiyo chama cha kwanza nchini kuanzisha utaratibu huo.

"Ili kujiongezea kipato, chama kimeanzisha ujenzi wa jengo pacha la kitega uchumi lililopo katika Manispaa ya Temeke na hatua zilizopo ni ukamilishaji wa ujenzi.

"Pamoja na mafanikio haya, pia chama kimefanikisha uundwaji na ufanyajikazi wa mabaraza ya wafanyakazi mahala pa kazi na kutoa mchango mkubwa katika marekebisho na utungaji wa sheria mbalimbali za kazi," anasema Mtima.

Katibu Mkuu, anasema wajibu wa chama hicho ni pamoja na kuwaelimisha wanachama wake kuhusu majukumu yao mahala pa kazi ili kuleta tija na kuongeza uzalishaji. Anawakumbusha wanachama kwamba kazi ya chama cha wafanyakazi mahala popote duniani siyo kutetea maovu kazini bali kuhakikisha haki inatendeka.

"Wanachama wote wa Talgwu tekelezeni majukumu yenu ipasavyo kwa mujibu wa sheria na taratibu ili kuepuka migogoro kazini."

Anasema wanachama wa Talgwu wanatakiwa kuzingatia sheria mbalimbali katika utekelezaji wa majukumu ya kila siku ya kazi ikiwamo katiba ya nchi ya mwaka 1977, sheria ya ajira na mahusiano kazini Namba ya 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Utumishi wa Umma namba 8 ya mwaka 2002.

## RIPOTI

# Pesa chafu na simu ni hatari

PESA chafu na simu za mkononi zinaweza kuwa hatari kubwa kwa afya yako, watafiti wameonya.

Fedha hususani zile za thamani ndogo, wanasayansi wanasema zinasababisha magonjwa mengi ya kuhara, miongoni mwa watu wanatumia chakula kinachoandaliwa hotelini, migahawani na vilabuni.

Utafiti uliofanywa miongoni mwa waandaaji wa chakula 395 katika maeneo 15 tofauti ya jiji la Nairobi na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Jomo Kenyatta na kile cha teknolojia nchini humo (JKUAT), kwa ushirikiano na taasisi ya utafiti wa masuala ya tiba ya Kenya (Kemri), na Kitengo cha Utafiti wa matibabu cha jeshi la Marekani Kenya, uligundua.

Ulionyesha kwamba kwasababu pesa na simu za mkononi huwa hazisafishwi hugeuka kuwa maficho ya vimelea vya magonjwa ambao husababisha sumu kwenye vyakula.

Baada ya kupima sarafu kuanzia Sh.1 hadi noti ya Sh.1,000 zinazotumiwa jijini Nairobi, ripoti ilifichua kuwa sarafu za Shilingi 5, 10, 20 ndizo zilizokuwa chafu zaidi zikifuatiwa na noti za Sh. 50, 100 na 200.

"Nyingi kati ya pesa pamoja na simu zilikuwa na bakteria wanaosababisha magonjwa ," matokeo ya utafiti huo yaliwasilishwa kwenye mkutano wa 7 wa Afya na Sayansi wa Afrika Mashariki uliofanyika Dar es Salaam, mapema mwaka huu.

Baya zaidi bado ni kuwahusu wahudumu wa vyakula, hususan wanaogawa vyakula kwa wateja pamoja na wapishi ambao ilibainika kuwa hawazingatii usafi hasa baada ya kupokea simu zao za mkononi.



ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Utandawazi unavyoongeza changamoto, malezi kifamilia



Watoto watafauluje kuwa na mafanikio na maisha bora katika zama hizi za utandawazi? Pengine kupitia malezi bora na familia imara. **PICHA: MTANDAO.**

KINACHOTOKEA shuleni au katika kufaulu kuanzia ngazi za chini hadi mwanafunzi anapofikia hatua ya juu kinategemea mara nyingi msingi kwenye familia unaohusu malezi na makuzi.

Dhana hii ni moja kati ya vigezo vya kampeni ya 'familia bora, taifa imara' ya 'ajenda ya kitaifa kuhusu wazazi.Walezi katika malezi na matunzo ya familia' - Akiwamafa.

Shauku ya kuwa na familia bora ili kuwa na taifa imara labda si ngeni, lakini siyo rahisi kusema kwamba imewahi kufanyiwa kazi kama mkakati wa kitaifa, kwani kimsingi ni eneo la maadili ya jamii.

Msomaji akiangalia chapisho au kipeperushi chenye mchoro kuhusu kampeni hiyo, anakutana na mama na baba anayempakata mtoto mchanga. Anachoweza kuwaza ni mosi kuna hisia kuwa ni watu wa kawaida katika jamii na kwa vile baba ndiye amepakata mtoto, inamaanisha kuwa kuna ushirikiano wa karibu wa malezi katika familia hiyo.

Picha ya kipeperushi hicho inaunganika na dhana nzima ya kampeni hiyo ya familia bora kwa taifa imara.

Kinacholeta changamoto katika kuitafakari kampeni hiyo ya mshikamano wa mama, baba na mtoto mchanga katika familia ya kawaida au ya watu maskini ni mchango wa tofauti za kitabaka katika malezi, elimu na ubora wa familia na hata uimara wa taifa hapo mbeleni.

Shauku hii ni jambo la msingi kwa sababu nchi zilizoendelea na kupiga hatua katika utandawazi zinapata shida na changamoto katika kuhakikisha kuwa watoto wao wanapenda kwenda shule na vijana wao wanazingatia kusoma na kuwa na shauku ya kufaulu na kupata elimu. Ni tatizo kubwa kwa sababu jinsi vijana wanavyoona maisha ni rahisi, ndivyo wanavyodharau masomo na kupuuza elimu.

Ina maanisha kuwa kuna makundi mawili ya vijana katika shule na vyuo na mizizi yake inaanza hata wakiwa watoto, na siyo ajabu ukifanyika utafiti wa chanzo hicho cha kukimbilia starehe badala ya kusoma kwa bidii itaonekana hata katika kipindi cha utoto.

Mtoto anayepata kila kitu atakacho anataka abaki nyumbani azurure au anakwenda shule kama sehemu tu ya kukutana na wenzie na kucheza. Anaweza kufaulu katika madarasa ya chini au elimu ya msingi ambapo inatosha kwa mtoto kwenda shule, lakini sekondari atatakiwa kujisomea hivyo ataanza kukwama, na chuoni hatafika kwa vile hata angeingia atakata tamaa kutokana na kasi ya masomo na mitihani.

Siyo rahisi kusema kuwa uwezo wa kujituma katika masomo unakwenda kinyume na uwezo wa kifamilia wa kumstarehesha mtoto au kijana, yaani anavyozidi kuridhika au kufurahishwa na maisha ya nyumbani ndivyo anavyoelekea kuboronga katika masomo au maisha ya shule kwa jumla.

Kimsingi inategemea vile vile malezi na aina ya mshikamano unaopatikana au kuonekana ndani ya familia, kuwa unajenga maadili gani kwa mtoto. Ziko familia zenye fedha ambazo zina nidhamu na mshikamano kati ya wazazi kana kwamba hawana fedha, na wako pia ambao fedha ikiingia katika maisha inakuwa balaa kwani inaelekea kusambaratika, hata kama hakuna talaka.

Unaweza kukisia haraka kuwa katika familia zenye fedha na maadili imara, utajiri hauharibu maadili na hivyo watoto watakuwa na ari shuleni ili kuwapendeza wazazi wao, kwani wanakuwa na shauku ya kufuatilia mtoto anachokifanya, kwani ni sehemu ya mshikamano wao.

Katika familia ya aina ya pili, ambako hakuna mshikamano kati ya wazazi, uwezekano wa mtoto kufanya vyema ni mdogo kwani hana mtu wa kumwonyesha anachokifanya, au kuulizwa, au kupongezwa akifanya vizuri.

Ndiyo maana suala la malezi bora ni la msingi kwa maendeleo ya mtoto kielimu, ila changamoto ni kuwa malezi siyo kile unachofanya kwa mtoto ila anachokiona.

Katika mazingira kama hayo kunakuwa na mashindano yasiyo rasmi kati ya familia tofauti nani ambaye mwanae atafaulu, zamani ilikuwa hasa ni kwenda sekondari kwani suala la vyuo linakuwa mbali, na halishindanishi familia kwa karibu.

Sasa kwa sehemu kubwa suala la sekondari limetatuliwa ila bado kuna suala la kufaulu, na hata kwa wale waliofika sekondari ni wangapi watatulizana wasome hadi wamalize vyuo, bila kuvurugikiwa na starehe.

Ni mtihani katika familia nyingi ambako suala la mshikamano na dhamira njema ni muhimu, kwani siyo tu linakuwa ni lengo la mwanafunzi kuweka mbele kilicho chema, ila hata 'aura' ambayo ni dhana ya Kihindi ya taswira au picha ya mtu iliyo kama kivuli inayoambatana naye pia pia inaboreshwa.

Aura ni sawa na kitu kinachofanya watu wengine wapendeke kwa urahisi na baadhi wachukiwe kwa urahisi pia, kuwa siyo muonekano wa sura bali mwingiliano wa vitu tofauti.

Jinsi mtu anavyokuwa na furaha ndani yake kuna sura au mwonekano huo wa furaha unaojidhihirisha kwa wengine, hivyo inakuwa rahisi wao kujiambatanisha na mtu mwenye furaha kuliko aliyejiokalia pembeni akitafakari.

Ndiyo maana wanaoshiriki katika kampeni ya 'familia bora, taifa imara' watakuwa na kazi ngumu kupambanua wanacholenga, kwani kwa kawaida shughuli za kijamii kuhusu malezi, kama katika mkakati huo, ni 'wajibu' wa wazazi kwa mtoto. Licha ya kuwa ni vyema na hata lazima kukumbushana majukumu hayo, bado kuna tofauti kati ya wajibu wa wazazi kwa mtoto na wajibu wao kwa wao wenyewe. Ina maana kila kitu hasa kinamtegemea baba, kwani yeye anapotimiza wajibu wake mama akawa na furaha, ndiyo hali hiyo ambayo mtoto atakuwa nayo.

> “Katika familia ya aina ya pili, ambako hakuna mshikamano kati ya wazazi, uwezekano wa mtoto kufanya vyema ni mdogo kwani hana mtu wa kumwonyesha anachokifanya, au kuulizwa, au kupongezwa akifanya vizuri.

Watoto wanaokulia katika mazingira ya furaha ndiyo wanaofanya vyema zaidi kwa dhamira ya kuendeleza furaha hiyo nyumbani wanapofaulu vizuri, wakati watoto wanaokulia katika familia duni wanaota kuwa na uwezo wa kuondoka nyumbani, au kupata raha hata kama bado wako nyumbani.

Mengine ni matatizo 'nyemelezi' yanayotokana na shauku ambazo tayari zimeanza kujijenga katika hisia za mtoto, kwa mfano mtoto mwenye changamoto za hapa na pale kila siku anakutana na 'fataki' ana mtumainisha vipesa vya kila wakati. Anaanguka mtegoni mara moja.

Sasa tatizo la msingi la kampeni hiyo ni kigezo cha 'familia bora,' kuwa itapatikana vipi katika utandawazi huu? Uwezo wa washiriki familia kuzuia vishawishi vinavyopatikana kwa urahisi kwa kutumia nyenzo rahisi tu kwenye dunia huru si mkubwa, au unategemea na makuzi ya hao hao wanafamilia na jinsi walivyo karibu na wazazi wao.



WADAU
**SABATO KASIKA**

# Sauti za wadau

MOJA ya vigezo vya Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) kwa wanafunzi, ni kutambua nani apate mkopo na kuwapa kipaumbele yatima na wasiojiweza. Wadau wanasemaje?



**MARY MBELE (MWALIMU SEKONDARI DUNDA, BAGAMOYO PWANI)**

KABLA ya yote nianze kuelezea faida za vigezo vya mikopo ya wanafunzi. Kwanza tofauti ya kitabaka.

Yaani wenye nacho na wasio nacho katika elimu linapungua.

Pili ni kwamba inaongeza takwimu kubwa ya wahitimu kwa kuwa maskini ambao ingewabidi kukosa elimu sasa watahitimu pamoja na wanaosomeshwa na wazazi wao.

Kwa upande wa hasara ni kwamba vigezo vinawachuja walengwa ambao walistahili na pia mkopo ni mkopo wala siyo msaada, hivyo kuwachuja raia wengine eti wana uwezo ni kuwanyima mkopo, ninaona kuna tatizo kidogo.

Wote wanaokopa na watalipa, vitafutwe vyanzo vya fedha vya kutosha, ili kila mwombaji awezeshwe. Vinginevyo kutakuwa na matabaka, ambayo hayapaswi kuwapo.

Elimu kwa wote maana yake ni kwamba kila mtu ana haki ya kupata elimu. Kuweka vigezo kama hivyo ni sawa na kuwafanya wengine wakose elimu au washindwe kufikia malengo yao katika elimu.

Hapa itakuwa ni sawa na kuwatenga au kuwabagua watoto wa viongozi bila kujali kama wana uwezo wa kuwalipia mikopo ya elimu ya juu.

Binafsi ninaamini kuwa mtu anapokuwa na kipato kikubwa majukumu nayo yanakuwa makubwa, kwa hiyo kusema tu kwamba watoto wa wakurugenzi wa kampuni au mashirika hawatakiwi kupata mikopo, siyo jambo jema.

Wote wapewe nafasi sawa za kupata mikopo, ili mradi kusiwe na upendeleo kama ilivyokuwa ikitokea miaka ya nyuma wakati wengine tukisoma elimu ya juu.



**FARES KAJIRU (MDAU WA ELIMU NA MKAZI WA DAR ES SALAAM)**


VIGEZO vya Bodi ya Mikopo Elimu ya Juu ni vizuri, lakini pia kuna haja ya kuvitafakari sana hasa kwenye suala la watoto wa vigogo ambao nimewahi kusikia kwamba wanatakiwa wajitemee kwa lengo la kuwasaidia watoto wa maskini wapate mikopo hiyo.

Kwa maoni yangu ni kwamba hili jambo linataka umakini sana katika kulitekeleza ingawa sijajua kama ni kisera au kisiasa, kwa sababu yapo mambo kadhaa ya kujiuliza kuwa mtumishi anayezungumziwa hapa ni wa ngazi ipi. Kwa mfano muuguzi daraja la kwanza Hospitali ya Mwananyamala na Katibu Mkuu Kiongozi.

Je, kwa kuwa hawa wote ni watumishi, watoto wao ni sawa wote wakose mkopo kwa kuwa ni watumishi? Ukiangalia lazima bado tujiulize ni aina gani ya watumishi watashughulikia suala hili, uadilifu wao na weledi ukoje? Je, wataweza kuvumilia watoe mikopo kwa watoto, ambao wazazi wao sio wafanyakazi na hawana uwezo?

Ni vyema tukatambua kuwa wapo watoto, ambao wazazi wao sio watumishi lakini wana uwezo wa kusomesha. Je, hao watapewa wakati wale wa watumishi wasio na ujira unaowawezesha kusomesha wamekosa? Kuwe na vigezo vinavyotoa fursa sawa kwa kila mtoto wa Kitanzania.

Mzazi kuwa kiongozi au mtumishi sio kuwa tajiri, lakini lengo liwe kuwainua wale wote ambao vipato vyao ni vidogo na udogo huo uwe na kigezo bayana. Kwa mfano mfanyakazi wa kipato cha chini ya milioni moja kwa mwezi, mtoto wake apewe mkopo kwa asilimia kama 80 na wale wa chini ya laki sita wapate asilimia 100 sawa na wale wasiojiweza kabisa.



**MBURA ZAKARIA (MKAZI WA JIJINI DAR ES MWANZA)**

KWA jinsi ninavyoona, vigezo hivi ni changamoto kubwa kwa wanafunzi wanaotafuta elimu ya juu na hasa wale wanaotajwa kuwa ni watoto wa wakubwa, bado wanatakiwa kukopeshwa fedha kwa kutambua kuwa mzazi awe kiongozi au nani, lazima tutambue kuwa cheo ni dhamana, kwani leo mzazi anaweza kuwa mkurugenzi, lakini akajikuta amefukuzwa, kushushwa cheo au kustaafu.

Sasa kama kuna watoto alikuwa anawalipia mkopo wa elimu ya juu itakuaje? Ndio maana nikasema kuwa vigezo hivi ni changamoto na zaidi ya hapo vinaweza kutafsiriwa kuwa ni ubaguzi. Niliwahi kusoma vigezo ambavyo Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu kwa mwaka wa masomo wa 2016/2017, vitaja kuzingatia vipaumbele vitano vya kitaifa vinavyoendana na mpango wa maendeleo wa taifa wa miaka mitano ijayo, huku kipaumbele kwa wakopaji watakaosoma mafunzo ya kuzalisha wataalamu wanaokidhi mahitaji ya kitaifa katika fani zilizochaguliwa, ambazo ni za sayansi za tiba na afya, ualimu wa sayansi na hisabati, uhandisi wa viwanda, kilimo, mifugo, mafuta na gesi asilia, sayansi asilia na mabadiliko ya tabianchi na sayansi za ardhi, usanifu majengo na miundombinu.

Mimi sina tatizo na hilo, lakini wasiwasi wangu ni kwa watoto wa viongozi, kuambiwa kuwa hawaruhusiwi kuomba, ingawa hakuna ufafanuzi zaidi. Sijui kama vigezo hivyo bado vipo, Iwapo vinaendelea kutumika, basi hii ni sawa na kubebesha mzigo wazazi wao, ambao sidhani kama wote wana uwezo wa kumudu kuwalipia.



**SOMOE DANIEL (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

SIYO vibaya kuwapa kibaumbele watoto wa maskini ambao miaka ya nyuma walikuwa wakiteseka kupata elimu ya juu kwa sababu mikopo ilikuwa ikiishia kwa wachache wenye uwezo.

Lakini pia ni vyema kukawa na ufuatiliaji wa hali ya juu kuwabaini vizuri wale wanaotoka katika familia duni na wenye uwezo. Kwa kawaida huwa tunasema eti wakulima ni maskini, lakini niwajulishe kuwa wapo baadhi yao wana uwezo mkubwa wa kifedha.

Mie nina rafiki yangu anajishughulisha na kilimo cha mboga, anaingiza zaidi ya milioni 4 kwa mwezi. Sasa huyo akiwa na mtoto wa kuingia chuo kikuu atapewa kipaumbele eti kwa sababu baba yake ni mkulima hana kitu? Kinachotakiwa kufanywa ni kuziba mianya ya ujanja ujanja, ambayo imekuwa ikidaiwa kuwapo kwenye utoaji wa mikopo.

Hilo likifanyika linaweza kusaidia kudhibiti fedha kwenda mikononi mwa wasiohusika, lakini kugawa wanafunzi kwa kivigezo vya yatima na maskini, sidhani kama ni njia ya kuwezesha kutatua kero kwenye utoaji wa mikopo. Wawe ni watoto wa watumishi au wa watu wasiojiweza kiuchumi, wote wawezeshwe, ili watimize ndoto zao kwenye elimu.

Nirudie kusema kwamba wapo wakulima wana uwezo mkubwa tu kifedha zaidi ya watumishi, kwa hiyo vigezo viliangalie hilo kwa ajili ya kusaidia watoto wote wa Kitanzania wanaohitaji elimu ya juu waweze kusema bila kukumbana na vikwazo visiyo vya lazima mbele ya safari.



**AMINATHA KYANDO (MKAZI WA JIJINI DAR ES SALAAM)**

KUMEKUWAPO na malalamiko kutoka kwa wanafunzi wa elimu ya juu hasa kwenye suala la vigezo vya kupata mikopo.

Kwa mfano mwaka wa masomo wa 2018/2019, wanafunzi waliwahi kuiomba bodi hiyo kuondoa ukomo wa idadi ya wanafunzi, kwasababu tu ya vigezo na masharti yakiwamo ya kuwapa kipaumbele yatima na wale wanaotoka katika familia maskini.

Sioni ugumu wowote kutoa mkopo kwa wanafunzi wote, sasa kama wengine wanaachwa wajitegemee kwasababu eti wazazi wao wana uwezo kiuchumi.

Je, ikitokea uchumi huo ukaporomoka ndipo watapewa mikopo? Ninauliza hivyo kwa sababu, katika maisha kuna kupanda na kushuka. Kwa maoni yangu, sioni umuhimu wa kuweka vigezo vya aina hiyo, na siyo vizuri kuviweka kwani ni kama ubaguzi.

Mtoto wa maskini na mwenye uwezo kifedha, wote wana haki ya kupata mkopo. Ikumbukwe kuwa huo ni mkopo ambao kila mwanafunzi ana haki ya kuupata na kurejesha. Inashangaza kuona kunakuwapo na vigezo ambavyo vimejificha kwenye dhana ya umaskini.

Ninadhani ipo haja kwa bodi kuachana na utaratibu huo, ili kwamba mwanafunzi akiwa ni mtoto wa mkurugenzi au meneja katika kampuni binafsi yanayotambuliwa na mamlaka za mapato naye akopeshwe.





# Mimba zawatesa wanafunzi miezi 9

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

JUMLA ya wanafunzi 82 wa shule za msingi na sekondari katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wamekatishwa masomo yao kwa sababu ya kupata mimba kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu.

Hayo yalibainishwa kwenye risala iliyoandaliwa na vituo vya taarifa na maarifa Wilaya ya Mbeya na kusomwa na Yustina Ngeleza wakati wa maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia ambayo kitarafa yalifanyika kwenye kijiji cha Mantanji.

Ngeleza alisema miongoni mwa sababu zilizosababisha idadi hiyo ya wanafunzi kuacha masomo ni umbali wanaotumia kwenda shule na wakiwa njiani hupata vishawishi kutoka kwa bodaboda.

Alisema bodaboda ambao ndio wahusika wakubwa kuwapatia wanafunzi mimba, huwarubuni watoto kwa kuwapa lifti na zawadi wakidai huwasaidia hatimaye hufanya nao mapenzi ambayo utajwa kama ukatili wa kingono.

Aliongeza kuwa jumla ya kesi 158 za vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto kuanzia Januari hadi Septemba mwaka huu zimeripotiwa kwenye vyombo mbalimbali vya sheria ikiwamo polisi na mahakamani.

Alisema kati ya kesi hizo watoto 100 wa kike na 58 wa kiume walifanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia katika maeneo mbalimbali wilayani Mbeya na kwamba ukatili uliokithiri zaidi ni wa kingono.

Mgeni rasmi katika maadhimisho ya Siku 16 ya Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Mwalingo Kisemba, alisema waendesha bodaboda ndio watu wa kwanza kuharibu watoto wa shule.

Alisema ili kutatua tatizo hilo serikali kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kutoa mafunzo ya mara kwa mara kuhusu ukatili wa kijinsia dhidi ya watoto.

Alidai njia hiyo itasaidia kuongeza uelewa kwa waendesha bodaboda juu ya athari za ukatili wa kijinsia kwa watoto, ambao umechangia kwa kiasi kikubwa kukatisha ndoto zao za kusoma.

"Mtoto anaona bora amueleze shida zake dereva bodaboda badala ya mzazi au mlezi kwa sababu sio rafiki yake, yupo bize na biashara hajui maendeleo ya mtoto shuleni wakati huo mwendesha bodaboda anatumia muda mwingi kukaa na binti na kutimiza mahitaji yake sasa unafikiri matokeo yake ni nini?" Alihoji Mwalyego.

Mwenyekiti wa vituo vya taarifa na maarifa wilayani Mbeya, Flora Mlowezi, alisema wameandaa mikakati kabambe ya kukabiliana tatizo la mimba shuleni kama vile kuunda klabu za wanafunzi ambazo kupitia hizo watoto wa kike watajadiliana vikwazo wanavyopata na namna ya kuviepuka pamoja na kamati za ulinzi kwa watoto.

Sambamba na hilo, alisema wataendelea kutoa elimu ya jinsia kwa shule zote za msingi na sekondari na kuikumbusha serikali kuongeza bajeti katika ujenzi wa hosteli ili kusaidia watoto wa kike kukaa hosteli.

# Mpango maalumu kukabili maambukizo mapya ya VVU

**Na Nebart Msokwa, KYELA**

MKOA wa Mbeya kwa kushirikiana na wadau umeanzisha mpango maalumu wa kukabiliana na ongezeko la maambukizo mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa kuzishirikisha taasisi za dini na wazee wa mila kuhamasisha watu kupima afya zao.

Hayo yalisemwa juzi na Mratibu wa Tume ya Kudhibiti Ukimwi Tanzania (Tacaids) wa Mkoa wa Mbeya, Emmanuel Petro, wakati wa maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani ambayo kimkoa yalifanyika Kijiji cha Bukinga kilichopo Kata ya Muungano wilayani Kyela.

Alisema kwa mujibu wa utafiti uliofanywa kati ya mwaka 2012 na 2019 maambukizo katika mkoa huo yameongezeka kutoka asilimia 9 mpaka asilimia 9.2 na kuufanya mkoa huo kuendelea kushika nafasi ya tatu baada ya Njombe na Iringa.

Petro alisema hali hiyo imeulazimu mkoa kwa kushirikiana na wadau kuanza kuchukua hatua za makusudi za kukabiliana na ongezeko hilo la maambukizo ili kufikia malengo ya kufikia ya serikali ya 90 tatu.

"Maambukizi katika Mkoa wetu yamekuwa yakiongezeka, sasa tumeanza kushirikiana na taasisi mbalimbali wakiwamo wenzetu wa World Vission kukabiliana na maambukizi haya kwa kuwatumia viongozi wa dini na wa mila kutoa elimu," alisema Petro.

Alisema kwa sasa utafiti unaonyesha kuwa maambukizi mapya yanawakabili zaidi vijana wenye umri kati ya miaka 15 mpaka 24 na kwamba kundi hilo linachukua asilimia 40 ya maambukizi yote na hivyo nguvu kubwa inaelekezwa kwenye kundi hilo.

Alisema watoto wa kike ndio wanaopata maambukizi zaidi kwa maelezo kuwa kati ya vijana wanaopata maambukizi mapya, asilimia 80 ni wa kike hali ambayo ni hatari zaidi.

Meneja wa Mradi ujulikanao kwa jina la 'Pepfar FBO Initiative' unaotekelezwa na Shirika la World Vission, Frida Chilimo alisema mradi huo unalenga kuwashirikisha viongozi wa dini kwa sababu wao ndio wana watu wengi wanaowaamini na hivyo ni rahisi kuwashawishi.

Alisema mradi unalenga kuwahamasisha wananchi kupima afya zao na kwa wanaobainika kuwa na maambukizi waingizwe kwenye matumizi ya dawa ili kufubaza VVU na kupunguza uwezekano wa kuwaambukiza wenza wao.

Alisema mradi huo unatekelezwa katika wilaya tatu za mikoa ya Mbeya na Songwe ambapo kwa Mkoa wa Mbeya unatekelezwa katika Wilaya ya Rungwe na kwa Mkoa wa Songwe unatekelezwa katika Wilaya za Ileje na Mbozi.

"Kwa Rungwe tunashirikiana na Hospitali ya Igogwe, lakini kwa Songwe tunashirikiana na Shirika la Caritus, na kwa mikoa hii tumekuja kwa mara ya kwanza baada ya kubaini kuwa ongezeko la maambukizi ni kubwa zaidi," alisema Chilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema aliwataka wananchi kila mmoja achukuwe tahadhari juu ya maambukizi kwa maelezo kuwa ukimwi una athari nyingi kwa jamii.



Mkuu wa Dawati la Jinsia na Wanawake Jeshi la Polisi Mkoa wa Mbeya, Janeth Masangano (mwenye sare za polisi), akitoa elimu kwa wananchi wa Kijiji cha Bikinga, wilayani Kyela juzi, kuhusu masuala ya ukatili wa kijinsia huku wananchi hao wakiendelea kunywa pombe za kienyeji, ambapo alisisitiza kuwa ulevi wa kupindukia ni miongoni mwa vyanzo vya ukatili pamoja na maambukizo ya Virusi vya Ukimwi. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Mzumbe kufanyia utafiti tatizo ajira

**Na Nebart Msokwa, MBEYA**

UONGOZI wa Chuo Kikuu cha Mzumbe tawi la Mbeya, umesema unakusudia kufanya utafiti juu ya tatizo la ajira nchini na mbinu za kumaliza tatizo hilo ili kupunguza idadi ya vijana wanaohitimu bila kuajiriwa.

Hayo yalisemwa na Kaimu Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Pius Maneno, wakati wa mahafali ya 18 mwishoni mwa wiki kwenye viwanja vya chuo hicho.

Alisema maeneo yanayolengwa kwenye utafiti huo ni kujua idadi ya ajira zinazohitajika nchini ikilinganishwa na idadi ya watu wanaohitimu mafunzo yao kwenye vyuo mbalimbali pamoja na kujua aina ya ajira hizo.

"Lakini tutaangalia uwezo wa vijana wetu wanaohitimu vyuo na vyuo vikuu katika kujiajiri na kuajiriwa, vilevile tutaangalia matumizi ya teknolojia ili tusije tukawa tunaachwa na mataifa mengine kwenye matumizi ya teknolojia za kisasa," alisema Maneno.

Alisema chuo kimeanza kuimarisha zaidi mafunzo kwa vitendo ili kuwawezesha wahitimu kujiajiri badala ya kuzidisha nadharia ambazo haziwezi kuwasaidia hasa wanapokosa kuingia kwenye mfumo wa ajira rasmi.

Vilevile, alisema chuo hicho kimeanzisha kitengo maalumu cha kutafuta vipaji vya wanafunzi ili kuwaendeleza na kuwafanya wajiajiri kupitia vipaji hivyo.


Alivitaka vyuo vikuu nchini kujikita zaidi kufanya utafiti ili kufanikisha azma ya serikali ya kufikia uchumi wa kati ifikapo 2025 kupitia viwanda.

Makamu Mkuu wa Chuo hicho, Prof. Lugano Kusiluka, alisema kwa sasa chuo hicho kimeimarika na kinatoa wahitimu ambao wanafanya kazi nzuri wanapokuwa wameajiriwa na hata waliojiajiri.

Alisema mwaka huu wanafunzi waliohitimu ngazi mbalimbali wako 1,023 na kwamba wanawake wapo 544 sawa na asilimia 53.2 wakati wanaume ni 479 sawa na asilimia 46.8 na hivyo kuwa miongoni mwa vyuo vyenye usawa wa kijinsia.

Nao baadhi ya wahitimu walisema chuo hicho kimeanzisha utaratibu mzuri wa kuwapatia vyuo wanafunzi mara tu baada ya mahafali tofauti na ilivyokuwa miaka ya nyuma ambapo walikuwa wanasubiri mpaka miezi sita.

Elius Ndabila, alisema utaratibu huo unawawezesha wahitimu kuingia mtaani kutafuta ajira wakiwa tayari wana vyeti hali ambayo inawafanya waaminike tofauti na zamani.





## Shonza afunda maofisa habari

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

NAIBU Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Juliana Shonza, amewataka maofisa habari wa serikali kutopuuza mitandao ya kijamii na badala yake waitumie katika kutangaza mafanikio yanayofanywa na serikali ya awamu ya tano.

Shonza alitoa kauli hiyo jijini hapa wakati akifungua mafunzo ya siku tano ya maofisa habari wa serikali yanayofanyika jijini Dodoma yaliyoandaliwa na Chama cha Maofisa Mawasiliano Serikalini (TAGCO) kwa kushirikiana na Idara ya Habari (Maelezo).

Alisema ni vyema maofisa hao wakashirikiana na Msemaji Mkuu wa Serikali, Dk.,Hassan Abbas, kutangaza mafanikio ya serikali.

Naibu Waziri huyo alisema mitandao hiyo ikitumiwa vizuri itasaidia kufikisha ujumbe kwa wananchi kwa haraka ili wajue serikali yao inafanya nini katika kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2015-2020.

"Nimefurahi kuona moja ya mada katika mafunzo haya ni matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii, tuisikilize vizuri maana imekuwa ni changamoto kubwa sana kwetu, hatutilii mkazo katika mitandao ya kijamii, tunapaswa tubadilike sasa," alisema.

Alifafanua wanapoelekea kwenye uchaguzi Mkuu mwaka 2020 Rais amefanya kazi kubwa ya kugusa maisha ya Watanzania, hivyo ni lazima wajue ili wawe na imani na serikali yao.

Aliongeza Watanzania hivi sasa wameamka wanahitaji kujua nini serikali yao inafanya ili kuleta maendeleo.

"Inasikitisha kuona watu wanaisema vibaya serikali na nyie maofisa wake mpo na mnaona jinsi gani serikali ya awamu ya tano inavyopigania kuleta maendeleo ikiwamo kutekeleza miradi mbalimbali hapa nchini," alisema.

Naye Msemaji wa Serikali, Dk. Abbas Hassan, alisema mafunzo hayo ni muhimu kwa wanahabari kwa kuwa yatasaidia kuongeza weledi katika taarifa za serikali kwa ujumla.

Alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwaongezea weledi katika utengenezaji wa vipindi vya runinga ambavyo vingi vinakuwa havina ubora.

Katibu wa TAGCO, Othman Njaidi, alisema ofisa habari anapaswa kuwa na weledi katika utoaji wa taarifa za serikali ikiwamo kutengeneza video nzuri ambazo zinamaudhui ya kufanya msikilizaji na mtazamaji kupata ujumbe husika.

**"Nimefurahi kuona moja ya mada katika mafunzo haya ni matumizi sahihi ya mitandao ya kijamii, tuisikilize vizuri maana imekuwa ni changamoto kubwa sana kwetu, hatutilii mkazo katika mitandao ya kijamii, tunapaswa tubadilike sasa," alisema.**

# Kikombo kulipwa fidia wiki hii

**Na Renatha Msungu, DODOMA**

MKURUGENZI wa Jiji la Dodoma, Godwin Kunambi amesema ulipaji fidia kwa wananchi 1,526 wanaopisha ujenzi wa Makao Makuu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Kata ya Kikombo, utaanza wiki hii.

Awali, Rais John Magufuli akiweka jiwe la msingi la ujenzi huo, aliagiza wananchi hao wanaodai fidia ya jumla ya Sh. bilioni 3.399 kulipwa ifikapo Desemba mosi mwaka huu.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kunambi alisema fedha ipo tayari lakini wanasubiri uhakiki wa majina ya watu wanaolipwa fidia kutoka Wizara ya Fedha ukamilike.

"Fedha ipo tunasubiri uhakiki ukamilike ndio tuanze utaratibu wa kugawa fidia hii kwa wananchi," alisema.

Aidha, alisema jiji linaendelea na taratibu za kuwapa elimu wakazi wa eneo hilo na ufunguaji wa akaunti za benki kwa kuwa malipo yao yataingizwa benki.

Aliwataka wakazi wa eneo hilo kutokuwa na wasiwasi wowote juu ya fidia hiyo ambayo iliagizwa kulipwa na Rais wakati akiweka jiwe la msingi katika eneo hilo la Kikombo.

"Wenzetu wa Wizara ya Fedha wapo katika hatua za mwisho za kukamilisha uhakiki wa majina na baadaye watayawasilisha jiji kwa ajili ya kuanza kulipa fidia," alisema.

Akizungumza kuhusiana na kuboresha Jiji la Dodoma, Kunambi alisema wanatarajia kuboresha stendi ya daladala ya Sabasaba kutokana na kuanza msimu wa mvua.

Kadhalika, aliwaasa wakazi wa jijini hilo kuacha kununua viwanja ovyo ambavyo havijapimwa ili kujiepusha na migogoro.

Alisema hivi sasa viwanja halali hupatikana eneo la jiji na si vinginevyo.

Katika hatua nyingine, mkurugenzi huyo aliwataka vijana, wanawake na watu wenye ulemavu kuchangamkia mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri ili kujikwamua kiuchumi.

Alisema hadi sasa halmashauri imetoa Sh. milioni 900 kati ya Sh. bilioni 3.7.



Mkuu wa Wilaya ya Chemba, Simon Odunga (kulia), akisikiliza kero za wananchi wa Kijiji cha Tandala, wilayani humo, mkoani Dodoma mwishoni mwa wiki, alipofika kijijini hapo kuhimiza umuhimu wa kilimo bora. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Wizara yaanza kutumia mfumo wa 'Force account'

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

WIZARA ya Maji, imeanza kutekeleza miradi ya maji kwa kutumia mfumo wa 'Force account' badala ya makandarasi ili kuondokana na matumizi ya gharama kubwa na ucheleweshaji wa miradi hiyo.

Hayo yalielezwa na Waziri wa Maji, Prof. Makame Mbarawa, katika ziara yake wilaya ya Chamwino ya kukagua ujenzi wa miradi mbalimbali ya maji.

Alisema hadi sasa kuna miradi 40 ambayo inatekelezwa kwa kutumia mfumo huo na serikali imeokoa fedha nyingi na utekelezaji wake unachukua muda mfupi ikilinganishwa na kutumia makandarasi.

Alieleza kuwa wizara itatoa vibali vya kujenga miradi ambayo wataalamu wake hawana uwezo wa kujenga na si vinginevyo.

"Kwa sasa wizara imefuta utaratibu wa kutangaza zabuni kwa ajili ya kuwapata makandarasi kwa kuwa utaratibu huo unachelewesha miradi na kusababisha gharama kubwa ikilinganishwa na wizara kutumia wataalamu wake."

"Hizi kazi za kuchimba mitalo, kujenga tangi la maji la lita milioni mbili, kuchimba visima tuna uwezo kubwa tuna wataalamu wazuri kushinda hata hao makandarasi, naomba nyie wahandisi muelewe na pale mkileta vibali vya kusaini kwa ajili ya makandarasi kujenga miradi hiyo mimi si saini," amesema.

Alitolea mfano kuna mradi wa maji ulikuwa ujengwe Wilaya ya Nkasi eneo la Kilando ambao kama wangetumia mkandarasi ingegharimu Sh.bilioni 4.6 lakini wamejenga kwa Sh. bilioni 3.2.

"Hata Wakala wa Uchimbaji Visima na Ujenzi wa Mabwawa (DDCA) wakileta gharama kubwa nawaondoa siwapi kazi, hatutaki nao wawe na gharama kubwa, kuna miradi ambayo wataalamu wa wizara wana uwezo mkubwa wa kufanya lazima tujengeane uwezo wa kazi," alisema.

Aliongeza: "Miaka yote tumekaa hii wizara hatujengi uwezo hata kubadilisha nati anaitwa mkandarasi, wakati nyumbani kwako ukitaka kubadili nati unafanya mwenyewe, najua makandarasi wanapiga vita utaratibu huu, lakini niwaambie serikali imeamua kutumia utaratibu huu."

Kadhalika, alisema mradi wa maji Chamwino unatekelezwa na serikali kwa asilimia 100 wenye gharama ya Sh.milioni 574 na tayari kiasi cha Sh.milioni kimeshatolewa.

"Tunajenga wenyewe tayari visima vitatu vimeshachimbwa, sasa tunajenga mitandao ya maji mradi utachukua miezi mitatu kama tungetumia mkandarasi angechukua zaidi ya miezi tisa, na serikali inapoteza fedha nyingi sana," alisema.

Awali, akisoma ripoti ya utekelezaji miradi wilayani Chamwino, Kaimu Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) Chamwino, Christina Msengi, alisema hadi Oktoba mwaka huu, watu 264,484 wanapata majisafi na salama sawa na asilimia 65 ya wakazi wote.



# Wahoji manufaa gawio la mashirika

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamehoji Zanzibar kutofaidika na mgawo wa fedha za gawio la mashirika ya umma kwa taasisi zenye sura ya Muungano.

Hilo liliibuliwa jana na Mwakilishi wa Mpendae, Mohamed Said Dimwa, aliyetaka kujua mgawo wa mashirika ya umma unaofanyika Tanzania Bara unainufaishaje Zanzibar.

Mwakilishi huyo alihoji wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi huku akitaka kujua gawio la mashirika hayo linainufaishaje Zanzibar.

Dimwa alisema hivi karibuni Rais John Magufuli alipokea gawio la fedha za mashirika ya umma zaidi ya Sh. bilioni 2.75 yakiwamo mashirika yenye sura ya Muungano na fedha zake hukusanywa zikitokea Zanzibar katika vyanzo vyake vya mapato. "Kutokana na fedha hizo, Zanzibar inanufaikaje kwa sababu baadhi ya mashirika yanayotoa gawio yana sura ya Muungano?" Alihoji.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mohamed Aboud, alisema ziko taasisi za Muungano zilizoko Zanzibar ambazo huchangia gawio la fedha zinazoingia katika mfuko mkuu wa serikali.

Aliyataja mashirika hayo kuwa ni Shirika la Mawasiliano ya Simu Tanzania (TTCL), Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) na Shirika la Posta (TPC).

"Tumefanya mawasiliano na wenzetu wa Wizara ya Fedha na Mipango ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano kuulizia kuhusu suala la mgawo wa fedha zinazotokana na gawio kwa taasisi na mashirika ya umma ambayo ni ya Muungano," alisema.



Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis (kushoto), akizungumza na wajumbe wanawake wa Baraza la Wawakilishi, nje ya ukumbi wa baraza hilo, Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uvunjaji nazi, matikiti njiapanda kwatikisa Baraza la Wawakilishi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

VITENDO vya baadhi ya watu Zanzibar kuvunja matikiti maji, mayai viza na nazi njia panda ikiwamo barabara ya Maisara mkabala na nyumba ya Rais mstaafu Ali Hassan Mwinyi, vimesababisha uchafuzi wa mazingira katika maeneo hayo.

Vitendo hivyo vimekuwa vikifanywa na baadhi ya wananchi kwa imani za kishirikina na kunaswa na kamera za ulinzi (CCTV) zilizofungwa katika maeneo ya barabara za mjini Unguja.

Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Shamata Shaame Khamis, alisema jana kuwa kamera hizo zilizofungwa, zinaona matukio yote yanayofanywa katika maeneo mbalimbali ya mji kwa lengo la kulinda na kudumisha amani na utulivu wa nchi kwa faida ya wananchi na watalii wanaoitembelea Zanzibar.

Aliyasema hayo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Paje, Jaku Hashim Ayoub, aliyetaka kujua kamera hizo zinasaidia vipi katika kuwatambua watu hao wanaofanya kafara katika njia panda za barabara na kuchafua mazingira.

"Serikali inatambua vitendo vinavyofanywa na baadhi ya wananchi vikiwamo vya kuvunja matikiti maji, mayai viza na nazi katika maeneo ya njia panda ya barabara ya Maisara vitendo ambavyo vinasababisha uchafuzi wa mazingira" alisema Shamata.

Alisema kamera hizo zipo kwa ajili ya kutambua matukio yanayotokea katika maeneo husika na kwamba lengo kuu ni kuimarisha ulinzi na usalama wa nchi.

Shamata alisema endapo vitendo vya kafara vinavyofanywa na baadhi ya wananchi vitaripotiwa katika vyombo vya sheria na kuhitaji ushahidi wa aliyefanya kitendo hicho, CCTV zilizopo maeneo hayo zina uwezo wa kumtambua mtu aliyefanya kitendo hicho.

"Mheshimiwa Spika hadi sasa hakuna mtu aliyekamatwa akivunja matikiti maji na nazi kupitia CCTV kamera kwa sababu hakuna mtu wala chombo chochote kilichoripoti tukio hilo na kuomba msaada wa CCTV katika kutoa ushahidi," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema matukio hayo yenye nasaba na imani za kishirikina, yanaweza kutishia amani na si mambo mazuri na hayapendezi kwa jamii.

Naye Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Muhammed Aboud, aliwataka wajumbe wa baraza hilo kuwaelimisha wananchi kuachana na matukio hayo ambayo yanaweza kusababisha ajali za barabarani.

## Wafanyabiashara ruksa kufanya watakavyoweza

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara na Viwanda, imeweka biashara huria kwa wafanyabiashara wa Zanzibar, imeelezwa.

Kutokana na mpango huo, mfanyabiashara yoyote anaweza kufanya biashara anayoipenda kutokana na uwezo wake wa kifedha.

Hayo yalisema na Naibu Waziri wa Biashara na Viwanda, Hassan Khamis Hafidh, katika kikao cha Baraza la Wawakilishi kinachoendelea Chukwani, Zanzibar.

Naibu Waziri Hafidhi alisema hayo jana wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Chakechake, Suleiman Sarahani, aliyetaka kujua serikali imeona biashara gani ambazo mpaka sasa hazijapewa kipaumbele na wafanyabiashara.

Alisema kuna fursa nyingi za uwekezaji katika viwanda, uvuvi wa bahari kuu na utalii ambazo wafanyabiashara wa Zanzibar wakizifanya watapata kipato na kukuza uchumi wa nchi.

Hafidh aliwaomba wafanyabiashara waangalie kuwekeza katika maeneo ya uvuvi wa bahari kuu na usanifu wa mazao na wizara iko tayari kushirikiana nao na kuwapa miongozo stahiki.

Alisema miongoni mwa biashara ambazo hazijapewa kipaumbele na wafanyabiashara wa Zanzibar ni uvuvi wa bahari kuu, viwanda vya kusarifu mazao ya kilimo kama vile nyanya, machungwa na matunda mengine.

Pia alisema wizara inachukua jukumu la kuwahamasisha wafanyabiashara wa Zanzibar kuingia katika biashara ambazo zitawawezesha kukuza kipato chao na kukuza uchumi wa nchi.

"Kama inavyojulikana kwamba Tanzania imeingia katika sera ya kukuza viwanda nchini na kwa upande wa Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara inawaomba wananchi wake kuwekeza katika viwanda mbalimbali nchini kwa kuwatengea maeneo kwa kila wilaya kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo na vya kati," alisema.

**"Kama inavyojulikana kwamba Tanzania imeingia katika sera ya kukuza viwanda nchini na kwa upande wa Zanzibar kupitia Wizara ya Biashara inawaomba wananchi wake kuwekeza katika viwanda mbalimbali nchini kwa kuwatengea maeneo kwa kila wilaya kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda vidogo na vya kati," alisema.**

# Mbunge aiombea ushirikiano Osha

**Na Gwamaka Alipipi**

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Kagera (CCM), Oliver Semuguruka, amewashauri viongozi wa serikali kushirikiana na Wakala wa Usalama na Afya Mahali pa Kazi (OSHA) katika kuboresha mazingira ya kazi.

Amesema viongozi wanapaswa kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Osha katika kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya kiusalama na afya ambavyo husababisha ajali na magonjwa katika sehemu nyingi za kazi.

Aliyasema hayo jana alipotembelea ofisi za Osha jijini Dar es Salaam kufanya mazungumzo na uongozi kwa ajili ya kuweka mikakati ya kuhamasisha uzingatiaji wa viwango vya usalama na afya mahali pa kazi kwa watu wenye ulemavu.

"Baada ya Osha kuniteua kuwa balozi wa watu wenye ulemavu katika masuala yanayohusu afya na usalama wao, niliona kuna haja ya kuonana na uongozi ili niweze kufahamu zaidi changamoto za kiusalama na afya zinazowagusa watu wenye ulemavu na hivyo kuweka mikakati madhubuti ya kuzitatua kwa kushirikiana na Osha," alisema Semuguruka.

Alisema kwenye mazungumzo na uongozi wa Osha alibaini kwamba wanafanya kazi kubwa na yenye changamoto nyingi ya kuhakikisha wafanyakazi wanakuwa katika hali ya usalama zaidi.

"Kama kiongozi, nimeguswa sana na kazi yao na ningependa kutumia fursa hii kuwashauri viongozi wenzangu katika maeneo mbalimbali ya nchi waunge mkono juhudi hizi za Osha katika kuwalinda wafanyakazi dhidi ya vihatarishi vya kiusalama na afya ambavyo husababisha ajali na magonjwa katika sehemu nyingi za kazi," alisema Semuguruka.

Kaimu Mtendaji Mkuu wa Osha, Khadija Mwenda, alimshukuru Mbunge huyo kwa kukubali jukumu hizo alizopewa pamoja na jitihada ambazo ameanza kuzifanya ikiwamo kutembelea ofisi za Osha kwa ajili ya kuweka mikakati ya kutekeleza wajibu huo aliopewa.

# Bashungwa awapa neno usambazaji nishati jadidifu

**Na Elizabeth Zaya**

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa, amezitaka kampuni za usambazaji wa nishati jadidifu kuwavutia na kuwahimiza wenye viwanda vya vifaa vya nishati hiyo kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika sekta hiyo nchini.

Bashungwa alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki wakati akifunga maonyesho ya 14 ya nishati jadidifu yaliyofanyika jijini Dar es Salaam ambayo yaliandaliwa na wadau wa nishati hiyo Tanzania (TAREA).

Alisema kutokana na kuongezeka kwa mahitaji na uelewa wa Watanzania kuhusu nishati hiyo, imesaidia kuongeza na kukuza soko lake na kwamba umefika wakati kwa wawekezaji kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika eneo hilo.

"Teknolojia ya nishati jadidifu inakua siku hadi siku, lakini vifaa vingi vinaagizwa kutoka nje ya nchi. Tunaomba wazalishaji watambue kwamba kwa sasa soko limekuwa la uhakika Tanzania, waje kuwekeza viwanda katika eneo hilo," alisema Bashungwa.

Alisema uwekezaji katika viwanda kupitia nishati hiyo, utakuza soko si Tanzania tu, bali hata katika nchi zote za Jumuiya ya Maendeleo, Kusini mwa Afrika (SADC).

"Isipokuwa ninachoona kwa sasa ni uwapo wa changamoto kwa wadau kushirikiana kushughulikia masuala yote yanayokwamisha upatikanaji rahisi, ueneaji na ongezeko la matumizi ya nishati hizi kwa wananchi wote hasa walioko vijijini," alisema Bashungwa.

Makamu Mwenyekiti wa TAREA, Prosper Magali, alisema changamoto zinazowakabili wadau na wasambazaji wa nishati hiyo jadidifu, ni kuingiliana katika matukio ya usambazaji na shughuli za uendelezaji wa miradi midogo ya kuzalisha umeme katika maeneo ya vijijini unaofanywa Wakala wa Nishati Vijijini (REA).

Changamoto nyingine alisema ni masharti magumu yaliyowekwa na taasisi za fedha ambayo yanawakwamisha wawekezaji binafsi kupata fedha za kuendeleza miradi.

"Tunaamini serikali ina nafasi ya kusaidia kutazama changamoto hii na kutafuta majibu ya kuisukuma sekta hii hususani kuhakikisha wawekezaji wadogo wanapata fedha katika taasisi za fedha ili wawekeze," alisema Magali.

Aliiomba serikali na wadau wote katika sekta ya miradi midogo ya uzalishaji na usambazaji umeme, kubainisha maeneo ambayo wawekezaji binafsi watafanya shughuli bila kuwa na wasiwasi wa mwingiliano na shughuli za usambazaji umeme zinazofanywa REA.



Meneja Msaidizi wa Masoko Kampuni ya Nabaki Afrika Ltd, Mukiza Mushumba (kulia), akifanyiwa mahojiano na mtangazaji wa kituo cha East Africa TV/Radio, Nasser Kingu, jijini Dar es Salaam wikiendi, katika kampeni ya Kibiashara Zaidi yenye lengo la kuhamasisha ukuzaji wa biashara nchini. **PICHA: EATV**

# Wahitimu udaktari wahimizwa uadilifu, bidii

**Na Romana Mallya**

WAHITIMU wa fani za udaktari, uuguzi na ustawi wa jamii katika Chuo Kikuu cha Kumbukumbu cha Hubert Kairuki (HKMU), wametakiwa kuwa mabalozi kwa kutoa huduma kwa uwadilifu, bidii na kwa kiwango cha juu ambacho kitasaidia maendeleo ya sekta ya afya.

Kaimu Mkuu wa chuo hicho, John Ulanga, aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akiwatunuku wahitimu 509 waliohitimu katika ngazi mbalimbali za elimu.

Alisema ubora wa taaluma wanayoitoa chuoni hapo inatambulika kitaifa na kimataifa na miongoni mwa wahitimu hao, mmoja ni kutoka Zimbabwe ambaye baba yake alimpeleka hapo kusomea udaktari baada ya kumaliza Shahada nchini Austaria.

Makamu Mkuu wa chuo hicho, Prof. Charles Mgone, alisema kati ya wahitimu hao, wanawake ni 298 na wanaume ni 211.

Alisema kati ya idadi ya wahitimu hao, 32 ni wa astashahada, 210 stashahada ya uuguzi, 56 shahada ya uuguzi, 201 shahada ya udaktari wa binadamu, wanane shahada ya uzamili ya udaktari wa binadamu,

Mmoja Shahada ya Uzamili ya Ustawi wa Jamii na mwingine aliyechukua Shahada ya Uzamili ya Sayansi ya Afya ya Jamii.

Alisema kwa mwaka wa masomo 2019/20 wanafunzi wapya waliodahiliwa ni 335 ambapo Stashahada ya Uuguzi 113, Shahada ya Uuguzi 31, Shahada ya Udaktari wa Binadamu 178, Shahada ya Uzamili ya Afya ya Jamii ni saba na Shahada ya Uzamili ya Udaktari wa Binadamu wapo sita.

Prof. Mgone alisema chuo hicho kinaendelea kufadhili masomo ya walimu kwa ngazi za uzamili na uzamivu ndani na nje ya nchi.

"Walimu watatu wamemaliza mafunzo ya uzamili na wengine saba wanasomea shahada ya uzamivu, saba shahada ya uzamili na wawili wanachukua mafunzo ya muda mfupi," alisema.

Prof. Mgone alisema ili kuendana na wingi wa wanafunzi, chuo kimeamua kujenga kampasi mpya ya Boko ambayo itatumia wataalamu na rasilimali za ndani ya nchi.

Alisema tafiti zilizofanyika mwaka huu zinahusu magonjwa ya kuambukiza hasa malaria na homa ya ini na yale yasiyoambukiza.

"Masuala mengine yaliyotafitiwa ni magonjwa ya wanawake na watoto na matizo ya ujana," alisema.

Pia alisema mwaka huu wataaluma wao wametoa machapisho 16 katika majarida ya kisayansi na wanafunzi wa uzamili wametoa ripoti za kisayansi.

"Baadhi ya machapisho ni pamoja na utafiti wa njia mpya za ugunduzi wa vimelea vya malaria mwilini mwa binadamu. Ukatili wa watoto unavyoleta matatizo ya kisaikolojia na msongo wa mawazo kwa vijana shuleni.

## HABARI KIMATAIFA

# Ripoti yawagawa wabunge Kenya

**NAIROBI,** Kenya

SIKU chache baada ya kuzinduliwa kwa ripoti ya maridhiano (BBI) nchini Kenya, wabunge wamegawanyika kuhusu utekelezaji wake.

Waasisi wakuu wa ripoti hiyo, Rais Uhuru Kenyatta na kiongozi wa upinzani, Raila Odinga walitarajia kuwa matokeo yake yangeleta mshikamano wa taifa na kuondoa misuguano ya kisiasa na kikabila.

Hata kabla ya maoni ya wananchi kusikilizwa, ripoti hiyo yaelekea kuwagawanya wanasiasa zaidi badala ya kuwaunganisha.

Walipokutana katika ukumbi wa Bomas, viongozi walionekana kuzungumza lugha ya umoja, lakini mwishoni mwa wiki kikundi cha wabunge 57 wa Mlima Kenya anakotokea Rais Kenyatta wameapa kuipinga kura ya maoni wakisema kuwa ni ghali mno kwa mlipa kodi.

**Nataka Raila awaambie Wakenya kwamba BBI na matarajio yake, amekosa yote, lazima akubali amepigwa chenga.**

Walisema kuwa taifa litahitaji shilingi bilioni 20 za Kenya kuandaa kura ya maoni. Fedha nyingine kama hizo zilitumika kuandaa ripoti yenyewe.

Msimamo wao unakwenda kinyume na azma ya Rais Kenyatta na Raila wanaotaka wananchi wahusishwe. Seneta Njeru Ndwiga alisoma mwafaka huo.

"Tunashikilia kuwa marekebisho yoyote ambayo yatafanywa kwa ripoti ya BBI, yanafaa kuongozwa na bunge. Tayari watu wetu wana mizigo mingi hivyo hawafai kuwekewa mzigo mwingine wa kura ya maoni," alisema Seneta Njeru.

Viongozi hao wanahoji kuwa bunge lina uwezo wa kuyafanyia marekebisho mapendekezo hayo bila ya kuwahusisha wananchi.

Hali ya wasiwasi inazidi kulikumba eneo hilo la Mlima Kenya, huku Rais Kenyatta akiwa kimya suala la urithi, baadhi ya viongozi wakielezea kutoridhika kwao na jinsi Rais Kenyatta, anavyomdhalilisha makamu wake.

Lakini ni matamshi ya Spika wa Bunge la Kenya, Justin Muturi ambayo yanavunja matarajio ya kundi linaloegemea upande wa Makamu wa Rais, William Ruto linalotaka ripoti hiyo ijadiliwe bungeni badala ya kuwahusisha wananchi.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa viongozi ambao wamejitokeza wazi kuelezea misimamo yao, hawajaonekana wakitoa hamasisho kwa wananchi kuhusu ripoti ya BBI, lakini wanaonekana kupigania maslahi yao binafsi kwenye majukwaa ya kisiasa.

Kwa viongozi wa chama tawala cha Jubilee wanasema kuwa ripoti ya BBI inalenga kumsaidia Rais Uhuru Kenyatta kumfanya Raila Odinga kusalia mamlakani baada ya kukamilisha utawala wake wa mihula miwili.

Aden Duale ni kiongozi wa chama cha Jubilee chenye wabunge wengi bungeni anasema:"Nataka Raila awaambie Wakenya kwamba BBI na matarajio yake, amekosa yote, lazima akubali amepigwa chenga".

Upande unaomuunga mkono Raila unataka nafasi ya Waziri Mkuu mwenye mamlaka kinyume na ilivyopendekezwa kwenye ripoti hiyo, ambapo atakuwa akichaguliwa na rais na anaweza akafutwa kazi wakati wowote na rais. **DW**



Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta akizindua ripoti ya maridhiano iitwayo BBI, nchini humo. **PICHA: AFP**

## Watu 14 wauawa kwa shambulio ndani ya kanisa

**OUAGADOUGOU,** Bukina Faso

WATU 14 wameuawa katika shambulio lililotokea wakati wa ibada katika kanisa la Hantoukoura, mashariki mwa nchi hiyo.

Imeelezwa kuwa waathirika wa shambulio hilo walikuwa wamehudhuria ibada katika kanisa hilo siku ya Jumapili.

Watu waliokuwa wanafyatua risasi hizo bado hawajafahamika na hata lengo lao bado halijawekwa wazi.

Mamia ya watu wameuawa katika taifa hilo katika miaka ya hivi karibuni na kundi la kigaidi la Jihadist, kutokana na mvutano wa kikabila na kidini haswa katika mpaka wa Mali. Taarifa kutoka serikalini zinasema kuwa watu wengi wamejeruhiwa.

Idara ya Usalama imeitaarifu chombo cha habari cha AFP kuwa watu wenye silaha ndio wamefanya shambulio hilo, na miongoni mwa waliofariki ni waumini akiwamo mchungaji na watoto.

Chanzo kingine cha habari kimesema kuwa watu hao waliokuwa wamebeba silaha walitumia pikipiki.

Oktoba, mwaka huu watu 15 waliuawa na wawili walijeruhiwa vibaya katika shambulio lililotokea katika msikiti.

Mashambulio ya kigaidi yameongezeka nchini Burkina Faso tangu mwaka 2015, na kusababisha shule nyingi kufungwa. Mgogoro kati ya nchi hiyo na nchi jirani ya Mali eneo ambalo wanamgambo wa kiislamu wamechukua eneo la kaskazini la nchi hiyo tangu mwaka 2012 kabla ya Jeshi la Ufaransa kuwaondoa. **BBC**

## Bunge Iraq lakubali kujiuzulu waziri mkuu

**BAGHDAD,** Iraq

BUNGE la Iraq limeukubali uamuzi wa Waziri Mkuu, Adel Abdul Mehd wa kujiuzulu baada ya wiki kadhaa za maandamano ya umwagaji damu dhidi ya serikali yake.

Mehdi ameamua kujiuzulu baada ya kiongozi mkuu wa waumini wa madhehebu ya Shia, Ayatollah Ali al-Sistani kulitolea wito bunge Ijumaa iliyopita lifikirie upya msimamo wake kuelekea serikali anayoiongoza ili kumaliza machafuko.

Kufuatia ridhaa hiyo ya bunge, Spika wa taasisi hiyo, Mohammesd a-Halbousi alimwomba Rais Barham Salih amteuwe waziri mkuu mpya.

Wabunge wanasema serikali ya Abdul Mehdi, ikiwa ni pamoja na waziri mkuu mwenyewe, wataendelea na wadhifa wao kwa muda hadi serikali mpya itakapoteuliwa.

Kwa mujibu wa Katiba ya Iraq, Rais Barham Salih atabidi kulishauri kundi lenye wawakilishi wengi zaidi bungeni limteue waziri mkuu mpya na kuunda serikali, hatua inayotazamiwa kudumu siku 15.

Vikosi vya Iraq vimewaua karibu watu 400, wengi wao vijana, waliokuwa wakiandamana bila ya silaha kuipinga serikali tangu Oktoba mosi iliyopita.

Zaidi ya mamia ya vikosi vya usalama wameuawa pia katika machafuko hayo.

Uamuzi wa kujiuzulu kwa Abdul Mehdi, hauonyeshi kumaliza maandamano ambayo lengo lake ni kuachana moja kwa moja na mfumo wa kisiasa unaotuhumiwa kuoza kwa rushwa na kuwatumbukiza wananchi walio wengi katika janga la umaskini.

Jana waandamanaji waliuchoma moto ubalozi mdogo wa Iran mjini Nadjaf, kwa mara ya pili katika kipindi cha wiki moja.

Maandamano yanaendelea mjini Baghdad na katika majimbo mengine ya kusini.

Waandamanaji wamezifunga njia ikiwa ni pamoja na ile inayoelekea katika bandari muhimu ya kusini. Vikosi vya usalama vimemuua mwanaharakati na kuwajeruhi wengine tisa karibu na daraja ya mji mkuu jana.

Katika mji wa Nassiriya, waandamanaji wawili wamefariki kutokana na majaraha walioyapata kufuatia machafuko ya awali dhidi ya polisi katika mji huo wa kusini. **DW**

# Mradi kuimarisha ulinzi rasilimali pwani, bahari

**Na Romana Mallya**

SHIRIKA la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira na Wanyamapori (WWF) Tanzania kwa kushirikiana na Serikali ya Ujerumani, wamezindua mradi wa Kuimarisha Usimamizi na Utunzaji wa Rasilimali za Pwani na Bahari wenye thamani ya Sh. bilioni 10.1.

Mradi huo wa miaka mitano ulizinduliwa jana jijini Dar es Salaam na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, ambaye ametaka uwe na tija kwa wananchi badala ya kuishia katika vikao na stadi.

WWF Tanzania kwa kushirikiana WWF ya Ujerumani chini ya Taasisi ya Blue Action Fund wamefanikiwa kupata fedha hizo ambapo kati yake, Sh. milioni 253 kimetolewa na WWF Uingereza na Wetlands International wamechangia Sh. bilioni 1.3.

Ulega alisema mradi huo utekelezaji wake ni wa kiwango cha kimataifa kijulikanacho kama 'Binadamu na Hifadhi'.

"Utekelezaji wake ni katika Wilaya ya Kibiti, Mafia, na Kilwa, moja ya Taasisi muhimu ni Shirika la WWF Ofisi ya Tanzania ambayo Wizara inalitambua na kuthamini mchango wake mkubwa wa kulinda rasilimali za uvuvi kuanzia miaka ya 1990 hadi sasa," alisema.

Ulega alisema kupitia miradi wanayoitekeleza WWF katika eneo la uvuvi mafanikio ni pamoja na kuanzisha eneo la usimamizi linalojumuisha Halmashauri watu lijulikanalo kama Uwanda wa bahari wa Rufiji-Mafia-Kilwa yaani (RUMAKI).

Alisema mafanikio mengine ni uanzishwaji wa vikundi 69 vya Shirikishi wa Rasilimali za Uvuvi (BMU) na Maeneo 17 ya Usimamizi wa Pamoja.

"Wametoa elimu ya ujasiliamali kwa jamii za wavuvi ambapo zaidi ya wanajamii 10,000 wamejiunga katika programu ya ujasiriamali na kuanzisha Vikundi 334 vya Kuweka na Kukopa (VICOBA)," alisema.

Pia alisema wamesaidia kuimarisha ukusanyaji wa takwimu za uvuvi baada ya kuanzisha mfumo wa kuzikusanya kwa kutumia simu za mkononi ambapo hadi sasa zaidi ya simu 100 zimetolewa kwa wakusanya takwimu.

Ulega aliwataka WWF kuwaelimisha watu wa Pwani kuhusu ufugaji wa majongoo wa baharini ambapo Zanzibar wanafanya hivyo na soko lake ni kubwa.

Alitaja changamoto zilizopo sekta hiyo kuwa ni pamoja na miundombinu hafifu ya kuhifadhi samaki inayochangia kuwepo kwa upotevu mkubwa wa samaki baada ya mavuno hususan kipindi cha mvua.

Nyingine aliitaja ni kuendelea kwa uvuvi haramu, ukosefu wa mitaji kwa wavuvi na soko la uhakika ya mazao ya uvuvi na uwekezaji mdogo kwenye sekta ya uvuvi hususan kwenye uvuvi wa bahari kuu na ukuzaji viumbe maji.

Naye, Meneja Mhifadhi Mkuu wa WWF, Dk. Simon Lugandu, alisema mradi uliozinduliwa ni mwendelezo wa kazi ambazo WWF imekuwa ikiwekeza kwa miaka zaidi ya 15 katika Pwani ya Bahari ya Hindi.

Alisema fedha hizo zinalenga kufanya kazi katika jamii za Pwani kuboresha miundombinu na kuongeza ufanisi wa kiutendaji wa eneo tengefu la bahari katika kisiwa cha Mafia na hifadhi ya mikoko Delta ya Rufiji.

"Mradi umelenga kuimarisha usimamizi na utunzaji wa rasilimali za pwani na bahari katika Wilaya za Kibiti, Mafia na Kilwa na pia kuimarisha usimamizi wa rasilimali katika Eneo Tengefu la Bahari katika kisiwa cha Mafia," alisema.

"Mchakato huu unaratibiwa na shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu, Sayansi na Utamaduni (UNESCO) kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (NEMC) chini ya Ofisi ya Makamu wa Rais," alisema.




Mkurugenzi wa Wateja wa Benki ya CRDB, Boma Raballa (katikati), akionyesha tuzo ya Benki Bora ya Mwaka -2019 kati ya benki zote nchini iliyotolewa na gazeti la Financial Times la London nchini Uingereza ambalo huandika habari za kibiashara baada ya benki hiyo, kuonyesha ufanisi mkubwa katika utoaji wa huduma zake katika sherehe iliyofanyika nchini humo. Wengine ni John Everigton (kulia) na Mhariri wa gazeti hilo, Michael Beurke (kushoto). **NA MPIGAPICHA WETU**

# Lukuvi amtumbua mkuu Idara ya Ardhi

**Na Friday Simbaya,** IRINGA

WAZIRI wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, amemvua cheo Mkuu wa Idara ya Ardhi ya Manispaa ya Iringa, Wilbert Mtongani.

Lukuvi amechukua hatua hiyo baada ya kubaini amefungua ofisi yake binafsi ambayo inashughulikia mambo ya ardhi kiasi cha kumfanya kupoteza muda mwingi wa kazi katika ofisi hiyo na kuipotezea halmashauri mapato.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara jana ambao lengo lake lilikuwa kupokea kero za ardhi katika mkoa wa Iringa, Lukuvi alisema amelazimika kuchukua hatua hiyo baada ya kuchukua muda wote wa kazi katika ofisi yake binafsi.

Pia alisema mtumishi huyo amekuwa akiwatoza wananchi kiasi kikubwa cha fedha kwa kushughulikia matatizo yao ya ardhi jambo ambalo limekuwa likiikosesha manispaa hiyo mapato yake halali.

Lukuvi aliitisha mkutano huo kwa lengo ya kupokea kero mbalimbali katika mkoa wa Iringa ndipo alishusha rungu kwa mtumishi wa ardhi kwa kumvua madaraka.

Awali, akimkaribisha Waziri Lukuvi, Mkuu wa Mkoa wa Iringa, Ally Hapi, alisema ofisi yake kwa kushirikiana na wataalamu imekuwa na utaratibu wa kudumu wa kushughulikia migogoro ya ardhi.

Hapi aliwaagiza wakuu wa wilaya wote mkoani Iringa watoke ofisini na kwenda kusikiliza kero za wananchi pamoja na kuzitatua ili kupunguza malalamiko.

**Lukuvi alisema amelazimika kuchukua hatua hiyo baada ya kuchukua muda wote wa kazi katika ofisi yake binafsi.**

# JSDS II kuwa chanzo cha taarifa mashauri kortini

**Na Mwandishi Wetu,** ARUSHA

JAJI Mkuu, Prof. Ibrahim Juma, amesema kuanzia Januari mosi, mwakani, taarifa zote za mashauri zitaanza kuchukuliwa rasmi kupitia Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Mashauri (JSDS II).

Akifungua rasmi mafunzo elekezi kwa majaji wafawidhi wa Mahakama Kuu ya Tanzania na baadhi ya majaji wa mahakama hiyo, Jaji Mkuu alisema utumaji wa takwimu kila mwezi kwenye madodoso, utakoma Desemba 31, mwaka huu.

"Kuanzia sasa hadi Desemba 31, mwaka huu, maandalizi muhimu yanayohusiana na maelekezo haya yafanyike ikiwamo kuhakiki usahihi wa taarifa za mashauri zilizoingizwa katika mfumo wa JSDS II na kuhakikisha kuwa mashauri yote yanaingizwa kwenye mfumo kama nilivyoelekeza kupitia nyaraka mbalimbali," aliagiza.

Washiriki 30, wakiwamo majaji wafawidhi na baadhi ya majaji wa Mahakama Kuu wanashiriki mafunzo elekezi yanayofanyika kwenye Ukumbi wa Mikutano wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) mkoani Arusha.

Jaji Mkuu alisema matumizi ya Tehama hayakwepeki, hivyo ni muhimu kwa kila mmoja kukumbatia teknolojia hususani katika zama hizi za mapinduzi ya teknolojia.

Aliwataka viongozi hao wa mahakama kuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha mfumo huo unafanikiwa kwa kuhimiza watumishi walio chini yao kuwajibika ipasavyo.

Prof. Juma aliongeza kuwa mfumo huo utasaidia upatikanaji wa taarifa sahihi za mashauri yakiwamo yaliyofunguliwa katika mahakama husika, yaliyosikilizwa na kumalizika na vilevile utasaidia kupunguza matatizo ya upotevu wa majalada ya kesi.

Alisema mfumo huo pia utawawezesha wananchi kufuatilia mienendo ya kesi zao kwa njia ya Tehama, hivyo akatoa wito kwa wananchi kutembelea mitandao ya mahakama ili kupata taarifa mbalimbali.

Mafunzo hayo ya siku tano yamelenga kuboresha utendaji kazi wa viongozi hao ambao ndiyo wawakilishi wa Jaji Mkuu katika maeneo yao ya kazi.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**IATHEMATICS TUITION.** Mlete kijana ·ako tufuatilie msingi wake wa isabati hadi pale shida ilipoanzia na uanza kuujenga tena upya. Wahusika i kuanzia darasa la tano hadi kidato ıa sita.Tuitions za majumbani inapatikana pia. Tupo Bunju Mwisho sm. Simu 0655.0754 617987

## KAZI /AJIRA

**Nafasi za kazi** ualimu masomo ya sst/diploma 0656490706/0784142792


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI BIDHAA YAKO

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz,

au piga simu: 0767 223311



## KUPOTEA KWA CHETI



**ASHA M. SULEIMAN** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.382/1** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia TUMEKUJA Sekondari mwaka 1981. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KW/RB/7659/2019.**

115540402

## KUPOTEA KWA CHETI



**ABDALLAH ADINANI MBAGA** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S/1038/0151** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia J.K. NYERERE Sekondari mwaka 2013. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/STA/RB/503894/2019.**

115540301

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**NATIONAL RANCHING CO. LTD.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC 981 CBZ.** Chassis No. **MD625AF75J1LA1125.** Engine No. **AF7LJ18A1464.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi **DOD/DOD/RB/511377/2019.**

115541402

## KUBADILI UMILIKI WA GARI

**BW. TYALLAMBULLA MPANDA MAKALLA** WA **SLP.1464 DODOMA** ANAFANYA UHAMISHO WA GARI **NO. T 669 AYE TOYOTA MARK 11 GX 110** KUTOKA KWA **KASSU HUSSEIN BACHU** KUJA KWA **TYALLAMBULLA MPANDA MAKALLA** .YEYOTE MWENYE PINGAMIZI ATOE NDANI YA SIKU 14 KUANZIA TAREHE YA TANGAZO HILI.

115541302

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**DANSTAN ALFRED KISHAKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA-GX100** yenye namba za usajili **T 607 BGF.** Chassis **No. GX1006016393,** Engine **No. IGEAA6393.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBE/RUJ/RB/427498/2019.**

115541202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**


**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 92 OF 2019**

### TANGAZO

**Ombi la: MARIAM GODFREY KUSAJA**
**Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu**
**JEREMIA GODFREY KUSAJA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo na wana nia ya kupinga au kuthibitisha uteuzi wa mwombaji wanaalikwa kufika mahakamani na kuhudhuria kesi, mnano tarehe 04/12/2019 ili kuwasilisha mapingamizi yao au la kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Imetolewa tarehe 20/11/2019.




115541602

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAMAKA**


**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI 2**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA DODOMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI NA. 86 OF 2019**

### TANGAZO

**Ombi la: TUMAINI ANDREA MATAGI**
**Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi Marehemu**
**NELSON JACKSON KIRALUGA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya marehemu huyo na wana nia ya kupinga au kuthibitisha uteuzi wa mwombaji wanaalikwa kufika mahakamani na kuhudhuria kesi, mnano tarehe 04/12/2019 ili kuwasilisha mapingamizi yao au la kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Imetolewa tarehe 20/11/2019.




115541502


Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa

Tupigie 0767 223311

Kwa Habari Motomoto usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku

NJOO UTANGAZE BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI MICHEZO

# COUTINHO HATAKI KUONDOKA BAYERN MUNICH



**MUNICH,** Ujerumani

KIUNGO Philippe Coutinho amesema angependa kubakia kucheza kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, Bayern Munich.

Coutinho anacheza kwa mkopo wa muda mrefu akitoka kwa mabingwa wa Ligi Kuu ya Hispania, Barcelona, lakini raia huyo wa Brazil bado hajawa na namba kwenye kikosi cha kwanza kwa miamba hao wa Bavaria.

Tangu alipoondoka Camp Nou na kutua pale kwenye dimba la Allianz Arena, Coutinho amefunga mabao matatu katika mechi 18 alizoichezea Bayern.

"Najihisi vizuri zaidi hapa," alisema Coutinho. "Nina mpango wa kubaki kwa mwaka mmoja zaidi na kuendelea kucheza hapa.

"Lakini kama kila kitu kitakuwa sawa, ningependa kubakia hapa."

Coutinho alitokea benchi wakati Bayern walipofungwa kwenye mchezo wa Bundesliga dhidi ya Bayer Leverkusen Jumamosi.

Ulikuwa mchezo wa kwanza wa kipigo kwa kocha Hansi Flick tangu achukue mikoba ya Niko Kovac aliyefukuzwa.

"Tunaelewa namna anavyotufundisha kwenye mazoezi," alisema Coutinho. "Mambo yanakwenda vizuri kwa sababu ya hilo.

"Flick anamfanya kila mtu kujihisi ni muhimu kwa timu na tuna furaha hapa, lakini tunajua kuna kazi kubwa ya kufanya."

# Ljungberg ajiaminisha Arsenal kumaliza 4 bora

**LONDON,** Engaland

FREDDIE Ljungberg anajiamini kwamba Arsenal ina ubora wa kumaliza kwenye nne bora katika Ligi Kuu ya England, baada ya kutoka sare na Norwich City kwenye mchezo wake wa kwanza kuiongoza timu hiyo.

Ljungberg alipewa nafasi ya kuwa kocha wa muda wa kikosi hicho cha 'Washika Bunduki' baada ya kufukuzwa kwa Unai Emery Ijumaa iliyopita.

Mchezaji huyo wa zamani wa Sweden alikiongoza kikosi hicho kwa mara ya kwanza Jumapili wakati kikilazimika kupata sare ya 2-2, huku mabao ya Arsenal yakifungwa na Pierre-Emerick Aubameyang pale kwenye dimba la Carrow Road.

Arsenal ipo nafasi ya nane kwenye msimamo na wamepitwa pointi saba na Chelsea wanaoshika nafasi ya nne, lakini alipoulizwa kama atafuzu kucheza Ligi ya Mabingwa Ulaya, Ljungberg, ambaye alishinda mara mbili taji la Ligi Kuu na mataji matatu ya FA, alijibu: "Kwa asilimia 100".

"Watu wanaachia pointi hapa na pale, hivyo kwa uhakika ni ligi ngumu," alisema. "Lakini bila shaka nafikiri Arsenal inaweza kumaliza kwenye nne bora.

"Sijui kama uliona wakati tukiwa nyuma kwa bao 1-0, wachezaji waliamua kupambana kwa nguvu. Hivyo naamini ubora wa wachezaji wangu."






# Conte ajivunia Inter Milan kileleni

**MILAN,** Italia

ANTONIO Conte anajivunia timu yake ya Inter Milan baada ya Nerazzurri hao kupaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, shukrani kwa ushindi wa 2-1 dhidi ya SPAL.

Mabao mawili ya kipindi cha kwanza kutoka kwa Lautaro Martinez yaliiweka Inter kileleni kwenye Uwanja wa San Siro Jumapili, ingawa Mattia Valoti alifunga la kufutia machozi kwa SPAL.

Na Conte baada ya mchezo huo alielezea namna alivyofurahia ushindi na kuiwezesha klabu hiyo kukaa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu.

"Tumekuwa tukifanya kazi kubwa tangu siku ya kwanza," alisema Conte akiambia Sky Sport Italia.

"Kurudi kileleni baada ya mechi 14 ni jambo la kujivunia, kwa sababu tunaijua safari tuliyokuwa tunaipitia.

"Katika wakati huu, ilitusaidia sisi nafasi nzuri, kwani tulicheza kwa kujiamini na tulipata ushindi ambao tuliutarajia.

"Tulifurahi zaidi baada ya kujua kwamba, Juventus wamepata pointi moja baada ya kutoka sare. "Tulistahili ushindi dhidi ya SPAL na ni muhimu kukumbuka kwamba, tulipambana kuhakikisha tunapata ushindi huu, hivyo hatujaribu kujilinganisha na wengine."

# Simeone: Siwahofii Barca wala Madrid

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone amesema kwamba hahofiii kuhusu Barcelona na Real Madrid, badala yake yeye anaifikiria zaidi Sevilla baada ya Atletico Madrid kupoteza mchezo wake wa Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, juzi Jumapili.

Atletico ilifungwa bao 1-0 na Barcelona, shukrani kwa bao la Lionel Messi alilolifunga dakika ya 86.

Matokeo hayo yaliiacha Atletico nafasi ya sita kwenye msimamo, wakipitwa pointi sita na mabingwa wa LaLiga, Barca na Madrid, na wakipitwa pointi tano na Sevilla iliyopo nafasi ya tatu.

"Barcelona na Real Madrid hawanipi hofu mimi," alisema Simeone akiwaambia waandishi wa habari.

"Sevilla ndio nawahofia, wamenipita pointi tano kwa sasa."

Atletico walionekana kuwa bora katika vipindi vyote viwili kwenye mchezo huo wa Jumapili uliochezwa jijini Madrid.

Hata hivyo, Atletico walishindwa kutumia nafasi walizozipata na hivyo kujikuta wakimaliza mchezo huo kwa kuambulia kipigo hicho.





# RAKITIC NJIAPANDA BARCA

**BARCELONA,** Hispania

IVAN Rakitic haelewi hali ilivyo ndani ya Barcelona, akisema kwamba anataka kucheza mechi nyingi zaidi na "hakuna sehemu bora" zaidi ya hapo kwa miamba hiyo ya LaLiga.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Croatia alianza mchezo wake wa pili msimu huu na wa kwanza tangu Septemba wakati Barcelona wakiibuka na ushindi wa 1-0 dhidi ya Atletico Madrid, juzi Jumapili.

Rakitic, ambaye amekuwa pale Barca tangu mwaka 2014, alisema alitaka kubaki Camp Nou, kama ataendelea kucheza.

"Sielewi hali ilivyo kwa sababu nataka kucheza. Kama nikipata nafasi ya kucheza, hakuna sehemu bora kama Barca," alisema akiliambia Gazeti la Marca.

"Nataka kufurahia kila siku na kama itakuwa hapa, itakuwa bora zaidi."

Rakitic ameshinda mara nne taji la Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga na moja la Ligi ya Mabingwa Ulaya tangu alipojiunga na Barcelona akitokea Sevilla.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, alisema Novemba kwamba, anahisi kama vile Barca wamechukua mpira wake, lakini kiungo huyo yupo tayari kuendelea kuipambania tena klabu hiyo.

"Nilisema kwamba, mpira wangu umechukuliwa kutoka kwangu kuonyesha kuwa kwa kiasi gani napenda soka," alisema Rakitic.

"Kama naweza kucheza, hakuna sehemu bora kama Barca. Ninachotaka ni kufurahia, na kuendelea kuwa kwenye ubora wangu kwa sababu nataka kuendelea kupigania klabu hii."

# Rodgers afunguka dau kutua Arsenal

**LONDON,** England

KOCHA wa Leicester City, Brendan Rodgers, amedokeza kiasi cha fedha anachotakiwa kulipwa kama akitakiwa na klabu nyingine, huku kukiwa na taarifa kwamba anahusishwa na kwenda kuchukua kazi pale Arsenal.

Rodgers ameripotiwa kuwa chaguo la kwanza la Arsenal kurithi mikoba ya Unai Emery aliyefukuzwa wiki iliyopita, huku ikidaiwa kwamba, kocha huyo wa zamani wa Liverpool na Celtic kwenye mkataba wake kuna kipengele kinachomruhusu kulipa pauni milioni 14 kwa klabu itakayomtaka.

Baada ya Leicester kuibuka na ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Everton na kukaa nafasi ya pili kwenye msimamo wa Ligi Kuu nyuma ya vinara Liverpool, Rodgers aliulizwa kuhusu uvumi wa kuhusishwa na Arsenal.

"Pengine kuna kipengele cha kiasi cha fedha za kuachiwa katika mikataba ya makocha wengi," alisema Rodgers, ambaye alijiunga na Leicester Februali mwaka huu akiiambia Sky Sports.

"Kwa upande wangu kwa wakati huu, tulikuwa na ushindi wa kuvutia. Akili yangu kwa sasa inaifikiria zaidi Leicester, nina furaha kuwa hapa tangu nilipofika.

"Najihisi vizuri na wachezaji wangu, bado tuna kazi kubwa ya kufanya. Mikataba ya makocha wengi ina kitu kama hicho, lakini kwa upande wangu akili yangu ipo kwa Leicester.

"Madhumuni yangu ni kuisaidia klabu, majukumu ambayo nimejiwekea kwa ajili ya klabu hii."



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# POGBA KUMUWAHI MOURINHO SPURS

## Solskjaer asema anatumai kumwona uwanjani kesho ama McTominay kwa kuwa...

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anatumai kumkaribisha tena dimbani ama Paul Pogba au Scott McTominay kwenye mechi ya Ligi Kuu wakitokea chumba cha majeruhi, watakapoivaa Tottenham ya Jose Mourinho kesho, Jumatano.

**Pogba na mchezaji mwenza wa United, kiungo McTominay hawakucheza mechi ya Jumapili wakati wakitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Aston Villa kwenye Uwanja wa Old Trafford.**

Nyota wa United, Pogba amekuwa nje ya kikosi tangu Septemba akiuguza jeraha la kifundo cha mguu, wakati McTominay naye alitonesha jeraha lake la kifundo cha mguu kipindi wakiibuka na ushindi dhidi ya Brighton & Hove Albion kabla ya mapumziko ya kimataifa.

Na wakati kocha wa zamani wa United, Mourinho - ambaye aliripotiwa kutofautiana na Pogba kabla ya kutimuliwa Desemba mwaka jana, akijiandaa kurudi Manchester na kikosi chake cha sasa cha Tottenham kesho, Solskjaer ametoa maendeleo ya majeraha ya viungo hao.

"Bado tunayo siku mbili na tunahitaji kumtazama kila mmoja hapa pia," Solskjaer aliwaambia wanahabari wakati alipoulizwa juzi kuhusu Pogba na McTominay.

"Tuna siku mbili (jana na leo) tu, ngoja tuone, lakini, natumai, tunaweza kumuona mmojawapo uwanjani. Wanafanya vizuri nyuma ya pazia."

United ipo katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu, pointi mbili nyuma ya washika nafasi ya tano, Spurs - ambao wameshinda mechi zote za Ligi Kuu tangu Mourinho alipotwaa mikoba ya kukinoa kikosi hicho kutoka kwa Mauricio Pochettino aliyetimuliwa mwezi huu.

Hadi sasa United imepoteza mechi nne na kutoka sare sita katika mechi 14 za Ligi Kuu ilizocheza msimu huu, na Solskjaer lazima awaandae vema wachezaji wake kuelekea kuivaa Tottenham nyumbani kabla kwenda kwenye 'Manchester dabi' katika Uwanja wa Etihad Jumamosi.

"Vijana hawa wataimarika na kujifunza kutokana na uzoefu huu," alisema Solskjaer. "Bila shaka sisi, kama Man United, kama klabu, hatupendi kuwa katika nafasi tuliyopo, lakini huo ndio ukweli sasa na tunaweza kuchukua tu mchezo mmoja kwa sasa.

"Tunayo Jumatano, tunayo mechi kubwa inakuja Jumamosi tena, hivyo vijana hawa wanatazama mbele kwa kila mchezo. Mara nyingine kutokuwa katika kiwango mfululizo kutatokea kwa vijana hawa wadogo, juu na chini.

"Unaona kwa muda mfupi tunacheza mpira wa kupendeza na wakati mwingine huwa wazi sana. Tunashindwa kumiliki mpira wakati mwingine, lakini hatuwezi kufanya lolote kuhusu hilo sasa."

## ZISIKUPITE

### RODGERS AFUNGUKA ARSENAL

BRENDAN Rodgers, anahusishwa na nafasi ya kuinoa Arsenal, na amefunguka kuwa kuna kipengele kinachomruhusu kuuvunja mkataba wake kwa pesa hapo Leicester City. ***(Mirror)***

### JUVE YAMKANA RAKITIC

MKURUGENZI wa Juventus, Fabio Paratici amefunguka kwamba klabu hiyo haivutiwi kumsajili kiungo wa Barcelona, Mcroatia Ivan Rakitic, 31. ***(Mail)***

### JUVE HAIJAAMUA KWA RUGANI

JUVENTUS bado haijaamua endapo imuuze beki Mturuki Merih Demiral, 21 - anayehusishwa na Manchester United, Manchester City pamoja na Arsenal - ama imuweke sokoni kiungo Mtaliano Daniele Rugani, 25, anayeaminika kuwindwa na Arsenal, Wolves na West Ham. ***(Calciomercato)***

### CITY KUMKOSA SOYUNCU

BEKI wa Leicester City, Mturuki Caglar Soyuncu, 23, anayehusishwa na Manchester City, hataondoka Uwanja wa King Power mapema, wakala wake amesema. ***(Leicester Mercury)***

### BARCA YAJIPANGA KWA WEIGL

BARCELONA inaweza kumtazama kiungo Mjerumani Julian Weigl ili kuisaidia kuimarisha idara ya kiungo katika majira ya joto, wakati huu miamba hiyo ya Catalunya ikipanga kumfuata na pauni milioni 21, mchezaji huyo wa Borussia Dortmund. ***(Mail)***

### AUBAMEYANG AWINDWA INTER

MSHAMBULIAJI wa Arsenal, Mgabon Pierre-Emerick Aubameyang, 30, yupo katika mipango ya Inter Milan kuelekea dirisha la usajili la Januari. ***(Star)***

### COUTINHO ANOGEWA BAYERN

KIUNGO mshambuliaji wa zamani wa Liverpool, Mbrazil Philippe Coutinho, 27, ambaye anaichezea kwa mkopo Bayern Munich akitokea Barcelona, anatumai kubaki jumla na miamba hiyo ya Ujerumani. ***(Marca)***

### POCHETTINO AMTIBULIA EZE

NDOTO za kiungo wa QPR na England U-21, Eberechi Eze, za kujiunga na Tottenham zinaweza kuwa zimetoweka kufuatia kuondoka kwa kocha Mauricio Pochettino. Chelsea, Leicester City na West Ham pia zimekuwa zikimtazama kwa karibu mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 21. ***(Sun)***

### LIVER, UNITED KWA CHERKI

LIVERPOOL imejiunga katika mbio moja na Manchester United pamoja na Manchester City kumfuatilia mshambuliaji wa Lyon, Mfaransa Mathis Rayan Cherki, 16, ambaye tayari ameshacheza mechi yake ya kwanza Ligue 1 na Ligi ya Mabingwa Ulaya. ***(90 Min)***

### AMPAGAWISHA SOLSKJAER

KOCHA wa Ole Gunnar Solskjaer, amesifu kiwango kilichoonyeshwa na kiungo mshambuliaji wa Aston Villa, Jack Grealish wakati wakitoka sare dhidi Manchester United juzi, lakini hakuwa wazi kuhusu uwezekano wa kwenda kumsajili mchezaji huyo Muingereza mwenye umri wa miaka 24. ***(Metro)***

## Tanzania ya tatu kuogelea Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

TIMU ya Taifa ya mchezo wa Kuogelea ya Tanzania, imeshinda Kombe la Shaba baada ya kumaliza katika nafasi ya tatu kwenye mashindano ya Kanda ya Tatu Afrika yaliyomalizika juzi jijini Nairobi, Kenya.

Tanzania iliwakilishwa na waogeleaji 25 ambao walishindana na wanamichezo wengine kutoka katika nchi tisa za Afrika kwa kukusanya jumla ya pointi 2,044.

Wenyeji Kenya ndio waliibuka washindi wa kwanza kwa kupata pointi 2, 447 na kufuatiwa na Uganda iliyopata pointi 2, 392.

Mbali ya kushinda nafasi hiyo, waogeleaji watatu wa Tanzania, Sydney Hardeman, Romeo Mihaly na Sylvia Caloiaro walishinda vikombe kwa kushika nafasi ya kwanza kwa waogeleaji wa makundi ya umri mbalimbali.

Sydney alipata pointi 130 kwa waogeleaji wenye miaka kati ya 11 na 12 wakati Romeo alikusanya pointi 118 katika umri huo huo na Sylvia alipata pointi 126.

Kwa mujibu wa matokeo hayo, waogeleaji wa kike wa Tanzania waling'ara zaidi kwa kumaliza katika nafasi ya pili kwa kukusanya pointi 1,083 huku wenyeji, Kenya wakishika nafasi ya kwanza kwa kupata pointi 1,180 na Uganda katika nafasi ya tatu kwa kupata pointi 851.

Kwa upande wa wanaume, Tanzania ilikusanya pointi 865.5 na kushika nafasi ya tatu nyuma ya Kenya iliyomaliza ya pili kwa kupata pointi 1,143.50 na Uganda iliyokuwa ya kwanza kwa kupata pointi 1, 421.

## Mjini Magharibi yapania riadha Dar

**Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

TIMU ya Riadha ya Wanawake ya Mkoa wa Mjini Magharibi, inatarajia kuondoka nchini Desemba 5, mwaka huu kuelekea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya kushiriki mashindano ya riadha yanayojulikana kwa jina ya JEICA.

Mashindano hayo yanatarajiwa kufanyika kuanzia Desemba 7 hadi 9, mwaka huu na yatatumika kupata timu ya Tanzania ambayo itakwenda kushiriki Michezo ya Olimpiki mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Masoud Tawakar, alisema amewaandaa vizuri wanariadha wake na anaamini watapeperusha vema bendera kwa kutetea ubingwa walioutwaa mwaka jana.

Tawakar alisema kikosi hicho chenye wanariadha 10, wote wakiwa wanawake kinafanya mazoezi kila siku kwenye Uwanja wa Amaan, huku kukiwa na changamoto ya kukosa uwanja wakati wa jioni kutokana na mechi za Ligi Kuu Zanzibar zinazoendelea kwenye uwanja huo.

Hata hivyo aliwataka Wazanzibar kufuatilia mchezo wa riadha na kuacha kuwekeza nguvu zao kwenye soka peke yake.

# KARIA ACHUKUA FOMU KUWANIA URAIS CECAFA

**Na Somoe Ng'itu**

RAIS wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Wallace Karia, amejitokeza kuwania Urais wa Baraza la Soka Afrika Mashariki na Kati (Cecafa), ambalo linatarajia kufanya uchaguzi mkuu ifikapo Desemba 18, mwaka huu jijini Kampala nchini Uganda.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Karia, alisema amefikia uamuzi huo baada ya kuombwa na marais wenzake wa nchi wanachama na kuamini ana uwezo wa kutoa mchango wake katika kuongoza baraza hilo.**

Karia alisema anaamini akichagulia kuliongoza baraza hilo, atahakikisha malengo ya Cecafa yanakamilika, ikiwamo kupandisha viwango vya nchi wanachama.

"Nimeshajaza fomu na kuirudisha, na kama nitakuwa mgombea peke yangu, basi sitapigiwa kura, mkutano mkuu utaniidhinisha moja kwa moja, naamini marais wenzangu, hawatanigeuka, kwa sababu wameshaonyesha kuniamini," alisema Karia.

Katibu Mkuu wa Cecafa, Nicholas Musonye, alisema mbali na nafasi ya urais, alitaja nafasi nyingine zitakazowaniwa katika uchaguzi huo ni pamoja na Makamu wa Kwanza wa Rais, Makamu wa Pili wa Rais na wajumbe watatu watakaounda Kamati ya Utendaji.

Musonye alisema tayari nchi wanachama wa Cecafa wameshaanza maandalizi ya kuelekea katika mchakato huo, ambao anaamini utaongeza nguvu katika utendaji.

Alizitaja nchi wanachama zitakazoshiriki katika uchaguzi huo kuwa ni pamoja na Tanzania Bara, Zanzibar, Uganda, Kenya, Rwanda, Burundi, Ethiopia, Eritrea, Djibouti, Somalia, Sudan na Sudan Kusini.

Uongozi mpya utakaoingia madarakani, ndio utamteua Katibu Mkuu mpya ambaye atarithi mikoba ya Musonye, ambaye ametangaza kustaafu kiti hicho ifikapo Juni mwakani.

Musonye amekaa madarakani katika nafasi hiyo kwa muda wa miaka 20, akifanya kazi na marais watano akiwamo Leodegar Tenga wa Tanzania na Mutasim Gafaar kutoka Sudan ambaye anamaliza muda wake.




Mkuu wa Kitengo cha Masoko na Mawasiliano wa Benki ya Stanbic Tanzania, Desideria Mwegelo (kulia), akimkabidhi jezi za mpira wa miguu Meneja wa timu ya Waandishi wa Habari (TASWA FC), Hussein Omari katika hafla fupi ya makabidhiano iliyofanyika Mkao Mkuu ya Benki hiyo jijini Dar es Salaam jana. Hii ni hatua ya awali kuelekea mchezo wa kirafiki wa mpira wa miguu kati ya Benki ya Stanbic na TASWA FC unaotarajiwa kuchezwa Januari 2020. **NA MPIGAPICHA WETU**

# *Nyota Azam FC alalamikia ratiba*

**Na Shufaa Lyimo**

BAADA ya timu yake kulazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya JKT Tanzania, beki mkongwe wa Azam FC, Aggrey Moris, amesema mabadiliko ya ratiba ya mchezo huo ndiyo yamewafanya washindwe kupata matokeo mazuri kama walivyotarajia.

Mechi hiyo awali ilitarajiwa kuchezwa kuanzia saa 1:00 usiku, lakini ikiwa imebakia saa chache, walifahamishwa kwamba mechi hiyo itachezwa saa 10:00 jioni.

Moris alisema hali hiyo iliwachanganya wachezaji na wanakiri kwamba hawakujiandaa kucheza mchana.

"Ratiba ndio imetufanya tupoteze mchezo wetu, sisi tulijua tunacheza saa 1:00 usiku na siku zote tukafanya mazoezi yanayoendana na muda wa mchezo, matokeo yake tumeambiwa tunacheza saa 10:00 tukiwa hatujajiandaa, imetuchanganya sana," alisema Moris.

Alilitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kutofanya mabadiliko ambayo yanaathiri timu na hali hiyo inawafanya waamini wanafanyiwa "hujuma" hasa kutokana na kila timu imejiandaa kufanya vizuri ili isishuke daraja.

Hata hivyo, aliwaomba mashabiki wa timu hiyo waendelee kuwapa ushirikiano ili waweze kufikia malengo yao ya kutwaa ubingwa wa ligi hiyo msimu huu na kukata tiketi ya kushiriki katika mashindano ya kimataifa.

# Michezo

Jumanne Desemba 3, 2019

Nipashe




Pogba kumuwahi Mourinho Spurs HABARI UK.30

HESABU...



Mshambuliaji wa Yanga, David Molinga akipiga hesabu ya kuwatoka mabeki wa KMC kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa Taifa na kumalizika kwa sare ya bao 1-1 jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Mwakinyo amrudia Matumla, ashukiwa

## ●●● Ruta, Abdallah 'Ustadhi' wamponda, atakiwa kuiga uungwana na uanamichezo wa Samatta, mwenyewe...

**Na Shufaa Lyimo**

WADAU mbalimbali wa mchezo wa ngumi wamemtaka bondia, Hassan Mwakinyo, kumwomba radhi bondia mkongwe hapa nchini, Rashid Matumla "Snake Boy" kutokana na kitendo chake cha kumponda kutokana na uchambuzi aliokuwa akiufanya wakati wa pambano lake dhidi ya Mfilipino Arnel Tinampay likiendelea.

**Licha ya Mwakinyo kujirekodi na kusikika katika mitandao mbalimbali akimkashifu Matumla, baada ya mkongwe huyo kutoa maoni yake wakati pambano likiendelea Ijumaa iliyopita na muda mfupi baada ya kutangazwa kuibuka na ushindi, bado alisikika kupitia redio moja jijini Dar es Salaam akiendelea kumponda mkongwe huyo.**

Kupitia redio hiyo, Mwakinyo alisema Matumala alipewa nafasi hiyo ya uchambuzi ili apate hela ya kula, lakini ameitumia vibaya na kuwafanya watu wakiwamo mashabiki wake wengi kutoka kwao mkoani Tanga kuamini kwamba alibebwa dhidi ya Mfilipino huyo.

"Siku nyingine Azam Tv wakiandaa pambano wasimtumie Matumla kama mchambuzi, amefanya wengi waamini nilibebwa, kwanza kamkosea sana kocha wangu," alisema Mwakinyo.

Katika sehemu ya uchambuzi wa Matumla wakati pambano hilo likiendelea, alisema Mwakinyo anapaswa kutomruhusu Tinampay kumpeleka hadi kwenye kamba, lakini asikubali kushambuliwa sana tumboni na kwenye mbavu maana itamsababishia kupoteza nguvu.

Aidha, Matumla aliendelea kuchambua kuwa, hadhani kama kocha wa Mwakinyo alifuatilia ipasavyo namna mpinzani wake huyo, Tinampay anavyocheza na kuweza kumwandaa vema bondia wake kuelekea pambano hilo lililofanyika katika Uwanja wa Uhuru.

Hata hivyo, Matumla alivyotakiwa kujibu hoja ya Mwakinyo, alisema kama bondia huyo ametaka kuombwa radhi basi yeye anamwomba radhi na hataki malumbano katika hilo kwa kuwa alichokifanya ilikuwa ni uchambuzi na si vinginevyo.

"Kama anataka nimwombe radhi basi namwomba, yeye ni mfalme anataka kuwa mfalme muache awe mfalme," Matumla alijibu kiungwana.

Kwa upande wake Katibu Mkuu wa Chama cha Ngumi za Kulipwa Tanzania (PST), Anthony Ruta, amesema Mwakinyo yeye ndiye anatakiwa amwombe radhi Matumla kutokana na kumkosea mkongwe huyo, kwa sababu alichokizungumza ni kwa ajili ya kumjenga na si "kumponda" kama ambavyo inadaiwa.

Ruta alisema kuwa hajafurahishwa na maneno aliyoyatoa Mwakinyo, na kuongeza kwamba bado ni bondia anayekua hivyo anahitaji kusikiliza ushauri kutoka kwa mabondia wengine waliomtangulia.

"Kiukweli sijafurahishwa na maneno aliyoyatoa Mwakinyo, cha msingi amtafute Matumla amuombe radhi kwa matokeo yote yasiyopendeza ambayo ameyasema," alisema Ruta.

Yassin Abdallah "Ustadhi", mratibu wa mapambano mbalimbali ya ngumi nchini, alisema Mwakinyo hakupaswa kutoa "maneno machafu" kwa Matumla hata kama angeshindwa pambano hilo.

"Mimi nashauri Mwakinyo amtafute Matumla kwa lengo la kumuomba radhi, yeye bado safari yake ndio imeanza, Matumla ni mkongwe na amepigana zaidi ya mapambano 50, hata kama nyota yake imeng'aa mapema ni bahati, hapaswi kumtukana Matumla," alisema Ustadhi.

Wadau wengi waliochangia mada hiyo walisema Mwakinyo anapaswa kuiga uungwana kama wa mshambuliaji na nahodha wa Taifa Stars, Mbwana Samatta ambaye baada ya kukosolewa sana kuwa aliboronga katika mechi mbili za kuwania kufuzu Afcon 2021 dhidi ya Equatorial Guinea na Libya alijibu kiungwana.

"Awe mwanamichezo kama Samatta, tazama alivyokubali kukosolewa na kusema ameyapokea maoni ya Watanzania na kuahidi kuyafanyia kazi, huo ndio uanamichezo na si kubishana na wachambuzi na mashabiki," alisema Juma Mmary.

Hashimu Kondo, yeye alisema: "Hata Messi [Lionel] wa Barcelona, huwa anakosolewa sana anaposhindwa kuisaidia Argentina, lakini kamwe humsikii akibishana na wachambuzi na mashabiki, halafu huwezi kusema mashabiki wako wa Tanga, wakati waliokuwa wakikushangilia ni Watanzania wote."

## Yanga yakwamia Kinondoni usiku

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

BAADA ya ushindi wa mechi tano mfululizo, Yanga jana ilikwama kwa bao la penalti ya 'usiku' [dakika za majeruhi] dhidi ya timu ya KMC inayomilikiwa na Manispaa ya Kinondoni jijini Dar es Salaam kwa kulazimishwa sare ya bao 1-1.

Bao la mkwaju wa penalti la dakika ya tatu ya nyongeza ikiwa imesalia dakika moja tu, lililofungwa na Abdul Hillary liliinyima Yanga rekodi ya kushinda mechi ya sita mfululizo inayoshikiliwa na Simba msimu huu.

Kelvin Yondani alimuangusha kwenye eneo la hatari winga Hassan Kabunda na mwamuzi Elly Sasi kuamuru 'tuta' lililopigwa kiufundi na mchezaji huyo, hivyo kuinyima Yanga pointi tatu ambazo ilionekana kama inataka kuondoka nazo ili kufikisha alama 19, lakini ikajikuta ikiambulia moja hivyo kufikisha pointi 17 ambazo zinaifanya kupanda hadi nafasi ya nane kutoka ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Hiyo ilitokana na mtokea benchi, Mrisho Ngassa kufunga bao dakika ya 75 baada ya kuwazidi mbio mabeki wa KMC na kuupachika wavuni.

Hata hivyo, KMC itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kuibuka na ushindi kwenye mechi hiyo kutokana na kuonekana kutawala mechi hiyo muda mwingi wa mchezo huo. Kama KMC ingefungwa, straika Ramadhani Kapera ndiye angepaswa kulaumiwa kwa kukosa mabao matatu ya wazi.

Dakika ya pili tu ya mchezo, KMC ilipeleka salamu kwenye lango la Yanga, baada ya Ramadhani Kapera kuwatoka mabeki wa Yanga na kubaki na kipa Farouk Shikalo, lakini kwa mshangao wa wengi alipiga shuti mtoto lililodakwa kirahisi, huku akikosa mengine dakika ya 50 na 65 mpira ukigonga nguzo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >